

24 JUNI, 2013

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Hamsini na Tano - Tarehe 24 Juni, 2013

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza maswali. Atakayeuliza swali letu la kwanza ni Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe.

MHE. DKT. PUDENCIANA E. KIKWEMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante nami kupata nafasi ya kuuliza swali langu. Kwa kuwa leo Bunge lako Tukufu linatarajia kupitisha bajeti ambayo itaenda kutekeleza majukumu yake kuanzia mwezi ujao, sasa naomba swali langu namba 447 lipatiwe majibu kwa ajili ya Wananchi wa Mkoa wa Katavi, hususan Kata ya Majimoto.

SPIKA: Haya uhusiano wa kumaliza bajeti na swali lako uko wapi? *(Kicheko)*

24 JUNI, 2013

Na. 447

Maji Moto Katika Maeneo ya Kata ya Majimoto

MHE. DKT. PUDENCIANA E. KIKWEMBE aliuliza:-

Eneo lote la Kata ya Majimoto, Tarafa ya Mpimbwe lina maji yanayosadikiwa kuwa ni salama kwa matumizi ya binadamu, hivyo Wananchi wa maeneo hayo wanawajibika kununua maji kwa bei kubwa kutoka Kata ya Mamba yenye maji yanayotoka kwenye miamba ya Bonde la Ufa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hilo ili kuwapunguzia ukali wa maisha na adha wanayopata Wananchi wa Kata ya Majimoto?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pudenciana W. Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Kata ya Majimoto ina uhaba mkubwa wa maji safi na salama kwa ajili ya matumizi ya binadamu. Aidha, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, maji moto katika Kata ya Majimoto hayafai kwa matumizi ya binadamu. Serikali kwa kulitambua hilo, imeipa Kata hii kipaumbele katika Programu ya Maji kwa ujenzi wa miradi ya maji katika vijiji kumi kwa kila Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa kisima kirefu cha maji kimechimbwa katika Kata ya Majimoto kwa gharama ya shilingi milioni 19.85 mnamo mwaka 2011/2012. Aidha, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kumpata Mkandarasi wa kujenga mradi huo kwa mtandao wa bomba utakaopunguza tatizo la maji katika Kata ya Majimoto. Gharama za kutekeleza mradi huu ni shilingi milioni 256.813 na utakuwa na vituo vya kuchotea maji 18. Halmashauri

24 JUNI, 2013

imepanga kutumia shilingi milioni 526.813 katika mwaka 2013/2014 zikiwemo shilingi milioni 493.824 zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 na shilingi milioni 32.989 zilizoidhinishwa katika bajeti ya mwaka 2013/2014. Halmashauri ya Wilaya ya Mlele katika mwaka 2013/2014 imeidhinishwa shilingi bilioni 1.329 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji.

MHE. DKT. PUDENCIANA E. KIKWEMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

(i) Kwa kuwa fedha za kutekeleza mradi huu zilianza kutengwa kuanzia bajeti ya mwaka 2012/2013 kiasi cha shilingi milioni 493.8 na fedha hizo kwa bajeti ile hazikuweza kutumika. Je, ni kwa nini fedha zile hazikuweza kutumika?

(ii) Kama hazikutumika kwa sababu ya kukosa mkandarasi; ni lini mkandarasi huyo atapatikana na mradi huo utanza na kukamilika? Ahsante.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la msingi, Halmashauri ilishatengewa fedha shilingi milioni 515.9 kwa ajili ya kutekeleza mradi mzima wa maji ili kuifanya wilaya hiyo ipate maji. Shilingi milioni 493 ni zile ambazo zimeshaenda kwa utekelezaji na ndiyo sababu nimeeleza kwamba, mkandarasi anakamilisha taratibu zake ili kuhakikisha kazi hii inakamilika, ambayo itaweza kusambaza mtandao wa bomba na kuhakikisha Wananchi wanafaidika katika vile vituo 18 vya kupatia maji kwenye maeneo haya.

Kwa mwaka huu wa fedha, fedha ambayo ilikuwa imesalia kati ya mahitaji yao makubwa ilikuwa shilingi milioni 32 ambazo tayari zimeshawekwa kwenye mpango wa bajeti ya mwaka huu ili kwenda kukamilisha utaratibu huo. Jambo ambalo ninasisitiza Halmashauri kwenye eneo hili ni kuhakikisha utaratibu wa kukamilisha taratibu za

24 JUNI, 2013

mkandarasi yule unakamilika kwa haraka ili Mradi huo ukamilike pia kwa haraka na Wananchi waweze kupata huduma inayokusudiwa.

MHE. DKT. PETER D. KAFUMU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuiona. Pamoja na kwamba maeneo haya yenye maji moto kama Kata ya Majimoto hayafai kwa matumizi ya binadamu, lakini yanaweza kutumika kwa ajili ya kuzalisha umeme kwa teknolojia ya joto ardhi au *geothermal*. Kwa nini Serikali isifikirie jambo hili ili maeneo haya yote yenye maji moto ambayo yako kwenye Bonde la Ufa yatumike kuzalisha umeme? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya *Energy*? Haya Mheshimiwa Majaliwa, nadhani unaweza?

Waheshimiwa Mawaziri, tunapouliza maswali ninaweza kumwita Waziri yeyote ajibu swali lolote. Kwa mfano, swali la maji moto hapa na umeme, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, yako maeneo mengi nchini ambayo yana maji yasiyokuwa salama na siyo safi kwa matumizi ya binadamu. Kwa kuwa umeona ni muhimu na umeshauri Wizara husika kwa mambo ya umeme, ione kama inaweza kutumia maji haya ambayo siyo salama kwa ajili ya kuanzisha miradi ya umeme. Kwanza ni lazima kuwe na tathmini itakayofanywa kwenye maeneo hayo ili kuona kama maji hayo yanatosha kuweza kusukuma mitambo ya kuzalishia umeme ili sasa mpango huo uweze kukamilika. Kwa maana hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), itawasiliana na Wizara ya Nishati na Madini, ili kuweza kutambulisha maeneo hayo, waende kuona kama jambo hili linawezekana katika maeneo hayo na Serikali ipo tayari kufanya kama ambavyo Mheshimiwa Kafumu ameshauri.

24 JUNI, 2013

SPIKA: Ndiyo Mheshimiwa Waziri ungeweza kujibu wewe moja kwa moja, mmh! (*Kicheko*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nimsaidie ni kwamba, umeme ule hauendani na wingi wa maji, haya ni maji ambayo yako chini ya ardhi. Kwa kuongezea tu ni kwamba, Wizara yangu katika vyanzo vya umeme kwa ajili ya Taifa letu hiyo joto ardhi *geothermal* ni eneo mojawapo. Tuna maeneo zaidi ya 15, kwa bahati mbaya au nzuri yalikuwa yamechukuliwa na watu binafsi na hao walikuwa ni watu wa kati waliokuwa wanatafuta wawekezaji wakiwadai kati ya dola milioni 5 na 20.

Mheshimiwa Spika, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, maeneo yote hayo tumeyachukua yamerudi Serikalini ili tupate wawekezaji wa uhakika. Sasa kinachofanyika ni kwamba, *Geological Survey* ya Tanzania imefanya utafiti, tumegundua kuna maeneo matatu ambayo tunaweza tukaweka mitambo ya kuzalisha umeme kutokana na joto ardhi na eneo ambalo ni zuri sasa hivi ni Ziwa Ngozi kule Mbeya. Kinachofanyika ili kujua eneo hilo linafaa kwa ajili ya umeme ni lazima tuwe na nyuzi za joto (*temperatures*) kati ya *degrees* 220 – 250 na tunafanya *drilling*. Mwaka huu tunachoronga kisima cha kwanza ambacho kitatupatia taarifa kama joto lile linatosha. Hata hivyo, joto ambalo tayari lipo juu ya ardhi ni zaidi ya nyuzi 120, kwa hiyo, eneo hilo linafaa sana.

Mheshimiwa Spika, kampuni kubwa za Japan na Iceland zimeomba kuja kuwekeza, kwa hiyo, tunaachana na wawekezaji ambao wanazunguka na miradi mfukoni na tunaenda kwa wale wenye fedha na utaalim.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaitumia. (*Makofi*)

SPIKA: Wale wote wenye maeneo yenye maji moto mwende mkaulize kama na maeneo yenu yatafaa. Tumetumia dakika 12 kwa swali hili, kwa hiyo, tunaendelea na swali linalofuata ambalo litaulizwa na Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye.

24 JUNI, 2013

Na. 448

Fedha za Matengenezo ya Barabara za Rungwe

MHE. CYNTHIA H. NGOYE aliuliza:-

Wilaya ya Rungwe hupata mvua nyingi sana zinazopelekea kuharibu barabara kiasi cha kupitika kwa tabu na kutopitika kabisa wakati wa masika:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimekuwa kikitengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Wilaya hiyo kuanzia mwaka 2010/2011 – 2012/2013?

(b) Je, fedha kiasi gani zimekuwa zikitolewa kila mwaka?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwaka 2010/2011 kiasi cha shilingi milioni 783.28 zilipokelewa na Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye jumla ya urefu wa kilomita 260; ambapo zilikuwemo shilingi milioni 203.1 kwa ajili ya matengenezo ya kilomita sita za maeneo korofi Barabara ya Igongwe – Mbeje.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011/2012 kiasi cha shilingi milioni 709.39 zilipokelewa na Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye jumla ya urefu wa kilomita 274.1; Mwaka huu wa Fedha wa 2012/2013 zilitengwa shilingi milioni 659.12, ambapo shilingi milioni 497.68 sawa na asilimia 75.5 zimeshapokelewa na matengenezo ya barabara zenye jumla ya urefu wa kilomita 122.3 yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 1.128 kwa ajili ya matengenezo ya barabara; kati ya hizo shilingi milioni 700 ni kwa ajili ya ujenzi wa kilomita mbili za barabara za lami katika Mji wa Tukuyu ili kurahisisha upitikaji wakati wa mvua nyingi.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyofafanua katika kipengele (a), fedha zilizopelekwa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kwa ajili ya matengenezo ya barabara ni shilingi milioni 783.28 mwaka 2010/2011, shilingi milioni 709.39 mwaka 2011/2012, shilingi milioni 659.12 zimepangwa mwaka huu 2012/2013 na shilingi bilioni 1.248 zimetengwa mwaka huu wa fedha wa 2013/2014. Kwa miaka minne zitakuwa zimepelekwa jumla ya shilingi bilioni 3.399 kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninamshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Hata hivyo, pamoja na majibu hayo ninaomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Pamoja na viwango hivi ambavyo Mheshimiwa Waziri amevitaja kutolewa, ikumbukwe Wilaya hiyo kama nilivyosema katika swali la msingi, ina mvua nyingi sana na ni eneo lenye milima mirefu na vivuko vingi. Fedha hiyo ambayo imekuwa ikitolewa ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji ya utengenezaji wa barabara katika maeneo hayo ambayo mvua inafikia kiwango cha mm 2500 – 2800 kwa mwaka.

(i) Kwa kuwa fedha inayotolewa ni sawa na ile inayotolewa katika Wilaya ambazo zina mabonde; je, Serikali sasa iko tayari kuifikiria Wilaya hii ambayo ina mvua nyingi kwa kuipatia fedha zaidi ukilinganisha na wilaya nyingine?

(ii) Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Serikali iliiongezea wilaya hii zaidi ya shilingi bilioni 150 kwa ajili ya

24 JUNI, 2013

kutengeneza barabara zake, lakini mpaka leo fedha iliyotolewa ni shilingi bilioni 110 tu; ni lini sasa fedha hiyo itatolewa ili barabara zake zitengenezwe?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nieleze kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inaratibu karibu matengenezo ya barabara zote za ngazi ya Wilaya nchi nzima kwa kilomita zaidi ya 58,000 kila mwaka. Fedha ambayo tunaitenga tunajaribu kuigawa katika Halmashauri zetu kulingana na uharibifu wa barabara zilizopo kadiri msimu wa mvua unavyokuwa. Kwa maana hiyo sasa, kama ambavyo tumetenga fedha hizi kama nilivyoeleza katika swali la msingi, bado tunahitaji na tunaweza kutuma na fedha hizi zitakapotumwa kama kuna uharibifu wa ziada, basi Halmashauri inashauriwa kutuandikia Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) maombi maalum kulingana na uharibifu uliojitokeza msimu huu wa mvua ili tuweze kuwaongezea fedha kwa ajili ya matengenezo.

Mheshimiwa Spika, juu ya fedha ambazo tulikuwa tumeshatenga katika kipindi kilichopita, sasa zimeingizwa kwenye mpango wa mwaka huu ili kuona ukarabati ule unaendelea vizuri na kwamba, fedha hizo zitakapokuwa zimepungua kadiri ambavyo tunazikusanya, tunaweza pia kuifikiria Halmashauri hii ya Rungwe ili iweze kupata fedha kwa ajili ya kukamilisha Miradi yake yote.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Kama ilivyo kwa Wilaya ya Rungwe, Kyera na maeneo mengine, Wilaya ya Ileje pia ina hali ya mvua nyingi wakati wote wa mwaka kasoro miezi mitatu katika mwaka mzima. Pia yapo maeneo ya milima ambayo magari hayawezi kupanda wakati wa masika.

Ningependa kuuliza kama Serikali ipo tayari kuweka kwenye vipande vifupi vya mita 500, vingine mita 700, ambavyo vinazuia magari kwenda kuwahudumia Wananchi maeneo mbalimbali katika Wilaya ya Ileje?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara hizi ziko katika makundi manne ya namna ambavyo zinahudumiwa. Kwanza, kuna barabara za vijiji ambazo vijiji vyenyewe vinaratibu namna ya kuzikarabati vikipata ushirikiano na Halmashauri. Ziko barabara za wilaya ambazo pia Halmashauri ya Wilaya kupitia mipango yake na Mfuko wa Barabara huwa zinawekewa mpango wake. Pia ziko barabara za mkoa ambazo zinapita ndani ya wilaya kwenda wilaya nyingine ambazo pia zinaratibiwa na taasisi yetu inaitwa *TANROADS* kupitia Wizara ya Ujenzi na zile barabara kuu ambazo pia nazo zinaratibiwa na Wizara ya Ujenzi.

Sasa inapotokea barabara ndani ya Halmashauri hata kama ni ya mkoa imeharibika, wahandisi wa ndani ya Halmashauri wanashirikiana na wale wa *TANROADS* walioko kwenye mkoa ili kutathmini uharibifu wa barabara zilizopo ili kuona nani anaweza kuzitengeneza kulingana na mahitaji yaliyopo.

Kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi kwamba, Halmashauri inaweza kuona kiasi cha mvua kilichonyesha na kuharibu miundombinu yetu na wanaweza sasa wakabainisha mahitaji ya maeneo hayo ili Halmashauri kupitia Mfuko wa Barabara au Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROADS* iliyopo mkoani kwenye wilaya husika, tayari iweze kufanya tathmini tuweze kutoa fedha kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya barabara.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kuna maeneo yenye miteremko ambayo kwa namna yoyote ile fedha za kupitia Halmashauri haziwezi zikajenga barabara hizo zikapitika kama ilivyo kwa Kwateke, Tuli na Kidalu na maeneo mengine yenye milima na miteremko. Kwa nini Serikali isifanye tathmini maeneo ya aina hiyo na hizo barabara zikapewa upendeleo hata kama haziunganishi Mkoa kwa Mkoa ili ziweze kutengenezwa na Wananchi waweze kupata huduma ya barabara?

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa kupitia *Amendment Act* No. 2 ya mwaka 1998 na makarebisho yake ya mwaka 2006, Mfuko wa Barabara huwa unatoa fedha kwa ajili ya Halmashauri zetu za Wilaya. Fedha hizo pia huwa zinatolewa kwenye Wizara ya Ujenzi kwa ajili ya *TANROAD* ili zitumike kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

Napenda nitoe wito, Waheshimiwa Wabunge pamoja na Halmashauri zetu zote zinazopokea fedha za Mfuko wa Barabara, kwa sababu fedha zinapopeleka kule kwenye Halmashauri siyo fedha zote wanazitumia kwa wakati unaotakiwa katika kutengeneza barabara. Katika ripoti iliyotolewa na Meneja wa Mfuko wa Barabara mwezi huu katika fedha zote zilizopeleka kwenye Halmashauri ya Wilaya katika awamu ya kwanza, awamu ya pili na awamu tatu, kuna Halmashauri 103 zimetumia kati ya asilimia zero na asilimia 36.4 ya fedha zilizopeleka kule. Halmashauri 22 tu ambazo zimetumika fedha kati ya asilimia 50 hadi asilimia 90.4 na bahati nzuri Halmashauri ya Mheshimiwa Kibona nilikuwa najaribu kuangalia hapa, imetumia asilimia 51.76. Wakati Halmashauri ya Rungwe imetumia asilimia 36 na ina milioni 315 hazijatumika mpaka sasa hivi. Kwa hiyo, nitoe wito kwa Halmashauri zetu na Wakurugenzi wote, wafuate masharti ya matumizi ya fedha za Mfuko wa Barabara ili fedha zinazotumika kule ziende zikatumike kwa kazi zilizopangwa kwa ajili ya kutengeneza barabara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya barabara ambazo zipo kwenye miinuko na kadhalika. Bahati nzuri kupitia Mwenyekiti wa *Road Fund*, Dkt. James Wanyancha, tunafanya ukaguzi sasa katika barabara zote na kuangalia ile hali ya barabara zingine zenye miinuko na mabonde makubwa ziweze kupangiwa fedha nyingi zaidi kuliko maeneo mengine ambayo yana barabara nzuri zaidi za Halmashauri. (*Makofi*)

SPIKA: Hamuwezi kuamini maswali mawili tu yametumia dakika 20. Sasa naenda kwa *speed*, naendelea na swali linalofuata; Mheshimiwa Rita Mlaki!

24 JUNI, 2013

Na. 449

Misaada Kutoka Taasisi Mbalimbali

MHE. RITA L. MLAKI aliuliza:-

Taasisi zisizo za Kiserikali na Mashirika ya Kigeni hushiriki katika huduma za kijamii kama kujenga shule na zahanati na baadaye huvikabidhi kwa Serikali ya Mtaa husika:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka walimu na wauguzi katika shule na zahanati hizo?

(b) Je, kwa nini Serikali isizisaidie taasisi hizo ili zilipe kodi za vifaa vinavyoletwa kama msaada kutoka nje?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na inaunga mkono jitihada zinazofanywa na Taasisi zisizo za Kiserikali na mashirika ya kigeni katika kutoa huduma za kijamii kama vile ujenzi wa shule na zahanati na kuikabidhi mikononi mwa Serikali. Serikali imekuwa ikipeleka watumishi wakiwemo walimu katika shule mbalimbali ambazo zimejengwa kwa ufadhili na baadaye kukabidhiwa Serikalini. Mifano ya shule ambazo zinanufaika na utaratibu huu ni Shule ya Sekondari Chifu Ihunyo, yenye walimu 18 na Shule ya Sekondari ya Oswald Mang'ombe, yenye walimu kumi zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, Shule ya Sekondari Rajani yenye walimu 13 katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Shule ya Sekondari Mwadui yenye walimu 14 na Shule ya Msingi Choba yenye walimu wanne katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu na Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Wama na Nakayama yenye walimu 11 iliyopo Nyamisati Wilayani Rufiji Mkoani Pwani.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali hutoa msamaha au nafuu ya kodi kwa Mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa vifaa na huduma, ambayo imelenga kutoa huduma bure kwa jamii. Kabla ya kuingiza vifaa, maombi yanapaswa kuwasilishwa kwa Waziri wa Fedha ambaye ndiye mwenye dhamana kwa ajili ya tathmini na idhini kulingana na taratibu zilizopo. Hivi karibuni Serikali imetoa msamaha wa kodi kwa vifaa vya michezo vilivyoingizwa nchini na Shirika lisilo la Kiserikali la *Sports Development Aid (SDA)*, kwa ajili ya kugawa bure kwenye shule ambazo zinafundisha somo la *Physical Education*. Jambo la msingi ni mashirika kuwa na mawasiliano na mamlaka husika kwa ajili ya ufahamu na taratibu na maeneo yanayostahili msamaha au unafuu wa kodi.

MHE. RITA L. MLAKI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu yanayotupa matumaini kutoka kwa Serikali. Ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Shirika la Afrika Amini Alama lililopo kwenye Momera huko Arusha limeanzisha zanahati pale Momera pamoja na kujenga shule mbili ya *Masai Vision* pamoja na Waleck, lakini mpaka tunavyoongea hivi sasa wameshindwa kupata misamaha ya kodi pale wanapoagiza vifaa kutoka nje, vya zanahati pamoja na mashule na vile hawajapata walimu katika Shule ya Waleck. Je, Serikali ina mpango gani kulisaidia Shirika hili kupata msamaha wa kodi na pia walimu katika shule ambazo wamezijienga na wamezikabidhi kwa Serikali kupitia PPP?

(ii) Kwa kuwa kuna hospitali nzuri sana kama Aga Khan ambayo inatuhudumia na inatupa huduma nzuri, tunaishukuru sana Serikali kwa msaada mkubwa inayoipa hospitali hii. Pia kuna hospitali nzuri kama hii inaitwa Regency ipo pale Dar es Salaam, haiipatii msamaha kabisa kwa sababu haijajiandikisha kama NGO. Je, Serikali ina mpango gani kuisaidia Hospitali ya Regency ili nayo iweze kupata msahama inapoleta vifaa vyake pamoja na madawa kama hospitali zingine nzuri kama Aga Khan?

SPIKA: Swali la kwanza anajibu Naibu Waziri na swali la pili atajibu Waziri wa Afya. Naomba ujibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kama taasisi iliyoko kule Moshi ilishawahi kutoa taarifa zake mapema kwenye Wizara husika kwa maana ya TAMISEMI, tunaweza sasa tukaona umuhimu na aina ya walimu na mahitaji yetu nchini ili kuweza kuruhusu walimu wengine kutoka nje kuja kwa ajili ya hilo. Walimu wa ndani tutaangalia pia shule ile ina mfumo upi na kama *syllabus* ni ile ile ambayo imethibitishwa na Wizara ya Elimu, sisi tupo tayari kupeleka walimu ili kuweza kuunga mkono jitihada za Taasisi hii ambayo imejenga kwa faida zake yenyewe.

Suala la hospitali pia ambalo amelieleza, tunayo maeneo ambayo tayari Serikali inapeleka waganga kwenye Halmashauri zetu kama vile *Millennium Challenge* iliyoko pale Ilolanguru kule Mkoani Tabora, ni eneo la mfano ambalo *Millennium Challenge* kama ni eneo ambalo limeletwa na wafadhili, tumeshapeleka madaktari pale kutoa huduma za afya kwenye hospitali zao.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya swali la pili.

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rita Mlaki, kama ifuatavyo:-

Kuhusu masuala ya kodi kwa hospitali; hospitali ambazo ni *not for profit* huwa zinapata msamaha wa kodi, lakini zile ambazo zinatengeneza faida, wanawajibika kulipa kodi stahili. Sasa ile ni kwa kodi kama *income tax* na kadhalika.

Tukija kwenye suala la vifaa, endapo vifaa vile, yaani *capital goods* zinahesabika kwa mujibu wa Sheria ya TIC kwamba hazistahili kutozwa kodi; kwa maana hiyo ni kwamba, hata Regency wanapoleta vifaa hivyo wanapaswa kuomba hiyo *certificate* ya TIC ili waweze kuingiza vifaa hivyo bila kodi yoyote. Nadhani hilo

24 JUNI, 2013

linawezekana na mimi nitapenda kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge, kuhakikisha kwamba tunakaa na Uongozi wa Regency ili kuwaelekeza utaratibu waweze kuleta vifaa hivyo bila kodi na waweze kutoa huduma kwa gharama nafuu zaidi.

SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata, tumetumia nusu saa kwa maswali matatu. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika Mheshimiwa Mustapha Akunaay na kwa niaba yake Mheshimiwa Joseph Selasini!

Na. 450

Mbegu na Mbolea Bora kwa Wakulima

MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY) aliuliza:-

Pamoja na kuwa na Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) lakini bado Wakulima wa Tanzania wameendelea kuuziwa mbegu na mbolea feki na kupata hasara sana:-

(a) Je, ni lini Serikali itawahakikishia Wakulima wa Tanzania upatikanaji wa mbegu na mbolea zenye viwango vya ubora?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuwalipa fidia Wananchi ambao wamepata hasara kwa kuuziwa bidhaa hizo feki?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mbunge wa Mbulu, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na changamoto ya uwezo, pembejeo zisizo na viwango na hivyo kuathiri uzalishaji na tija katika mazao ya kilimo. Ili kudhibiti ubora

wa mbegu, Serikali ilianzisha Taasisi ya Udhibiti na Uboru wa Mbegu (*Tanzania Official Seed Certification Institute – TOSCI*), ambayo inahusika katika kuthibitisha viwango vya ubora wa mbegu kwa kusajili mashamba ya mbegu, kukagua, kuchukua na kupima sampuli za mbegu katika maabara zake zilizopo Morogoro, Tengeru (Arusha), Njombe na Ukiriguru (Mwanza) kwa mbegu zinazozalishwa hapa nchini. Aidha, mbegu zinazoingizwa kutoka nje ya nchi nazo zinapimwa kabla ya kusambazwa kwa wakulima ili kuhakikisha kuwa wakulima wanapata mbegu bora kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa mazao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa udhibiti wa mbolea isiyo na viwango, Serikali kupitia Sheria ya Mbolea ya mwaka 2009, kifungu cha 7(i) imeunda Mamlaka ya Usimamizi wa Mbolea (*Tanzania Fertilizer Regulatory Authority – TFRA*), ambayo kazi zake ni pamoja na kudhibiti ubora wa mbolea za viwandani (chumvichumvi) na asilia (*fertilizer supplements*), kutoa leseni za uagizaji na usambazaji wa mbolea, kukagua mbolea zinazoingia nchini kabla ya kusambazwa nchini na kukagua ubora wa maghala ya kuhifadha mbolea hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mbegu ya mwaka 2003 na Sheria ya Mbolea ya mwaka 2009, mfanyabiashara anayethibitika kuuza pembejeo zisizo na ubora anakuwa amevunja Sheria na hivyo kustahili kupata adhabu ya kifungo au faini isiyo zidi shilingi mitano au vyote kwa pamoja. Aidha, Sheria ya Mbegu inatoa fursa kwa Mahakama kuamuru Kampuni husika kuwalipa fidia wakulima kutokana na kuuziwa mbegu feki.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge italeta Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali za Kilimo (*Agricultural Laws Miscellaneous Amendment*). Katika Muswada huo, Wizara yangu inatarajia kufanya marekebisho ya Sheria ya Mbolea na Sheria ya Mbegu ili kukabiliana na upungufu uliojitokeza katika utekelezaji ikiwa ni pamoja na kupendekeza kuongeza adhabu kwa makampuni na watu

wote watakaowauzia wakulima pembejeo feki. Aidha, naomba nitoe wito kwa Halmashauri zote za Wilaya nchini, kuwapa ushirikiano wakaguzi wa pembejeo ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo na hivyo kupunguza tatizo la uwepo wa pembejeo zisizo na ubora kwa wakulima.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba, kuna changamoto ya usambazaji wa mbegu zisizokuwa na viwango; na kwa kuwa Sheria zipo; je, Naibu Waziri anaweza kutuambia kama kuna kampuni au kiwanda chochote ambacho kimeshachukuliwa hatua za kisheria kutokana na kusambaza mbolea na pembejeo hizi ambazo hazina viwango?

(ii) Kwa kuwa mawakala wa usambazaji wa mbegu pamoja na mbolea katika Halmashauri wanafahamika. Je, Serikali haioni kwamba ni busara kufanya uchunguzi ili wale mawakala ambao wamekuwa wakisambaza mbolea na pembejeo hizi ambazo hazina viwango wachukuliwe hatua za kisheria mara moja ili zoezi hili liweze kukoma?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

Mheshimiwa Spika, hili swali la kwanza, tatizo kubwa na ndiyo maana tunasema lazima mwezi Agosti, Mwenyezi Mungu akijalia salama, tulete Sheria ya *Miscellaneous Amendment*, watu watatu hawa kwa maana ya *TOSCI*, Sheria ya Mbegu na watu wa mbolea na watu wa madawa katika vipengele vya kisheria vinavyoongoza vya biashara hili tatizo kubwa limekuwa ni adhabu.

Unapompa mtu adhabu isiyozidi milioni mitano wakati yeye akichakachua mbegu au akichakachua mbegu au akichakachua mbolea anapata faida ya milioni 200, 300, bado anapata hamasa ya kuendelea kufanya biashara hiyo chafu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulichosema ni kwamba, tunatarajia Bunge lako liridhie adhabu kali kwa watu wote hawa wanaohusika na watakaobainika na kwa maana hiyo, fedha iliyopatikana mwaka huu kwenye bajeti kwa ajili ya Taasisi hizi za udhibiti zitawasaidia kufanya kazi hiyo kwenda kufanya *sporadic inspection* ili kubaini watu hawa.

Mheshimiwa Spika, hili swali la pili la mawakala ni kweli baina ya mawakala wa mbegu na mawakala wa mbolea, tatizo kubwa lililokuwepo ni kusajili. Hawa *rural agro-dealers* na *distributors* wamekuwa wengi mno na wengi hawajasajiliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika pesa ambayo tumepata mwaka huu, moja tunalotarajia kufanya ni kuwa na *registrar distributors* na *agro-dealers* wote hawa ili tuweze ku-*monitor* kazi zao wanazofanya na kuweza kuwafuatilia wanapofanya hiyo kazi.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa miongoni mwa wakulima walioathirika sana na tatizo la mbegu ni wakulima wa pamba, zao ambalo linaajiri Watanzania takriban milioni 16. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kutuma timu yake ama yeye mwenyewe angalau katika Wilaya moja ya Kishapu kufanya uchunguzi wa kina na kubaini tatizo kwa kina ili tujue suluhisho la wakulima hawa na athari walizozipata?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana muda umeshapita.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, suala la mbegu za pamba linajulikana na matatizo yake yanajulikana. Tatizo la mbegu za pamba lipo kubwa kidogo, lipo tatizo baina ya matumizi ya mbegu bora na utayari wa kutumia mbegu bora na matumizi ya mbegu zilizokuwepo sasa hivi.

24 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninakubaliana naye tutarudi kufanya kazi hii ya kuangalia tatizo la mbegu za pamba. Tukubaliane tu, ninawaomba sana wadau wa pamba kwamba, badala ya kuingiza na sisi hisa zetu katika biashara hii ya mbegu za pamba na kadhalika, tufuate sana maelekezo ya wataalam na matumizi ya pamba hiyo ili Wananchi wetu na wakulima wetu wapate pamba kwa tija kubwa zaidi.

SPIKA: Ahsante. Muda, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, swali linalofuata.

Na. 451

Uchunguzi wa Umiliki wa Mashamba Pori

MHE. SALUM K. BARWANY aliuliza:-

Serikali iliunda Kikosi Kazi kwa lengo la kuchunguza umiliki wa mashamba na kuainisha sababu zinazopelekea yageuke mapori:-

(a) Je, uchunguzi huo umebaini nini kwenye maeneo yenye mashamba pori?

(b) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Wananchi wanaoishi kwenye maeneo hayo na hawaruhusiwi kulima?

(c) Je, kwa nini Zao la Mkonge Lindi limefutika kabisa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA

alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda, kujibu swali la Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali iliunda Kikosi Kazi kwa lengo la kutathmini hali ya mashamba ya mkonge na

changamoto zinazokabili mashamba hayo na tasnia nzima ya zao la mkonge.

Mheshimiwa Spika, uchanguzi wa Kikosi Kazi umebaini kuwa, baadhi ya mashamba hayaendelezwi kama ilivyotarajiwa kwenye mkataba wa ubinafsishaji pamoja na umiliki wa mashamba hayo kuhama kutoka kwa mmiliki mmoja kwenda kwa mwingine kwa baadhi ya mashamba bila kuwepo kwa uwazi wa taratibu zilizotumika kubadili umiliki huo na waendeshaji wa mashamba husika. Aidha, katika baadhi ya maeneo ikiwemo Mkoa wa Lindi, kutokana na ongezeko la idadi ya watu kunapelekea uvamizi wa mashamba ya mkonge ambayo hayaendelezwi kwa ajili ya shughuli za kilimo cha mazao mengine na makazi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inathamini jitihada za kuendeleza ya mashamba ya kilimo cha mazao ya chakula na biashara kwa pamoja ya wakulima wadogo na wakubwa kwa mfumo unaozingatia utaratibu wa sheria. Aidha, Serikali pia inatambua haki ya Wananchi kujiendeleza kwa shughuli za kilimo pamoja na kutambua haki ya wamiliki wa mashamba yaliyopatikana kihalali ya kuendeleza mashamba hayo bila kubughudhiwa. Hata hivyo, haki ya kumiliki mashamba inaendana na wajibu wa kuyaendeleza, pale ambapo mashamba husika hayaendelezwi na Wananchi wanabaki bila kuwa na maeneo ya kulima. Hali hiyo huwa chanzo cha migogoro na hupelekea uvamizi wa mashamba hayo. Wizara yangu inatarajia kuleta hapa Bungeni Muswada wa Sheria ya Kulinda Ardhi ya Kilimo (*Agricultural Land Management Act*), ambayo itaweka utaratibu ulio bora na wa wazi zaidi katika kupanga matumizi bora ya maeneo ya kilimo pamoja na kugawa maeneo maalum kwa ajili ya wakulima wakubwa na wakulima wadogo.

(c) Mheshimiwa Spika, kilimo cha Zao la Mkonge Mkoani Lindi kimesimama kutokana na changamoto mbalimbali hususan kuyumba kwa bei na masoko ya zao hilo katika miaka ya 80 na 90. Hata baada ya kuimarika kwa bei na masoko ya mkonge, wamiliki wengi walishindwa

kuyaendeleza kwa kuwa walishabadili matumizi na wengine walishatelekeza mashamba hayo. Aidha, kutokana na kupanuka kwa Mji wa Lindi na vijiji vyake, takriban mashamba yote ya Kikwetu, Mkwaya na Kitunda, yamevamiwa na Wananchi wanaofanya shughuli za kilimo, ufugaji na makazi; hivyo, kuchangia katika kudhoofisha maendeleo ya Zao la Mkonge Mkoani Lindi.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali yafatayo:-

(i) Kwa ahadi ya Serikali Kikosi Kazi ambacho kilifanya tathmini katika maeneo mbalimbali nchini sasa hivi ni takriban mwaka mmoja bado taarifa hiyo haijaja katika Bunge hili. Serikali inaweza kutuambia nini kuhusu kuletwa ripoti hii Bunge tuone ni tatizo gani ambalo linakabiliwa katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili?

(ii) Mashamba haya mengi yalikuwa yameasisiwa katika zama za ukoloni na yalikuwa yametafutwa maeneo ambayo yana rutuba, maeneo mazuri kwa kilimo na Wananchi wa kawaida walikuwa wamekosa kabisa maeneo ya kilimo kwa wakati ule. Serikali inakubali kwamba kulikuwa na ukiukwaji mkubwa kabisa wa umiliki na kubadilishana umiliki katika maeneo hayo. Je, Serikali kwa sasa ina utaratibu gani bila ya kuzingatia utaratibu wa baadaye katika kubadilisha umiliki huu ili Wananchi waweze kuyatumia maeneo haya kwa ajili ya kilimo kwani sasa hivi kuna uhaba mkubwa wa maeneo ya kilimo katika maeneo mengi katika Taifa letu? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, ni kweli mwaka jana tulizungumzia utekelezaji wa Taarifa ya Kikosi Kazi, iliyofanya kazi hii ilikuwa na watu wa Idara mbalimbali za Serikali, wamepita kule, lakini hawakumaliza hiyo kazi kwa sababu ya kukosekana kwa fedha za kumalizia ile kazi. Hata hivyo, pale walipofikia tayari palikuwa pameshatoa sura ya kwamba, tatizo la mashamba hayo ni kitu gani. Kwa hiyo, kwa taarifa ile iliyokuwepo ukiwa umeridhia sisi tunaweza tukaiwasilisha

kwenye Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ili na wao wapate sura ya hali halisi ya mashamba hayo ikoje, hatuna ugomvi katika kuleta taarifa hiyo Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hili la pili la mashamba ambayo hayana matumizi. Tulichosema ni kwamba, mashamba hayo yanawezekana hayana matumizi lakini yana umiliki ulio halali uliopatikana kisheria. Kwa hiyo, tathmini tunayoifanya ni kwamba, kama una shamba lakini hujaliendeleza, wajibu wako unaondoka. Serikali itafanya tathmini hiyo pamoja na watu wa Wizara ya Ardhi na wenzetu wa TAMISEMI ili hapa kwenye mashamba ya namna hiyo, tuwanyang'anye na wakulima wapate kugaiwa mashamba na jambo hilo limeshafanywa kwenye maeneo mengine. Kwa hiyo, sioni kama litakuwa na mgogoro, isipokuwa wakulima wadogo wakipewa nao wayafanyie kazi, siyo nao wayakalie wayafanyie biashara.

MHE. DAVID Z. KAFULILLA: Mheshimiwa Spika, katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ameelezea tatizo la mkonge kama ambavyo limeulizwa na Mheshimiwa Barwany. Tatizo lile linafanana kabisa na Zao la Mchikichi lilivyopotea katika Mkoa wa Kigoma. Malaysia mwaka 1990 walikuja Kigoma kujifunza Zao la Mchikichi na mbegu na mpaka sasa Malaysia inauza asilimia 44 ya Mazao ya Mchikichi yote Duniani. Naomba kujua Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha hizi *potentials* za mchikichi katika Mkoa wa Kigoma ambako Malaysia walijifunza na sisi Kigoma sasa tunapiga hatua?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme tu kwamba, *scenario* ya Zao la Mchikichi halifanani kabisa na *scenario* ya Zao la Mkonge. Zao la Mkonge kwenye miaka ya 1980 na 1990 bei ilishuka pamoja na soko zima lilishuka, sasa limeanza kupanda tena. Kwa hiyo, waliochukua mashamba hayo kwa kuendeleza Zao la Mkonge bei ilipoanza kupanda walikuwa wao wameshakuwa taabani, Zao la Mchikichi halijawahi kupoteza thamani yake; kwa sababu mafuta yanayopatikana na mchikichi ni mafuta ambayo yana afya

24 JUNI, 2013

zaidi. Kilichotokea ni kwamba, kwa sababu michikichi haikupatiwa utaratibu wa kulimwa katika mfumo ambao umeratibiwa, kwa hiyo, zao lile limeendelea kubaki katika mazingira yale wakati nafasi yake katika soko ni kubwa. Kilichotokea pia ni kwamba, zao mbadala la alizeti sasa linakwenda kwa kasi zaidi, kwa sababu mafuta ya alizeti yana ubora wa afya kama yalivyokuwa mafuta ya michikichi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunachosema ni kwamba, Serikali ina mkakati wa kuongeza uzalishaji kwenye mazao yote mawili isipokuwa tunaomba ushirikiano wa viongozi na wadau wote wa Zao la Michikichi kama wadau wa alizeti walivyofanya ili tuweze kuongeza uzalishaji wa michikichi na mafuta ya michikichi ambayo yana manufaa zaidi katika uchumi wetu.

SPIKA: Wizara ya Kilimo kwa kujibu maswali kwa kirefu mpaka muda unaisha. Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Neema Mgaya swali linalofuata.

Na. 452

Utengenezaji wa Barabara ya Njombe - Makete

MHE. NEEMA M. HAMID aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa lami barabara ya kutoka Njombe hadi Makete?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Njombe - Makete yenye urefu wa kilomita 109.4 ni Barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Nchini (*TANROADS*).

Ili mradi huu uweze kutafutiwa fedha za ujenzi kwa barabara nzima, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unatakiwa kufanyika. Serikali kupitia Wakala wa Barabara, mwezi Machi mwaka huu wa 2013 ilitiliana saina na Mhandisi Mshauri (*M/S Crown Tech. Consult (T) Ltd.*), ambaye atafanya kazi ya upembuzi yakinifu (*Feasibility Study*) na usanifu wa kina (*Detailed Engineering Design*) na kutakiwa kukamilisha kazi katika kipindi cha mwaka mmoja. Kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara nzima itaanza kutekelezwa baada ya kazi ya usanifu kukamilika.

MHE. NEEMA M. HAMID: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina swali moja la nyongeza.

Nataka kujua ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Makete - Mbeya ukizingatia kwamba barabara hii imepita hifadhi ya Kitulo, lakini vilevile imepita Shamba la Kitulo. Barabara hii inatumika kusafirisha viazi na *apples* ambazo zinaenda kuliwa Mbeya pamoja na Dar es Salaam na inaunganisha Mkoa wa Mbeya na Njombe. Kwa kuzingatia umuhimu huu; je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nikupongeze kwa kuwatetea Wananchi wa Mkoa wa Njombe na Mbeya ili waweze kupata barabara. Kuhusu swali lini tutaunganisha barabara hii; kwanza, kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi tumeahidi kwamba, tutajenga barabara ya kilomita 109 toka Njombe mpaka Makete, hatukusema mpaka Mbeya. Suala la kwenda mpaka Mbeya hili linaweza likaangaliwa katika awamu nyingine, ila kwa awamu hii tumeahidi hiyo na ndiyo tumeanza kutekeleza kwa kufanya *design*.

Namhakikishia Mheshimiwa Mgaya kwamba, baada ya *design* tutaanza kazi ya kujenga Barabara ya Nziha. Vilevile katika kuona umuhimu wa barabara hii, wakulima wakubwa wa viazi waweze kusafirisha mazao

24 JUNI, 2013

yao, tumekuwa tunajenga vipande vipande kwa awamu, maeneo ya Mang'oto tumeshajenga karibu kilomita 12 na nusu ya barabara hii ili kurahisisha usafiri wa Wananchi kwa barabara ya lami.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa maudhui ya swali la msingi yanafanana sana au kwa kiasi kikubwa na ujenzi wa Barabara ya Mto wa Mbu – Loliondo – Musoma; na kwa kuwa maandalizi ya barabara hiyo yameshaanza kwa upande wa Musoma; ni lini maandalizi kama hayo yataanza kwa upande wa Loliondo kwa sababu ni barabara moja?

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, barabara ya kutoka Makutano - Nata kuja Loliondo hadi Mto wa Mbu iko kwenye Ilani ya Uchaguzi na katika bajeti ya mwaka huu tumetenga fedha kwa ajili ya kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami baada ya *feasibility study* na *detailed design* kukamilika. Katika upande wa Musoma, tumeshatangaza *tender* na kandarasi ameshapatikana, ataanza kufanya *mobilisation* mapema. Kwa upande wa Mto wa Mbu hadi Loliondo, napo katika bajeti ya mwaka huu kuna karibu shilingi bilioni nne ambazo zimetengwa na tutatangaza *tender* na ujenzi utanzia Loliondo kulingana na maagizo tuliyokwisha kuyapata.

Na. 453

Mpango wa Kupeleka Umeme Katika Kata ya Ruvu Stesheni Hadi Kitomondo

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (K.n.y. MHE. HAMOUD
A. JUMAA)** aliuliza:-

Je, utekelezaji wa Mradi wa Umeme katika Kata ya Ruvu Stesheni hadi Kitomondo chini ya *REA* umefikia wapi?

24 JUNI, 2013

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini itatekeleza Mradi wa kupeleka Umeme katika Kata ya Ruvu Stesheni pamoja na maeneo ya Pangani, Tondoroni, Kitomondo, Kwala Dutumi, Magindu, Rukenge, Vikuge, Ngoingo, Misufini, Makazi Mapya, Ngeta, Zegero, Mzenga B na Ruvu Umwagiliaji. Mradi utatekelezwa chini ya Mpango Kabambe wa Umeme Vijijini Awamu ya Pili.

Mheshimiwa Spika, zabuni ya kuwapata wakandarasi wa kazi hizi ilitangazwa mwezi Desemba, 2012 na kufunguliwa mwezi Machi, 2013. Kazi za Mradi huu zitahusisha:-

(i) Ujenzi wa njia ya umeme ya msongo ya kilovoti 33 umbali wa kilomita 15.1.

(ii) Ujenzi wa njia ya umeme ya msongo ya kilovoti 0.4 umbali wa kilomita 9.5.

(iii) Ufungaji wa transfoma mbili zenye uwezo wa kVA 100 na tatu zenye uwezo wa kVA 50; na kuunganisha wateja wa awali wapatao 145.

Mchakato wa kumpata mkandarasi wa kutekeleza Miradi hii, unaendelea vizuri na upo katika hatua za mwisho. Inategemewa kuwa mwishoni mwa mwezi Juni, 2013 mchakato huo utakuwa umekamilika na taratibu za ujenzi zitaanza. Mradi unakadiriwa kugharimu shilingi milioni 775.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Mheshimiwa Abuu anataka kufahamu Mradi huu kama unavyoona *tender* imetangazwa.

SPIKA: Ni wewe mwenyewe wala Mheshimiwa Abuu hayupo hapa.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, tangu mwezi Desemba ambapo *tender* hii imetangazwa, utaratibu huu umechukua muda mrefu kuliko wakati ambao ni wa kawaida au uliotarajiwa:-

(i) Je, ni muda gani ambao Serikali inaaahidi kwamba utakuwa umekamilika?

(ii) Mradi huu wa Awamu ya Pili unawiana na maeneo ya Somanga, Manzese, Mtandango na pale Miteja. Pale hata hiyo *tender* haijulikani kama imeshatangazwa au imeshafanyika. Je, Serikali inawaahidi nini Wananchi wa eneo la Kilwa Kaskazini?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE): Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Abuu, kwanza, kwa kuwa mfuatiliaji mzuri sana wa Mradi huu hasa kwenye Kata zake hizi alizozisema.

Kuhusu swali kwamba mradi utaanza lini na imechukua muda mrefu. Utakumbuka kwamba, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini, ilileta maombi Bungeni kuweza kuongezewa fedha kwa ajili ya kutekeleza Miradi hii ya kupeleka Umeme Vijijini na Bunge lako Tukufu limepitisha fedha za nyongeza kwa ajili ya *REA* ili iweze kujenga uwezo zaidi wa kutekeleza Miradi hii. Dhamira ya Serikali ni kuhakikisha Vijiji vyote vya Tanzania vinapatwa umeme.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, maeneo ya Somanga na Kilwa kama tulivyoeleza mwanzoni katika mpango wetu, vijiji vyote ambavyo vinapatwa na laini kubwa za umeme, tutaendelea kuviwekea umeme. Pia katika mipango ya Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini ni kuhakikisha kwamba, Wilaya mpya pamoja na vijiji vyote vitapatwa umeme kwa awamu kulingana na upatikanaji wa bajeti

24 JUNI, 2013

yetu. Kwa hiyo, kama vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge havimo kwenye orodha ile ambayo tuliipitisha katika Bunge lako, basi tutahakikisha kwamba, katika awamu inayofuatia vinakuwemo. Kama vimo kwenye orodha ile, basi vitatekelezwa katika awamu hii katika bajeti hii ambayo tumeipitisha.

SPIKA: Ahsante. Kwa ajili ya muda, tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria.

Na. 454

Wanawake Kushiriki Kwenye Mdahalo wa Katiba Mpya

MHE. SARA M. ALLY aliuliza:-

Wanawake wamekuwa wakilalamikia Sheria ya Ndoa na mfumo dume unaowanyima haki ya kumiliki mali:-

Je, Serikali imejipanga vipi kuwaelimisha wanawake kushiriki kwenye mchakato wa Katiba mpya ili kutoa maoni yao juu ya Sheria zinazowakandamiza?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria ni kutoa elimu kwa Wananchi kuhusu mchakato wa Mabadiliko ya Katiba. Jukumu hili linatekelezwa na Wizara kwa upande mmoja na Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa upande mwingine kupitia mikutano, machapisho na vyombo mbalimbali vya habari.

Mheshimiwa Spika, wakati Tume ya Mabadiliko ya Katiba ilipokuwa ikiendesha mikutano ya kukusanya Maoni ya Wananchi kuhusu Mabadiliko ya Katiba, ilitumia mikutano hiyo kuwaelimisha na kuwahamasisha Wananchi

wa makundi mbalimbali wakiwemo wanawake, kushiriki katika kutoa maoni yao. Aidha, Tume ya Mabadiliko ya Katiba, ilitoa elimu kwa umma kwa Wananchi mbalimbali wakiwemo wanawake na kuwahamasisha kushiriki katika hatua zote za mchakato wa mabadiliko ya Katiba kupitia vyombo mbalimbali vya habari vikiwemo radio, runinga, magazeti, tovuti na machapisho mbalimbali. Aidha, kupitia mwongozo uliotolewa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba kuhusu uundwaji wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya, wanawake wamepewa nafasi maalum ya kuwa Wajumbe wa Mabaraza hayo nchini kote. Kazi ya Mabaraza hayo itakuwa ni kujadili na kuitolea maoni Rasimu ya Katiba.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, napenda kuipongeza Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa kutoa nafasi maalum kwenye Mabaraza ya Katiba kwa ajili ya Wanawake. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa kumekuwepo na vitisho vinavyotolewa na baadhi ya Viongozi wa Vyama vya Siasa hasa inapofikia wakati wa kupiga kura kwenye chaguzi mbalimbali. Je, Serikali haioni isipodhibiti mambo haya wanawake wataathirika sana kwenye mchakato wa Mabaraza ya Katiba na kupelekea kuwa na matokeo mabaya ya Katiba hasa itakapofikia wakati wa kupiga kura?

(ii) Sheria ya Mabadiliko ya Katiba inaruhusu Vyama vya Siasa kuwaelimisha wanachama wake kuhusu mchakato mzima wa Katiba. Je, Sheria hiyo inasemaje pale kinapotokea Chama cha Siasa kinapotosha Wananchi kwamba mchakato mzima wa upatikanaji wa Mabaraza ya Katiba umekosewa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ameelezea vitisho mbambali ambavyo vimekuwa vikitolewa na baadhi ya watu na ameelezea woga wake itakapofikia wakati wa kupiga kura

24 JUNI, 2013

ya maoni inayoweza kupelekea wanawake kutojitokeza kupiga kura ya maoni.

Kwanza, kuhusiana na suala hili tunatarajia katika Bunge lijalo la mwezi Agosti, kutakuwa na sheria mahususi itakayoendesha mchakato wa kura ya maoni. Kwa hiyo, mambo yote nadhani tusebiri yatakuwa yameainishwa katika sheria hiyo.

Swali la pili kuhusu Sheria ya Mabadiliko ya Katiba inasemaje kuhusiana na chama ambacho kinapotosha ukweli kuhusiana na mchakato wa Katiba. Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura Namba 83 iko wazi, hili ni kosa la jinai na atakayethibitika kufanya hivyo, atachukuliwa hatua kali za kisheria. Kwa hiyo, kwa yeyote anayefahamu mtu anayepotosha au chama kinachopotosha basi asisite kutoa taarifa katika Vyombo vya Dola.

Na. 455

Askari Kuwabambikia Kesi Wananchi

MHE. JAKU HASHIM AYOUB aliuliza:-

Kwa mujibu wa Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu ya 2007/2008, ukurasa wa 113, Wananchi wanalalamikia vitendo vya Polisi kuwabambikia kesi Wananchi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti vitendo hivyo kwa vile vinakwenda kinyume na misingi ya Haki za Binadamu na Utawala Bora?

(b) Je, Serikali imeshawachukulia hatua gani za kinidhamu na kisheria Askari waliojihusisha na vitendo hivyo ili iwe fundisho kwa Askari wengine wenye tabia kama hivyo?

(c) Ripoti ya Haki za Bindamu na Utawala Bora imesema Askari wamekuwa na tabia ya kuwatisha Wananchi na kusababisha washindwe kufuatilia kesi zao

vituoni; je, Serikali imechukua hatua gani za kukabiliana na tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a), (b) na (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo mikakati mbalimbali ya kudhibiti vitendo vya ukiukwaji wa haki za Binadamu na Utawala Bora, ikiwa ni pamoja na vitendo vya baadhi ya Askari Polisi kuwabambikia Wananchi kesi na kuwatishia ili wasifuatilie kesi zao vituoni. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kutoa elimu kwa Wananchi na Askari ili waweze kuelewa haki na wajibu wao. Lengo la elimu ni kuwafanya zaidi Wananchi kuwa ni sehemu ya ulinzi na siyo wahanga wa vitendo vya Askari.

(ii) Kuwachukulia hatua kali za kinidhamu na kisheria Askari wote wanaobainika Kujihusisha na vitendo hivyo na ukiukaji wa maadili ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2007 – 2010, jumla ya Askari 114 walifukuzwa kazi kwa makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa maadili na baadhi yao walifikishwa Mahakamani. Mafanikio ya mkakati huu wa Jeshi la Polisi itategemea zaidi upatikanaji wa taarifa ya matukio haya kutoka kwa Wananchi.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya rafiki yangu Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali madogo ya nyongeza.

24 JUNI, 2013

(i) Alipokuwa akijibu swali la msingi alisema askari 114 walifukuzwa. Tunataka kujua kati ya hao waliofukuzwa; Zanzibar ni wangapi na Tanzania Bara ni wangapi?

(ii) Kwa kuwa tatizo hilo limeathiri kesi za ubakaji Zanzibar na baada ya watuhumiwa kushitakiwa na askari kugeuza Masheikh kuozeza; je, anatoa kauli gani?

(iii) Kwa kuwa Jeshi la Polisi limepoteza mwelekeo...

SPIKA: Maswali ni mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kuhusu Askari 114 waliofukuzwa kazi ametaka kujua ni wangapi wa kutoka Zanzibar. Takwimu hizi nasikitika sinazo hapa, lakini nitampatia nikitoka hapa. Kuhusu suala la askari kushiriki kama Makadhi wa kuozeza watu ambao wamebaka, kwa kweli hili ni kosa kubwa sana la jinai na kwa kiasi kilekile naomba nichukue fursa hii kuwakumbusha Askari na Wananchi kwamba, wabakaji ni wahalifu wa digrii kubwa sana na kwa vyovyote kushirikiana nao ubakaji uwe ni kupeleka posa, hatuwezi tukakubaliana nao na tutachukua hatua za kufaa pale ambapo tutagundua hili limefanyika.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi.

Na. 456

Ada za Hati za Uraia na Visa kwa Wageni

MHE. HERBERT J. MNTANGI aliuliza:-

Tangazo la gazeti la Serikali (*GTN*) Namba 185, 186 na 189 la tarehe 1 Julai, 2011 lilirodhesha viwango vya ada za hati za uraia na visa kwa wageni mbalimbali:-

Je, mwanamke wa kigeni anapoolewa na Raia wa Tanzania na kuishi Tanzania anapaswa kufanya nini kuepuka kulipa ada hizo kwa miaka mingi kama mgeni?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tangazo la Gazeti la Serikali Namba 185,186 na 189 la tarehe 1 Julai, 2011 liliorodhesha viwango vya ada za hati za uraia na visa kwa wageni mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, raia yeyote wa kigeni anapoingia nchini, hupaswa kufuata sheria na taratibu wa kiuhamiaji ikiwa ni pamoja na kulipia ada mbalimbali zinazohusika. Kwa mantiki hiyo, mwanamke anayeolewa na Raia wa Tanzania ni mgeni kama wengine; hivyo, hupaswa kufuata Sheria na Taratibu za Uhamiaji. Pale mwanamke aliyeolewa na Raia wa Tanzania anapoamua kuomba na kukubaliwa kuwa Raia wa Tanzania, analazimika kulipia ada ya uraia mara moja tu na kuendelea kuishi kama raia wengine na hivyo kuondokana na hitaji la kulipa ada za uhamiaji kwa miaka mingi kama ilivyo kwa wageni wengine.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri, lakini ninalo swali dogo la nyongeza. Katika nchi nyingi siku hizi kuna utaratibu wa kuwa na uraia wa nchi mbili. Je, mpango huo unafikirowaje katika nchi yetu ya Tanzania?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Spika, suala la uraia wa nchi mbili ni moja kati ya masuala ambayo tumeanza kuyajadili kwa muda mrefu hapa; na hivi karibuni tulivyopata rasimu ya Katiba pia imelitaja suala hili kwenye Sura ya Tano, Ibara ya 56 na juu

ya Sheria ambayo itaundwa na kuweza kuliingiza; na kama tutalikubali hasa hapa Bungeni, suala hilo litakuwa ni moja kati ya mambo ya kawaida ya Tanzania.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wenyewe pia umekwisha. Leo tuna wageni wa aina mbalimbali, napenda kuwakaribisha wote, lakini nitamtaja Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa tu, ambaye ameambatana na Wajumbe 16 kutoka kwenye Baraza hilo, ambao wapo Bungeni kuonana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali; ni Mheshimiwa Peter Kuga Mziray.

Wageni wengine wote mnakaribishwa, waliokuja kwa mafunzo mtajifunza hukohuko na watendaji wangu.

Matangazo ya Kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Edward Lowassa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba mchana kutakuwa na kikao katika Ukumbi wa Msekwa C.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa, leo saa saba na robo watakuwa na kikao katika Ukumbi wa Msekwa C. Naomba Makatibu wenu wawasiliane kupanga vyumba ili Wajumbe wasigongane. Mtaenda kugongana hukohuko mtajua.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, saa saba leo watakuwa na Kikao cha Kamati hiyo katika Chumba Namba 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba na robo watakuwa na kikao Chumba Namba 219.

24 JUNI, 2013

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba na robo, watakuwa na kikao chao katika Ukumbi wa Msekwa. Sasa sijui Msekwa gani? Kwa hiyo, kuna Kamati tatu zinaenda Msekwa, Makatibu wenu watajua hukohuko.

Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Tundu Lissu, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa, leo tarehe 24 Juni, 2013 baada ya kuahirishwa kwa Bunge, saa saba mchana, kutakuwa na kikao kwenye Ofisi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa Iddi Azzan, anaomba niwatangazie matokeo ya Mchezo wa Mpira wa Miguu na Mpira wa Pete kati ya *Bunge Sports Club* na *Barafu Jogging*, uliofanyika Siku ya Jumapili, tarehe 23 Juni, 2013. *Bunge Sports Club* walipata goli moja na *Barafu Jogging* walipata moja. Kwa hiyo, walitoka *draw* hawa. Naomba tuwapongeze wote waliotoka *draw*. Nyota wa mchezo alikuwa Mheshimiwa Godfrey Zambi. Kumbe na wewe umo? (*Kicheko*)

Mpira wa Pete, Bunge Sports iliifunga bila huruma Timu ya *Barafu Jogging* jumla ya magoli 70 kwa matatu. Nyota wa mchezo alikuwa Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha. Kwa hiyo, wanaongezeka; hongera sana. Timu yenyewe ya *Barafu Jogging* ya wachezaji 50 kutoka Magomeni Dar es Salaam wapo na naomba msimame; michezo ni urafiki na siyo uadui. Ahsante sana na siku nyingine mjiandae muwafunge hawa jamaa.

Baada ya kusema hivyo, nawashukuru tena, Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mwongozo wa Spika.

24 JUNI, 2013

SPIKA: Mwongozo kuhusu nini michezo?

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, hapana. Tulikuwa kwenye Bajeti kwa muda karibu wa wiki nzima na leo kwa mujibu wa maelezo ambayo umetutangazia na ilivyo ada, tunafikia mwisho na Waziri wa Fedha atahitimisha Bajeti yake leo. Mwongozo ambao ninaomba ni kwamba, tumefanya mabadiliko mengi sana kwenye vitabu vya bajeti ambavyo tuligawiwa kuvipitia na kimsingi vile vitabu kwa sasa ukivipitia havioneshi hali halisi ya bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako; kwa kuwa tunafika mwisho na tumefanya mabadiliko katika vifungu mbalimbali kwa sehemu kubwa sana. Je, isingekuwa busara vikachapishwa vitabu vipya hata vichache kwa ajili ya kumbukumbu ambavyo vitaonesha kwamba hii ndiyo ilikuwa Bajeti halisi ya Serikali kwa sababu vinginevyo vitabu hivi havitaonesha sura yoyote ya bajeti ambayo tumeifanya sasa hivi?

Naomba mwongozo wako katika hilo.

SPIKA: Ahsante. Tumelifanyia kazi na kwa mujibu wa Kanuni zetu, *Appropriation Bill* itajadiliwa kwa mara moja. Kwa hiyo, kwa kuwa tuna Kamati ya Bajeti ambayo inaingia katika kila kifungu, Wizara inafanya kazi na Kamati ya Bajeti leo kabla ya kupiga kura kesho, watakuwa wametoa na wamekubaliana yale mabadiliko yaliyofanyika na hivyo itawasilishwa kwa maana ya Kamati ya Bajeti ikajiridhishe.

Kwa vyovyote vile, baada ya hapa Serikali itachapa vitabu vingine, lakini kwa leo hawawezi ila sasa Kamati ya Bajeti ndiyo inafanya kazi ya kupitia kila mabadiliko tuliyoletewa humu ndani kwamba, yameingia kama inavyostahili. Huo ndiyo mwongozo wangu.

Katibu tuendelee na hatua inayofuata.

24 JUNI, 2013

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2012 na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Majadiliano kwa maana ya Wabunge tulifunga Siku ya Alhamisi, kwa sababu wale wote walioomba kuchangia na walikuwepo walichangia. Kwa hiyo, utaratibu wa sasa ni kwamba, kwa kuwa Waziri wa Fedha ndiye mwenye hoja ya pili, tutaomba Waziri wa Ofisi ya Rais, anayehusika na Mambo ya Mipango, ajibu kwa muda wa saa moja halafu watakuja Naibu wawili na Waziri wa Fedha atakuja jioni. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa Wasira!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, kwanza, napeda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi na Wenyeviti wa Bunge, kwa kuongoza vizuri mjadala ambao niliuwasilisha hapa tarehe 13 Juni, 2013 mpaka kufikia hivi leo. Napenda vilevile kutambua mchango mkubwa sana wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mbunge wa Bariadi, kwa kupitia Bajeti pamoja na Mipango ya Maendeleo na kwa mawasiliano yaliyofanywa baina yake na Waziri wa Fedha na Serikali na kuleta mabadiliko ambayo yameweza kuleta tija katika Mpango wetu wa Maendeleo ambao utaanza kutekelezwa kuanzia Julai Mosi.

Mheshimiwa Spika, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, yote ni mambo mazuri sana na itakuwa vigumu pengine kuweza kufafanua yote katika muda wa saa moja. Ninataka niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba, yote yaliyosemwa na kila Mbunge...

SPIKA: Wale wanaotoka kwa mujibu wa Kanuni zetu, wanatoka kimyakimya.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, endapo nitashindwa kuyajibu hapa kwa mdomo basi nitaweza kuyajibu kwa njia ya maandishi. Tume ya Mipango itaandika majibu yote na kuyawasilisha kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, zipo hoja kubwa ambazo zimeelezwa katika Bunge hili kuhusu mipango ya maendeleo, ambazo nikizisema zote kwa kujumlisha moja baada ya nyingine, nitakuwa najibu hoja nyingi sana ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Hoja moja kubwa ambayo imezungumzwa ilikuwa ni kwamba, tuna vipaumbele vingi sana na kwa hiyo tunakuwa inakuwa ni vigumu sana kuweza kuvitekeleza vyote kwa pamoja. Ninapenda kutumia nafasi hii kusema, vipaumbele ambavyo vipo katika mpango wa mwaka 2013/2014 ni vilevile ambavyo vilikuwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Hakuna kipaumbele kilichoongezeka. Kwa hiyo, napenda nieleze kwamba, vipaumbele vyetu vilikuwa vitano na vimeendelea kuwa vitano.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha kwanza ni miundombinu na miundombinu inachukua sehemu ya nishati, usafirishaji, TEHAMA na maji. Kwa hiyo, utaona ya kwamba, ukizungumza miundombinu, unazungumza habari ya vitu hivi ambavyo tumevitaja bila kusahau barabara ambazo ni sehemu ya usafirishaji. Kwa hiyo, kusema ya kwamba tunavyo vipaumbele vingi siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha pili ni kilimo ambacho nacho ni muhimu sana na kilimo hicho kinajumuisha kilimo mazao, ufugaji, uvuvi na misitu, ambayo yote kwa pamoja inajumuishwa kuwa ni kilimo. Kipaumbele cha tatu ni viwanda ambavyo ni muhimu sana katika kukuza uchumi. Huwezi kukuza uchumi bila kuwa na viwanda. Kwa hiyo, viwanda vinapewa nafasi katika vipaumbele ambavyo vimetamkwa. Kipaumbele cha nne

ni rasilimali watu, ambacho kinajumuisha elimu na afya. Kipaumbele cha tano ni utalii biashara na huduma za fedha. Hivi ndivyo vipaumbele ambavyo vimetolewa.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme kwamba, vipaumbele hivi ni vigumu sana kuvitenga. Kwa mfano, ukichukua kilimo na ili kiweze kupata tija, lazima utaweka huduma za nishati, lazima kishughulikie biashara kwa sababu unalima, unazalisha halafu unauza. Miundombinu ni ya lazima katika kukuza kilimo. Kwa mfano, kama unataka kulima na wewe huna barabara, maana yake ni kwamba, mazao unayolima hayawezi kufika kwenye masoko. Kwa hiyo, vipaumbele hivi vinaingiliana na vinahusiana. Ili ufikishe pembejeo na uchukue mazao kutoka kwa wakulima, lazima uwe na barabara na vilevile lazima uwe na reli kwa ajili ya kuchukua mizigo iliyo mizito zaidi.

Mheshimiwa Spika, vilevile nishati na umeme inasaidia sana katika ujenzi wa viwanda na usindikaji na uongezaji wa thamani wa mazao ya kilimo. Rasilimali watu ni ya lazima, kwa sababu huwezi kuahirisha elimu ukasema mwaka huu hatuwekezi katika elimu. Elimu ni endelevu na lazima iendelee kupewa fedha. Ni vyema Waheshimiwa Wabunge tukatambua kwamba, katika uhalisia, nchi maskini kama yetu, kazi ya kupanga vipaumbele ni ngumu, kwa sababu kila kitu mtu anakiona ni kipaumbele. Ukisema uache hiki, huyu anasema hiki unachoacha ndiyo kipaumbele.

Kwa hiyo, kusema ukweli kupanga ni kuchagua. Pamoja na ugumu uliopo katika kupanga na kuchagua vipaumbele katika nchi ya namna yetu, ambayo ina matatizo mengi na yote yanahitaji kushughulikiwa, basi ni vizuri tujikite katika mpango wenyewe na tuache kusema ya kwamba tutaacha tena hiki mwaka huu tutaenda navyo hivi mpaka mpango umalizike, lakini mpango ujao ambao utaanza mwaka 2016 na kuendelea mpaka miaka mitano baadaye, mwaka 2020/2021, basi tutakuwa na vipaumbele vingine vipya ambavyo navyo vitatengenezwa kujengwa

24 JUNI, 2013

katika vipaumbele ambavyo tunavimaliza katika mpango huu wa awali.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe rai tu kwamba, tuendelee kusimamia. Jambo kubwa la maana hapa ni kusimamia yale tuliyo yakubali. Kama tumekubali fedha ziende kwenye maji, basi tuhakikishe maji yanapatikana. Kama tumekubali fedha ziende kwenye kilimo, basi kilimo kifanye kazi yake na vipaumbele vilivyowekwa na miradi yake vitekelezwe.

Mheshimiwa Spika, kama tumeweka fedha kwenye umeme, tuhakikishe kuwa umeme tuliokusudia ambao tulisema kwa miaka mitano tutapata megawati 2780 au zaidi, basi kweli tupate megawati zile na ikiwezekana tuzipate kwa bei nafuu zaidi kuliko hali ilivyo. Maana kwa sasa tunapata umeme lakini gharama yake ni kubwa, tunatumia mafuta mazito kuzalisha umeme na ndiyo maana kipaumbele chetu kikubwa katika nishati ni kuweka bomba la gesi kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam ili tupunguze kwa kiwango kikubwa kabisa gharama. Wataalamu wa umeme wanatuambia sasa hivi tunazalisha umeme kwa kutumia mafuta na gharama yake ni senti 35 mpaka 55 kwa *unit* moja.

Kwa namna yoyote huu ni umeme aghali sana na hauwezi kusaidia sana kujenga uchumi, kwa sababu unafanya uzalishaji nchini uwe aghali sana. Kwa hiyo, kipaumbele cha umeme tumekifanya namba moja, kwa sababu kitasaidia sana katika kukuza uchumi wa viwanda, kukuza uchumi wa kilimo na kufanya gharama za uzalishaji zishuke na vilevile kudhibiti mfumko wa bei. Kwa hiyo, vipaumbele hivi vinahusiana. Ninarudia, jambo kubwa ni kuhakikisha tunajenga nidhamu ya kuhakikisha kuwa kile tulichokikubali tunakitekeleza.

Ninajua Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema fedha haziendi kwenye Miradi kwa wakati na wakati linasemwa Waziri wa Fedha nilikuwa naye, nikamwuliza umesikia na hilo? Nami ninaamini kabisa kuwa, Waziri wa

Fedha amelisikia na atatumia muda mrefu zaidi kueleza jinsi atakavyofanya kuhakikisha nidhamu ya utekelezaji inakuwepo, rasilimali fedha inapatikana na Miradi iliyokubaliwa na Bunge hili inatekelezwa, kwa sababu ni kwa kufanya hivyo tu mabadiliko yatapatikana.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ambayo ilisemwa sana hapa na ambayo ni ya kweli ni kwa nini ukuaji wa uchumi haupunguzi umaskini. Kwanza ni lazima tukubali kuwa, tunalo tatizo kubwa sana la umaskini nchini na hili halina ubishi. Tukubali vilevile kuwa, yapo ambayo au tumeyafanya lakini hayajafanikiwa sana na zipo hatua ambazo ni lazima tuchukue katika kuleta mabadiliko.

Ukuaji wa uchumi kwa kasi kubwa ni jambo la lazima katika kupunguza umaskini, kwa sababu ukuaji wa uchumi ndiyo unaweka kipato ambacho watu watagawana katika sekta mbalimbali. Kama uchumi haukui kwa haraka na umaskini vilevile hauwezi kupungua. Hata hivyo, ukuaji huo wa uchumi wa asilimia kubwa zaidi unahitaji udumu kwa kipindi fulani; Wachumi wanasema kati ya miaka 10 na 15. Sasa tuangalie kwa nini hali ipo hivyo.

Jibu lake ni kwamba, inagawa uchumi wetu, unakua lakini sekta zinazokua kwa haraka sana na kwa kiwango kikubwa ni zile ambazo haziajiri watu wengi; kwa mfano, biashara na viwanda vinakua kwa asilimia 8.1, madini asilimia 8.3, ujenzi asilimia 9.7, biashara ya fedha ni asilimia 15, mawasiliano ni asilimia 20, lakini sekta zote hizi zinazokua kwa kasi kubwa unaona ajira inayopatikana katika sekta hizi ni watu wachache sana. Unaweza kujua tu bila mahesabu sana ni watu wangapi wanaajiriwa viwandani, watu wangapi wapo kwenye madini, watu wangapi wapo kwenye ujenzi, watu wangapi wapo katika sekta ya fedha na watu wangapi wapo katika mawasiliano licha ya kuwa mawasiliano inakua kwa asilimia 20.

Sekta ambayo inaaajiri watu wengi ni kilimo; kilimo kinaajiri watu zaidi ya asilimia 70, lakini ukuaji wake kwa muda mrefu sasa umekua asilimia nne kwa wastani. Kwa hiyo,

kwa namna yoyote ile ukichukua ukuaji wa asilimia nne na ukachukua ongezeko la watu ambalo linaongezeka kwa asilimia 2.7, ukitoa utaona ya kuwa pato la kilimo linaongezeka kwa asilimia 1.5. Kwa hiyo, hili ndiyo tatizo ambalo tunakabiliana nalo katika kuonesha ya kwamba ingawa tunapambana na tatizo hili la umaskini, lakini ukuaji wa sekta ambayo inaweza kuondoa umaskini bado haiko sawasawa.

Suala ambalo mtu anaweza kujjuliza; tunafanya nini ili tuondokane na adha hii ya kuwa uchumi unaokua lakini umaskini haupungui kwa kiwango kilekile? Jambo kubwa mahususi ambalo tunafanya ni kujaribu kubadilisha uchumi, ili hata vijijini tusitegemee kilimo tu, lazima iwepo *diversification*, lazima viwepo viwanda vidogovidogo ambavyo vinaongeza thamani ya mazao ya kilimo, vinavyoweza kutoa ajira. Tukifanya hivyo, watu wengi zaidi watapata ajira katika viwanda vidogovidogo kule vijijini. Tusitegemee umaskini kweli utapungua kwa jembe la mkono peke yake, ni lazima tuchukue hatua zaidi.

Kwa kilimo chenyewe ni lazima tuongeze tija; yako mazao mengine ambayo wakulima wakiamua kuyalima wanaweza kupunguza umaskini. Kwa mfano, wanaweza kulima mbogamboga katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ina hali nzuri sana ya hewa na kule tumejenga Kiwanda cha Songwe. Wakiweza kulima mazao mengi sana ya thamani kubwa kutoka kule, umaskini unaweza ukapungua. Kwa hiyo, ni lazima tuweke mkakati ambao unawawezesha wakulima kuongeza.

Katika Mpango huu ambao ninahitimisha hoja yake hapa, tumeweka tija katika kilimo, tumetenga shilingi bilioni 120 kwa ajili ya ruzuku ya pembejeo, tumetenga shilingi bilioni tisa kwa ajili ya utafiti wa kilimo, tumetenga shilingi bilioni 22 kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji na vilevile tumetenga shilingi bilioni 339 kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa umeme vijijini. Mimi ninaamini kabisa, tukipeleka umeme vijijini na tukaanza kushughulika na viwanda vidogovidogo vikawa vina-*support* kilimo, tatizo

la umaskini vijijini litapungua, kwa sababu tutakuwa tumefanya *diversification* ambayo inasaidia kuongeza uzalishaji na ubora wa kile kinachozalishwa huko vijijini.

Shilingi bilioni kumi ni kianzio ambacho kimewekwa kwa ajili ya kuongeza mtaji kwa ajili ya Benki ya Kilimo. Moja kati ya tatizo kubwa ambalo inabidi tulikubali, hatuwezi kukuza kilimo kwa kutumia Bajeti ya Serikali peke yake; haiwezekani, hata kama tukifika lile lengo la asilimia kumi, yako mambo ambayo Serikali itafanya lakini vitu vingine haviwezi kufanywa na Serikali. Kwa mfano, kama mkulima anataka kubadili kilimo chake, anataka kuongeza ukubwa wa shamba lake ambalo analima kwa jembe la mkono, sasa anataka kutoka katika jembe la mkono aende kwenye plau au atoke kwenye plau aende kwenye *power tiller* au anataka kununua trekta, mkulima huyu hawezi kupata fedha kutoka Bajeti ya Serikali. Mkulima huyu ataenda kwenye chombo kinachokopesha. Hiyo ndiyo ninaamini kuwa inaweza kusaidia uwekezaji katika Sekta ya Kilimo ambayo unaweza kufanya kilimo kikaongeza tija na kuongeza mapato ya wakulima.

Liko suala ambalo linaulizwa kwamba, ongezeko la watu linaharibu sana uchumi, umaskini unaendelea kuongezeka. Hili ni jambo ambalo haliwezi kutungiwa sheria na wala huwezi kupunguza ongezeko la watu kwa sheria, elimu ndiyo jibu. Nami ninaamini ya kwamba, elimu kwa wasichana na kuhakikisha wasichana karibu wote wanasoma, kiwango cha ongezeko la watu kitapungua. Kwanza, ukiwasomesha wote unawachelewesha kuzaa, ukiacha wamalize la saba wanazaa. Watu wengine wanasema Shule za Kata, lakini zimepunguza hii *problem*, wasichana hawa ambao wangezaa mara moja, sasa wako shuleni hakuna nafasi ya kuzaa. Tuwajengee hosteli ili wasionane na wenye kuwaharibia shule *then* kwa kweli tunaweza kabisa kupunguza ongezeko la watu kwa njia ya elimu zaidi kuliko kufikiria unaweza ukapitisha hapa sheria ukasema sasa watoto ni idadi fulani; haiwezekani hiyo. Tena kwenye jamii hizi za kwetu huku haiwezekani, hii inawezekana Uchina zaidi kuliko hapa.

24 JUNI, 2013

Vilevile kuwepo kwa viwanda kama *EPZ* na Wataalamu wa Kilimo na Benki ya Kilimo kama nilivyosema, vyote vitasaidia katika kuwekeza katika kilimo na hivyo kupunguza zaidi kasi ya umaskini. Vilevile tukumbuke kuwa, tunao watu ambao ni maskini sana vijijini, ambao hata kukopa kwao ni *problem*, hawa tunataka kuwainua na tumeanzisha mpango unaoitwa *Conditional Cash Transfer* au uhawilishaji wa fedha kwa watu ni maalum tunafanya hili kupitia Mfuko wa *TASAF*.

Tutafanya hivyo baada ya kufanya *survey* katika vijiji vyote nchi nzima, Tanzania Bara na Visiwani ili tuone wale watu ambao hawawezi kabisa, yaani wengine ni watu wazima kabisa, wengine ni vilema, wengine ni nani, watu wasiojiweza lakini wanalea watoto, wengine wameachiwa wajukuu wanalea, lakini hawana uwezo wa kuwasomesha, tunaazisha mpango ambao utawapa fedha watu hawa ili waweze kujisaidia wenyewe.

Kwa mfano, unaweza unaweza ukakuta ana wajukuu hawaendi shule kwa sababu hana uwezo wa kuwanunulia viatu na mtoto anaona aibu kwenda kusoma shule kwa sababu wenzake wote wana viatu yeye hana au yeye mwenyewe hawezi kwenda hospitali kwa sababau hawezi kulipa ile shilingi 1000, tunataka kuwapa fedha kwa utaratibu maalumu wa uhawilishaji wa fedha ili waweze kugharamia Bima ya Afya, waweze kwenda Hospitali, watoto wao wanaowalea waweze kusoma; hii itasaidia kidogo katika kupunguza adha ya umaskini uliopindukia ulioko katika maeneo ya vijijini na hata mjini. Hii hatua inachukuliwa, inaanza kufanya kazi katika bajeti ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lililozungumzwa, wanasema hakuna mpango madhubuti wa kukuza uchumi hasa katika Kanda ya Ziwa. Ninasema mipango ipo inayohusu nchi nzima na Kanda ya Ziwa ikiwemo. Kanda ya Ziwa tunatambua, kwanza, ina watu wengi, asilimia 27.12 ya Watanzania wote wanaishi katika Mikoa sita hapa

24 JUNI, 2013

nchini, tunatambua mchango wa uchumi unaotolewa na eneo hili wa asilimia 20. Kwa hiyo, hakuna uwezekano ambao unaweza kupanga mpango halafu ukaacha eneo maalumu lolote katika Tanzania. Iko mipango ya utengenezaji wa barabara ambayo inaendelea na Miradi ya Umeme ipo ambayo inatengenezwa kule Mwanza. Kwa hiyo, masuala haya yote yanaunganishwa, yatasaidia kukuza uchumi, lakini ninatambua kwamba, lipo tatizo katika Ukanda wa Ziwa la Pamba.

Pamba hii inalimwa kila mwaka, lakini haijasaidia sana katika kupunguza umaskini wa Kanda hii na sababu zake ni rahisi kueleza; kwanza, bei zinashuka na kupanda sana, kiasi kwamba mwaka mwingine inapanda sana halafu ikishuka sana watu wanapunguza kilimo na umaskini unaongezeka katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kusema kweli kuna mambo mawili ambayo ni lazima tufanye kwa ajili ya zao hili na mazao mengine nchini. Moja ni kutia moyo watu kuwekeza kwa ajili ya utengenezaji wa nguo na nyuzi kwa kutumia zao hili la pamba ili tuache kuuza nje pamba ambayo ni ghafi. Hili jambo tunalifanya, lakini vilevile ni lazima tuhakikishe ya kwamba, tunawasaidia watu katika maeneo haya kuweza kufanya kazi kwa maarifa zaidi, ndiyo maana tuliwapelekea Mabwana Shamba, hata uzalishaji wenyewe wa zao hili bado wastani wetu wa uzalishaji wa Zao la Pamba ni kilo 300 kwa ekari.

Tunaweza tukafika mpaka kilo 1200, hata kama bei itakuwa ya chini au ya wastani, lakini kama ongezeko lako la mazao ni kubwa, bado inakulipa zaidi kuliko kama una kilo 300 ya wastani wa ekari moja. Kwa hiyo, juhudi hizi zitaendelea, lakini ninataka kuwahakikishia ndugu zangu kutoka Kanda ya Ziwa kuwa, Serikali haijaacha na wala siyo kwamba haina mpango kabisa wa kufanya kazi ya kuleta mabadiliko katika eneo hilo.

24 JUNI, 2013

Serikali ina mpango gani wa kuwezesha wawezeshaji wa ndani kuwekeza na kutoa ajira zaidi kwa Watanzania? Mipango iko mingi, moja ya mipango hiyo ni mpango wa udhamini wa mkopo wa mauzo ambao unasimamiwa na Benki Kuu. Kama mtu anataka kutengeneza kiwanda na anataka kuuza mazao yake nje, huu Mpango, *export guarantee* unaweza kupatikana Benki Kuu na huu Mpango unaweza ukawasaidia sana wawekezaji na hasa wale wawekezaji wa ndani.

Mheshimiwa Spika, nimeigiza Tume ya Mipango itazame kwa makini zaidi na itoe ushauri kwa Serikali jinsi inavyoweza kuweka mipango mingine zaidi inayoweza kuwa-*encourage* wawekezaji wa ndani kuweza kupata uwezo wa kuwekeza katika Sekta ya Viwanda. Lazima tukubali kuwa, uwekezaji wa nje tunaupenda na tutaendelea kuutia moyo, lakini vilevile *base* ya uchumi inaweza kuwa kubwa zaidi kama wawekezaji wa ndani wanawekeza.

Lazima tuwe na watu hapahapa, hii *local capitalism* ya hapa lazima nayo ikue. Kuna Mbunge mmoja alisema hapa tu-*breed* hapa mabilionea mia moja; sasa bilionea mia moja hatuwezi kuwapata mpaka wawekeze, maana huwezi kuwa milionea labda uwe unafanya bahati nasibu, lakini kama unataka kupata ubilionea ni lazima uwekeze na kama wewe huwezi basi usaidiwe na Serikali iweke mazingira ambayo yanaweza kukufanya ukawekeza na kwa hiyo ukapata bilionea na kujenga hiyo *middle class* inayozungumzwa.

Hoja ya tano ilihusu *Presidential Delivery Bureau* kwamba, kwa nini hii *Bureau* haijawekewa utaratibu wa Kisheria? *Bureau* hii imeanzishwa tayari, imeanzishwa kwa mamlaka aliyonayo Rais kupitia Ibara ya 36(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, ambayo inampa Rais, mamlaka ya kuanzisha au kufuta Taasisi yoyote ya Umma kwa manufaa

ya nchi. Kwa kutumia mamlaka hayo, Mheshimiwa Rais na kwa kutumia Kifungu cha 5(51) cha Sheria ya Majukumu ya Mawaziri, yaani *Ministers' Discharge of Ministerial Function Act*, Sura ya 299, ameunda Taasisi hii na ameipa kazi. Hii haina maana kwamba Taasisi hii haiwezi kuundwa Kisheria, tumeona ianze hivyo ili ianze kazi, lakini mpango wa kuandika sheria ambayo italetwa Bungeni hapa siku zijazo ili *Delivery Bureau* hii iweze kuundwa kisheria, itafanywa. Kwa hiyo, hakuna kilichoharibika na Bunge hili litapewa fursa ya kujadili na kutoa mawazo.

Mheshimiwa Spika, tutapata *experience* zaidi baada ya kuwa imeanza kazi na tumeona inavyo-*function*. Kwa hiyo, hata tutakapokuja kujadili, tutakuwa tunajadili kitu ambacho tayari kipo, tumekiona, kinafanya kazi, sasa tunasema hiki kwa kweli kinaweza kutusaidia au vinginevyo au tutapata mawazo ya namna ambavyo kinaweza ku-*function* vizuri zaidi.

Hoja nyingine ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge kama hoja ya jumla ni hoja inayosema fedha za kutosha zitengwe kuwezesha Taifa kuwa na Wanasayansi katika fani za mafuta na gesi. Hili limezungumzwa na Mheshimiwa Profesa Msolla, ninadhani alilieleza vizuri zaidi jambo hili. Ninataka kusema kuwa, jambo hili linafanyika sasa; kwa mfano, Serikali imeanzisha Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela na kimeanza kuchukua Wanachuo 295 wanaendelea kugharamiwa. Kati ya hao, 195 ni wa Shahada ya Uzamili na 100 wa Uzamivu, wanasoma katika Vyuo Vikuu vingine vitano vya Umma ambavyo ni Dar es Salaam, Sokoine, Muhimbili, Ardhi na Nelson Mandela.

Chuo cha Madini Dodoma kinaendesha mafunzo ya Diploma ya Sayansi ya Miamba ili kuandaa wataalamu katika eneo la gesi na mafuta. Tayari wanafunzi 61 wamedahiliwa na kuanza masomo. Wizara ya Nishati na

24 JUNI, 2013

Madini, kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC*), imefadhili vijana wa Kitanzania 122 katika fani ya mafuta na gesi, ambapo vijana 30 walifadhiliwa katika Chuo cha Madini Dodoma, wanafunzi 15 wamefadhiliwa katika fani ya uhandisi na usimamizi wa mazingira na wanafunzi 15 katika fani ya jjiolojia ya mafuta na gesi.

Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*), kina vijana 64, Lindi 50 huko *VETA* Mtwara. Kwa hiyo, jambo hili limeanza na linafanyiwa kazi na matumaini yangu ni kuwa, kazi hii ya kusomesha Wazalendo ili gesi na Sekta ya Mafuta iweze kusimamiwa na watu ambao ni wazalendo wa nchi hii, hatimaye ni lazima iendelee.

Vilevile Serikali inakamilisha utaratibu wa kupeleka vijana 20 huko Brazili na China, kusomea Shahada ya Uzamili na Uzamivu. Tume ya Sayansi na Teknolojia inagharimia mafunzo ya wataalam 184 wa ngazi ya Shahada ya Uzamili na 84 wa ngazi ya Uzamivu kwenye Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *MUHAS*, *SUA*, *Nelson Mandela* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 500 fedha za ndani na shilingi bilioni kumi fedha za nje, kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Uendelezaji Rasilimali Watu. Kwa hiyo, kazi hii itaendelea.

Hoja nyingine ambayo imesemwa ni matumizi ya kawaida kuwa makubwa zaidi kuliko matumizi ya maendeleo. Mimi ninajua wote tungependa fedha za maendeleo ziwe nyingi zaidi, lakini tumepiga hatua kiasi, katika Mpango wetu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, tuliweka lengo kwamba, tutakuwa tunapata fedha ya maendeleo asilimia 35 ya bajeti nzima, mwaka jana tulitenga asilimia 30, mwaka huu tumetenga asilimia 31; kwa hiyo, tumepiga hatua, lengo ni kufika asilimia 35 ya Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini lazima tujiulize, hivi unaweza ukafanya maendeleo halafu ukaepuka matumizi ya kawaida? Hilo nalo ni hoja. Ukiongeza shule unaongeza Walimu na unaongeza mahitaji ya vitabu. Ukijenga hospitali, unaongeza mahitaji ya dawa, kwa hiyo hakuna namna, tena kama unaendelea ndiyo inakuwa *problem* zaidi mpaka unapofika hatua unaweza ku-*balance* kiasi fulani. Lakini kama unataka maendeleo ukitengeneza barabara mpya unahitaji *repair* na *repair* ile ni matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, tusiwafanye wananchi wafikiri kwamba, matumizi ya kawaida ni posho, matumizi ya kawaida ni mambo ambayo hayaeleweki. Matumizi ya kawaida yana huduma kwa jamii, kwa hiyo tuiseme tu matumizi ya kawaida yamezidi, yanakwenda wapi ndiyo hoja.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Mbunge anadhani matumizi ya kawaida yanakwenda katika maeneo ambayo hayahudumii wananchi hapo kwa kweli kuna *problem* na ana haki ya kuhoji, lakini kama yanakwenda kununua dawa ili watu watibiwe, kama yanakwenda kuwasomesha watoto, unawapa vifaa, nadhani matumizi ya kawaida ni lazima yawepo ili kuweza kutoa huduma nzuri zaidi na *i-support* maendeleo yanayoendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya nane inasema mbinu zinazotumika kuwasaidia wakulima ni zipi. Nimekwishaeleza kiasi fulani, lakini Serikali inachukua hatua kusaidia wakulima na wananchi kukidhi matakwa haya ya kibenki kwa sababu benki hizi hazikopeshi wakulima kwa sababu ni benki za biashara. Benki ya Kilimo tunategemea itafanya hivyo, lakini kinachosemwa ni kwamba wakulima hawana dhamana.

Mheshimiwa Spika, nataka kutumia nafasi hii kutoa wito kwa Halmashauri zote nchini, kwamba tunayo MKURABITA, MKURABITA ile inakwenda kwenye Wilaya, inatoa mafunzo kwa watu wanaoweza kueneza elimu ya kupima ardhi na kuwapa wakulima hati za kimila, lakini wakitoka pale Halmashauri nayo inaacha, MKURABITA inapima vijiji viwili.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilikwenda katika Wilaya ya Geita, nikakuta MKURABITA ile iliahidi kupima vijiji viwili na ikaachia Halmashauri, pale walipokomea ndipo na Geita ilipokomea hapo hapo na ikapita mwaka. Sasa nadhani *priorities* zetu ndizo *problem*. Lakini kama Halmashauri zitawezesha watu hawa kupimiwa ardhi yao na wakapata hati, hata hili tatizo la kusema hawakopesheki litapungua, kwa sababu watakuwa na dhamana na ardhi ni mali ambayo inaweza ikawekezwa na mtu akaweza kukopa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo napenda Halmashauri zichangamkie fursa hii ili zipime ardhi ya Watanzania, iwe mali ya Watanzania, na itumike kwa ajili ya kuwasaidia kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo mambo ninayoweza kusema kuhusu suala la mikopo, lakini tunaendelea, tunawahimiza Wakulima kuweka *SACCOS* zao na zenyewe zinakuwa dhamana, zote zinaweza zikawasaidia katika kupiga hatua.

Mheshimiwa Spika, pia tunalo Baraza la Uwezeshaji ambalo linasaidia sana vile vile kuwafanya wakulima waweze kupata hasa mikopo ile midogo midogo siyo ile mikopo mikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limesemwa hapa ni kwamba, wakulima wananyonywa sana, bei ya mazao yao ipo chini. Bei za mazao ya wakulima hapa nchini zinapanda na kushuka sana, lakini kuna jambo moja ambalo lilisemwa hapa kwamba wanapewa bei ndogo sana asilimia ndogo ya mazao ya soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, nataka kueleza mshangao wangu katika hili, kwa sababu ninao uzoefu, nilikuwa Waziri wa Kilimo na tulileta hapa mabadiliko ya sheria za mazao yote nchini, ambazo zinatoa mamlaka kwa mazao hayo kusimama na kuzungumza na wanunuzi baada ya kuelewa bei soko ya dunia ikoje.

Mheshimiwa Spika, maelekezo yetu ni kwamba mkulima huyu asipewe chini ya asilimia 70. Sasa sielewi kwa nini wakulima wapewe bei ndogo kwa mazao yao, lakini takwimu za Benki Kuu tumezitifuta ili zituoneshe nini hasa kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, takwimu za Benki Kuu zinaonesha kuwa bei ya kahawa kwa mfano iliyobanguliwa maganda ya Robusta katika soko la dunia kwa mwaka 2012 ilikuwa ya wastani wa dola za marekani mbili na senti thelathini na nne, (*USD*2.34) sawa na shilingi elfu tatu mia saba na nne (sh. 3,704) kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ili kupata kilo moja ya kahawa iliyobanguliwa unahitaji kilo moja ya kahawa isiyobanguliwa ambayo ilikuwa na bei ya sh. 1300 kwa kilo. Maana yake ni kwamba mkulima alilipwa shilingi 2600 kwa kilo ambayo ni asilimia 70 ya bei ya soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, bei ya nyuzi za pamba kwa kilo moja unahitaji kilo tatu kuweza kupata nyuzi. Kwa hiyo, unapoweza kuchukua bei ya soko la dunia ukaigawa mara tatu, unaweza ukapata wastani wa bei ambayo mkulima anapewa. Bodi za Pamba na Bodi zingine, Bodi za Mazao Mbalimbali pamoja na Mazao Mchanganyiko ambayo tuliyaundia Bodi ya Mazao Mchanganyiko, ni lazima zisimame upande wa wakulima, zi-*negotiate* kwa niaba yao.

Mheshimiwa Spika, kama hazifanyi hivyo kwa kweli zitakuwa zinawa-*betray* wakulima, Bodi ni lazima zisimame zihakikishe kwamba mkulima hata bei ikishuka, lakini bado anapata asilimia 70 ya bei ya soko la dunia, vinginevyo wakulima watakuwa wanawalimia wafanyabiashara, kitu ambacho siyo sawasawa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya jumla sasa nitatumia muda kueleza mambo ambayo yamesemwa. Kamati yetu ya Bajeti imezungumzia mambo mengi, lakini hatuna matatizo na mambo yaliyozungumzwa. Kwa mfano, wamesema kwamba, vipaumbele ni vingi, hilo nimeshalieleza

kwamba vipaumbele ni vilevile. Wanasema miradi mingi inaandaliwa bila ya kuwa na muda na kiasi cha fedha kinachohitajika kugharamia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango sasa inaandaa mwongozo wa jinsi ya kuandika andiko la mradi litakalosaidia kutoa taarifa stahiki kuingia katika vitabu vya bajeti, kuonesha mpango mzima utakuwa na gharama gani, ili gharama inapokuwa imezidi hapo tuweze kujiuliza kwa nini gharama imezidi. Lakini tunaishukuru sana Kamati ya Bajeti imefanya kazi yake vizuri na tunaendelea kupokea ushauri mzuri kutoka kwao.

Mheshimiwa Spika, Kamati walihoji juu ya mfumo mahsusi wa Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi (*Presidential Delivery*). Hata hivyo ni muhimu sana walisema ni lazima tubadili fikra ndiyo mpango huu ufanikiwe. Nakubaliana nao, kama hatubadili fikra, hiki kitu kitakuwa kigumu, kwa sababu wapo wengine wanauangalia mpango huu kwa jicho la husuda, wanaona kama Upolisi hivi.

Mheshimiwa Spika, lakini na Upolisi nao unasaidia vile vile. Kama wewe unataka kufanya uhalifu na Polisi wapo karibu, unaweza ukaahirisha, kwa hiyo, kama wewe unaiogopa hii *bureau*, unaiona kama kofia ya dola hivi, basi na uione hivyo ili uache kufanya vitu ambavyo havieleweki. Lakini *bureau* hii itafanya kazi na sisi tunaamini kwamba, itakuwa inafuatilia siyo kwa nia ya kutaka kufanya Upolisi lakini kwa nia kutaka kujua kwa nini mpango huu hauendi vizuri, tatizo ni nini, na kusaidia kukwamua matatizo ili mpango ule ufanikiwe, ndiyo hoja.

Mheshimiwa Spika, siyo hoja ya kusema nani ameiba hapa, hiyo siyo kazi ya hii, lakini hata hiyo nayo ikifanyika, kama umeiba watakuuliza vilevile, kwamba wewe umepewa hela kiasi hiki, mbona kazi iliyofanyika hailingani na hela, hiyo nayo ni hoja. Sasa kwa nini wewe unanuna kwa jambo hili?

Mheshimiwa Spika, licha ya kuridhishwa na ukuaji wa uchumi, bado kuna tatizo la umaskini, nimekwishalieleza ni

tatizo la kweli na nakubaliana na tatizo. Kupunguza matumizi ya Serikali Waziri wa Fedha atalieleza vizuri zaidi, Deni la Taifa vile vile atalieleza vizuri kwa sababu yeye ndiye mkopaji mkuu wa hii Serikali, kwa hiyo anayekopa ndiye anayejua akope tena au asikope tena.

Mheshimiwa Spika, jitihada ziongezwe katika uzalishaji wa bidhaa ndani ya nchi hii tunakubaliana, lakini kusema tusitishie kuagiza nayo ni ngumu mpaka hapo tutakapokuwa tunazalisha mazao mengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Richard Ndassa, alizungumzia juu ya bandari ya Dar es Salaam na kutaka ifanyiwe ukarabati na ichukue hatua ambayo inaweza kuifanya ikawa na ufanisi mkubwa, tunakubaliana naye kabisa kwa jambo hili, lakini hatua zimeshaanza kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kuna *operations* za pamoja zinazoshirikisha wadau wote wanaohusika katika shughuli za bandari zimefanyika, kuna kuboresha mifumo ya ulinzi bandarini, kuwa na njia moja ya kuingiza na kutoa mzigo bandarini *one way cargo traffic* na kuanzisha mfumo wa kisasa wa uendeshaji wa *terminal* ya *TPA* utakaosaidia menejimenti na makontena kufanyika kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zote zinachukuliwa pale bandarini. Hatua hizi zote zimeifanya bandari imeanza kuwa na ufanisi kidogo, lakini bado tunadhani Wizara inayohusika inaendelea. Ndugu yangu Mheshimiwa Mwakyembe nadhani yupo hapa atakuwa ananisikia kwamba, bado inahitajika kuchukuliwa hatua zaidi ili bandari yetu iwe *competitive* na bandari zingine kama vile Mombasa na kadhalika. Hiyo ndiyo hoja kubwa ambayo Mheshimiwa Ndassa alisema na sisi tunakubaliana nayo.

Mheshimiwa Spika, dada yangu Mheshimiwa Agripina Buyogera na Mheshimiwa Felister Bura, walizungumzia reli kwamba, ni lazima tuwekeze katika reli. Nakubaliana na wote, reli ile ni lazima kabisa, kwanza ukitengeneza barabara

bila reli unafanya jambo ambalo ni la muda, kwa sababu baada ya muda hutakuwa na barabara, kwa hiyo tuwekeze katika reli. Vile

Mheshimiwa Spika, vile reli hii si kwa ajili ya ku-*protect* barabara tu, inasaidia sana katika kupunguza mfumuko wa bei katika mikoa inayotegemea reli hii. Ukichukua kwa mfano, bei ya saruji Mwanza, Mara na Kagera ni kubwa karibu mara mbili ya bei hiyo katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa sababu uchukuzi ni wa magari. Lakini ukipeleka mizigo hii kwa reli mpaka Kigoma, Mwanza bei ya saruji hasa ile mizigo mizito sana itafika katika maeneo hayo na bei zitashuka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili ni jambo muhimu na sisi tunalipa umuhimu mkubwa, ndiyo maana tumetenga shilingi bilioni mia moja ishirini na tisa, mia sita ishirini na nne milioni kwa ajili ya kusaidia mambo ya ukarabati na ununuzi wa injini za treni, mabehewa na vifaa mbalimbali, ukarabati wa njia kuu ya reli na kubadilisha njia ya reli na kuiweka uzito wa ratili themanini kwa *yard*. Haya tunayafanya kwa ajili ya kutaka reli ifike mahali ambapo itatoa huduma nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kidawa Hami na Mheshimiwa Profesa Msolla wote walizungumzia fedha za utafiti tunakubaliana nao, lakini fedha hizi za utafiti ingawa hazijatosha, lakini zinakwenda katika mashirika mbalimbali, Kilimo wanapewa, Shirika la Utafiti nalo linapewa na mashirika mengine kama *CARMATEC*, *TEMCO*, *TIRDO*, *NIMR* nayo yanapewa fedha hizo. Kwa hiyo, ukiziunganisha unaona siyo mbaya sana, lakini bado naamini hatujafikia lengo la asilimia moja ya kuwapa watafiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa Msolla alitaka juhudi kubwa zaidi zichukuliwe kwa ajili ya kupatikana elimu ya ufundi stadi. Juhudi hizi zinaendelea, tunaendelea kupanua elimu ya ufundi, tumejenga Vyuo vya Ufundi katika Mikoa ya Pwani, Lindi na Manyara hivi karibuni, lakini juhudi zinaendelea za kubadilisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili viweze kutoa elimu ya ufundi katika ngazi ya

Wilaya. Kwa hiyo, tunafikiri tunakwenda, lakini nafikiri ni tamaa ya kutaka twende haraka zaidi na mimi nakubaliana na Profesa Msolla.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwe na mpango kabambe wa kuboresha elimu juu ya uzazi wa mpango, anasema Mheshimiwa Augustino Masele, nakubaliana naye na nimekwishasema. Namna moja ya kupunguza uzazi ni kusomesha wasichana, kwa sababu ndiyo wanaozaa na wao wakiamua kupunguza uzazi kwa sababu wameelimika, kasi yetu ya ongezeko la watu litapungua, siyo kwa nia ya kuwazuia watu kuzaa, lakini kuzaa kwa mpango ili waweze kutoa huduma nzuri zaidi kwa watoto wanaowazaa. Kwa hiyo, ndiyo maana kuna msemu kwamba, ukielimisha wanawake unaelimisha jamii nzima. Kwa hiyo, suala hilo nalo tunalitilia mkazo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Salehe Pamba alizungumzia tutenge 0.5 ya bajeti ya Serikali au pato kwa ajili ya masuala ya mazingira, tunasisitiza sana suala la mazingira. Uharibifu wa mazingira ni tatizo kubwa na nakubaliana naye, jambo hili lishughulikiwe kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla alizungumzia kwamba, bajeti haijatoa mikakati ya kuongeza ajira kwa vijana. Nadhani tuseme ukweli kwamba, vijana tunao wengi, waliomaliza darasa la saba, waliomaliza *form four*, waliomaliza *form six* na hawakuendelea, lakini vilevile tunao vijana ambao wamesoma kwenye Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano una-*provision* ya kuongeza ajira. Ukitilia mkazo ongezeko la viwanda, unazungumzia habari ya ajira na kila sekta iliyo katika mpango huu inaweza kuongeza ajira. Lakini vile vile tumeweka Mifuko, tunachotaka ni vijana waji-*organise* kule vijijini na mijini, wawe na shughuli za kufanya, wapate elimu ya ujasiriamali kwa sababu haiwezekani vijana wote wakaajiriwa katika sekta iliyo rasmi. Kwa hiyo, tukifanya hivyo naamini tutaweza.

Mheshimiwa Spika, hili jambo ni la muhimu na sisi ni lazima tulipe umuhimu wa kipekee kwa sababu vijana wetu ni lazima wapate kitu cha kufanya ama sivyo tutakuwa na tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jenista Mhagama, alizungumza kwamba mipango inaacha sekta isiyo rasmi, nataka kusema kwamba tunayo mipango ya kuisaidia sekta isiyo rasmi kwa kuwaelimisha ili iweze kutoa mazao mazuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Gosbert Blandes na Mheshimiwa Azza Hillary walizungumzia juu ya haja ya kuwa na Viwanda vya Saruji katika Mikoa ya Ziwa. Ni kweli kabisa haja ipo, utafiti ambao umeshafanyika unaleta utata kidogo katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, moja ni kwamba, utafiti ulifanyika katika mikoa yote ya Ziwa juu ya kutafuta namna ya kupata saruji. Kwa mfano, kule Mara utafiti ulifanyika Fort Ikoma katika Wilaya ya Serengeti na Guta katika Wilaya ya Bunda, madini ya mawe ya chokaa ya kuweza kutengeneza saruji yapo lakini ni kidogo, yaani hayawezi kuanzisha kiwanda kwa sababu ni machache.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mwanza hakuna kabisa madini ya namna hiyo, Mkoa wa Shinyanga utafiti ulifanyika katika maeneo ya Mwamala, Ibadakuli, Isaka na Mwamasele na kubaini kuwa kiasi cha malighafi yenye ubora ni kidogo kutosheleza mahitaji ya kiwanda.

Mheshimiwa Spika, Kagera utafiti ulifanyika Biharamulo na kubainika kuwa ubora wa mawe ya chokaa yaliyopo pale ni hafifu, Kigoma utafiti ulifanyika Makere, Kasulu na Bulombora na kubaini kuwa japokuwa mawe ya chokaa yaliyopo ni mengi yana mchanganyiko wa madini ya *magnesium* na hivyo hayafai kwa uzalishaji wa saruji hadi ipatikane teknolojia ya kutenganisha mchanganyiko huu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, juhudi za utafiti zimefanyika kwa nia ya kutaka kuwa na viwanda katika eneo hili ili kupunguza kasi ya usombaji wa saruji kutoka Pwani kwenda katika mikoa ile. Lakini upo mpango mwingine ambao unaonekana unaweza kufanikiwa kule Mwanza wa kutengeneza saruji kwa kutumia kitu kinaitwa *clinker* lakini hii inaweza ikaagizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, ili kiwanda hiki kiweze kulipa pale Mwanza inabidi reli ya kati ifanye kazi, ili malighafi hii iweze kusafirishwa kwa gharama nafuu zaidi na kutengeneza saruji kule Mwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hizo ndiyo juhudi zinazoendelea, lakini tutaendelea na utafiti zaidi kufanyika ili kuona kama inawezekana kuanzisha Kiwanda cha Saruji katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na kupunguza gharama yao ya ujenzi katika mikoa ile.

Mheshimiwa Spika, tumekwishazungumza na Wizara ya Viwanda na tumewaomba waendeleo na utafiti kutafuta namna wanavyoweza kusaidia mikoa ile kwa kupata kiwanda kinachoweza kuzalisha simenti katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ally Keissy alisema kwamba, tunawekeza katika viwanja vya ndege na sisi hatuna ndege, kwa hiyo hakuna haja, hii siyo muhimu sana. Lakini Mheshimiwa Keissy naye anakuja Bungeni hapa kwa ndege, kwa hiyo inasaidia.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, viwanja hivi umuhimu wake ni utalii zaidi. Kama unataka utalii ni lazima uwe na viwanja na ni lazima uwe na ndege ili watalii wakifika lazima waende hasa kama unafanya utalii kule Rukwa, watalii hawawezi kufika Dar es Salaam wakaendesha gari mpaka Rukwa, ni lazima waende kwa ndege, wafike pale wafanye utalii wao halafu waondoke.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ndugu Keissy nadhani atakubaliana nami kwamba, ili tuweze kukuza zaidi utalii hivi

viwanja ni lazima tuviimarisha, lakini vile vile vinasaidia huduma za biashara ya ndani, kwa sababu wafanyabiashara hawa wanaruka kwa haraka zaidi na kufanya shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Zaynab Vullu alisema tuangalie vipaumbele muhimu kama maji, tumeshaviangalia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Keissy anasema vipaumbele siyo tatizo, anasema tuvizingatie na nakubaliana naye.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu anasema kwamba, hakuna mpango madhubuti wa kukuza uchumi ili tuweze kudhibiti thamani ya fedha kwa kuwekeza dhahabu katika Benki Kuu. Mpango huu ulikwishanza na sisi tutalipeleka suala hili Benki Kuu kuona kama wanaweza tena wakalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Peter Serukamba alizungumzia mpango wa kupeleka maendeleo vijijini, nakubaliana naye, lakini mpango huu unaopitishwa hapa leo unawekeza katika maji, elimu na umeme, haya ni mambo yanayokwenda vijijini. Naamini kwamba vijiji vyetu vyote vikipata umeme Tanzania tutakuwa tumepiga hatua kubwa na watu wote watajua sasa tunaelekeza zaidi rasilimali zetu kule vijijini.

Mheshimiwa Spika, lakini nakubaliana naye ni lazima tutilie mkazo suala la vijijini kwani tutapunguza vilevile *Rural-Urban migration*, vijana wanakimbia kule kwa sababu mazingira ya umeme huku mijini yanawapa matumaini kuliko kule. Kwa hiyo, nafikiri uwekezaji huu utasaidia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kidawa Saleh alitaka utolewe ufafanuzi juu ya matumizi ya kawaida, ni makubwa kuliko matumizi ya maendeleo. Nimekwishatoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Limbu alisema miradi ya kimkakati ni mingi sana na kila kitu ni kipaumbele. Hapana, vipaumbele ni vile vile ambavyo nimevieleza na kwa

kweli nimeshasema kwamba, katika nchi kama yetu hakuna namna ambayo unaweza ukaacha hata kimoja; huwezi kuacha elimu, kilimo, miundombinu wala nishati. Kwa hiyo, kuna mambo ambayo unaweza kuacha, mengine huwezi kuacha kabisa. Haya yamekwishasemwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Chacha Nyambari Maliba, alisema kwa nini uchumi wa Tanzania unakua na wananchi wengi wanabaki maskini. Nimekwishalieleza vizuri jambo hili na hatua ambazo Serikali inataka kuchukua ili kupunguza pengo kati ya umaskini na kipato cha watu walio katika Sekta nyinginezo. Hakuna jibu rahisi isipokuwa kuwekeza katika kilimo, kuwasaidia wakulima waache kulima kilimo cha kizamani, walime cha kisasa ili wazalishe zaidi kwa tija.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Felix Bura alisema Serikali itoe fedha za miradi ya maendeleo hasa kwa miradi inayoendelea. Waziri wa Fedha nafikiri atatoa maelezo zaidi jinsi anavyotoa pesa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Martha Moses Mlata alisema Serikali iamue kwa dhati kuwekeza katika maeneo yanayochochea uwekezaji wa biashara. Mfano, Kurasini *Logistics Hurb* na maeneo ya *SEZ* na *EPZ*. Ndiyo maana tumetoa shilingi bilioni 30 kwa ajili ya Kurasini.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo mambo ambayo yamezungumzwa sana. Nasema kwa sababu ya muda, ni vigumu sana kuweza kujibu kila hoja ambayo imetolewa katika Bunge lako Tukufu, ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, ningependa kabla sijamaliza nizungumzie mambo mawili ambayo nisipoyazungumza mpango huu utakuwa bado haujakamilika. Mambo hayo ni kwamba, ili tuweze kuendelea yako mambo ambayo ni lazima tuyatilie mkazo. Moja, Bunge lako Tukufu Wabunge wamezungumza sana juu ya rushwa. Wamesema sana juu ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme hapa kwamba, rushwa ni adui wa maendeleo kabisa, tena nalisema hili bila kutafuna maneno. Kwa sababu kila kitu ambacho kinafanywa kwa rushwa hakiwezi kuwa endelevu na Serikali inatumia fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, tunatumia zaidi ya shilingi trilioni tano kwa ajili ya maendeleo na ukijumlisha na matumizi ya kawaida na mengine yote tunatumia shilingi trilioni 18 katika mpango ujao. Asilimia 70 ya fedha hii itapatikana kupitia manunuzi. Chini ya Sheria inaitwa *Procurement Act*.

Mheshimiwa Spika, ushahidi upo mwingi sasa ambao unaonesha kwamba *Procurement Act* inanunua vitu kwa bei kubwa zaidi kuliko bei ya soko. Nauliza hivi *Procurement Act* yenyewe inanunua wapi na Watanzania wananunua wapi? Kwa nini bei ya maji yanayonunuliwa kwa tenda yawe ghali kuliko maji ninayonunua kutoka mtaani, *why?*

Mheshimiwa Spika, bei zote za vitu vinavyonunuliwa chini ya *Procurement Act*, kwa tenda vyote bei iko juu. Sasa nasema, nadhani wakati umefika tukubali kuitazama upya *The Procurement Act*. Maana hii kitu sasa maana unaweza ukajificha kwenye *Procurement Act* halafu ukawa unaiba kwa mujibu wa Sheria. Ndiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani tutazame vizuri tu, *what is going on?* Maana maendeleo na hasa yale ya vitu, tunatengeneza barabara, tunatumia fedha nyingi kwenye barabara. Tunataka kutumia fedha nyingi sana kwenye *irrigation*. Tunatumia fedha nyingi sana katika miradi ambayo ni *physical*. Lakini kama hali hii ya ulaji rushwa na utendaji mbaya utaendelea, kila kitu tutakachofanya kitakuwa hafifu. Utatengeneza barabara hafifu.

Mheshimiwa Spika, najua yuko rafiki yangu Mheshimiwa Magufuli, anawafuatilia kwa makini makandarasi wale, lakini hata yeye Magufuli hakai kwenye *Tender Board*. Nilikuwa Waziri, Bodi ya Tenda ile

imetengenezewa utaratibu wa ajabu, hata ukiwauliza wanasema, unataka kuvunja sasa Sheria ya *Procurement*.

Mheshimiwa Spika, sasa hii Sheria ya *Procurement* huulizi swali. Ukiuliza ni kuingilia. Nasema hiki kitu lazima kitazamwe ama sivyo unaweza ukampa mtu tenda ya barabara anatengeneza, kule anakotoka inabomoka kabla hajafika mwisho. Unajenga jengo ambalo lingedumu miaka 50, 100 linadumu miaka kumi, linapata nyufa, linaelekea kuanguka.

Mheshimiwa Spika, tukiendelea kwa namna hiyo tuna-*erode* kabisa maendeleo ya nchi yetu. Sasa jambo hili siyo la kulionea haya, tunalionea haya, tunamwonea haya nani? Nadhani tuwaambie Watanzania wote tukatae jambo hili na wote tuwe Polisi wa jambo hili. Kama jambo linafanyika na wewe una ushahidi mzuri, useme hapa bwana mambo hayaendi vizuri, maana nchi hii ni yetu wote na maendeleo haya ni maendeleo yetu wote.

Mheshimiwa Spika, tusipofanya hivyo, tutakuwa kila siku tuna-*vote* pesa hapa. Lakini hakuna kinachofanyika au kinafanyika, lakini kwa mazingira hafifu. Kwa hiyo, nataka niliseme jambo hili kama jambo moja katika mambo ambayo hatuwezi kuyaachia na kuyanyamazia.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ambalo nalo ni muhimu sana, ni amani. Hili nalo tusilionee haya. Amani ina uhusiano na maendeleo, amani ikikosekana hakuna maendeleo na maendeleo yakikosekana hakuna amani. Amani na maendeleo ni pacha. Ukikosa maendeleo, watu watasema hakuna maendeleo kuna nini, lakini vile vile amani ikikosekana, hakuna mtu atafanya kazi. Lazima tukubaliane hili kama nchi, tuache hapa ushabiki wa vyama, maana amani haina vyama, amani ni ya Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiivuruga unavuruga amani ya Watanzania wote na tuseme hivi sasa sisi tulichaguliwa hapa kuvuruga amani au kuilinda. Hivi ni chama gani kinaweza

kwenda kwa Watanzania kikawaambia tuchagueni sisi amani itakosekana. Hebu jaribu kama watakupa kura. Lazima tukubali hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa juzi kuliulizwa swali hapa, Mheshimiwa Waziri Mkuu akasema lazima tuchukue hatua dhidi ya wanaokaidi. Mmoja akasema Katiba, sasa na mimi nauliza kifungu kipi cha Katiba kinaruhusu watu kukaidi? Namba ngapi? Maana lazima tuelewane, maana kukaidi ni kuvunja Sheria na Bunge hili kazi yake ni kutunga Sheria.

Mheshimiwa Spika, sasa unatunga Sheria halafu tena unalalamika watu wakishughulikiwa, wale wanaokaidi Sheria uliyotunga. Nasema, wale wanaotaka, maana Katiba ni yetu wote vile vile. Unajua ni sawa sawa na kuchukua *Quran* au Biblia ukasoma aya moja tu halafu ukaunda Msikiti wa kwako kwa aya moja, bila kusoma zingine au ukachukua Biblia ukasoma sentensi moja tu ukasema hivi ndivyo Biblia inasema kwa hiyo unaunda Kanisa kwa sentensi hiyo hiyo, haiwezekani. Lazima usome yote.

Mheshimiwa Spika, sasa katika suala hili tusijifiche sana katika kitu kinachoitwa haki za binadamu. Haki zako wewe zinaweza kuwa zinapingana na haki zangu na Katiba haiwezi kukulinda wewe tu katika kuvunja haki zangu na lazima haki zangu zilindwe. Mimi nauza nyanya, wewe unafanya maandamano, unakanyaga nyanya zangu. Unasema nilikuwa natekeleza demokrasia, demokrasia ya kukanyaga nyanya zangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lazima tu-*balance*, tujue tunafanya ghasia, watu wetu wanapoteza maisha, halafu tunaanza kubishana. Tunabishana wakati wale wamekufa. Kwa nini tusifanye mambo kwa utaratibu ambao unaweza ukafanya amani ikatawala katika mazingira yetu tunapofanyia shughuli zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani, hatuwezi kusema turuhusu nchi yetu ifanye majaribio ya fujo na ghasia, haiwezekani. Kwa hiyo ni *obligation* ya viongozi wote, ni

obligation ya vyama vyote vya siasa kuhakikisha kwamba amani inakuwepo ili maendeleo yawepo na hapo hakuna salia Mtume, hatuwezi kujificha tu katika kusema ooh wanazuia *democracy*, *democracy* inasema tujadiliane na tukiamua tutekeleze tulichoamua. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, marehemu Julius Nyerere alisema *democracy* bila nidhamu ni ghasia. Mfumo wa Vyama Vingi tunashindana kwa Sera na hoja. Kwani kuna ubaya gani kama Chama cha Siasa kitasema nyinyi mlisema mtafanya elimu na mna matatizo. Tukuambie wewe mbadala wako nini? Hakuna tatizo. Nenda popote sema tu na sisi tutatoka nyuma tutajibu.

Mheshimiwa Spika, wale wanaotawala watasema bwana tumeanzisha Shule za Kata zimekuwa nyingi kweli mfumo huu wa kupanua elimu umeshusha, sasa tunapandisha kiwango. Tutajibu, lakini na wewe uwaambie wewe utafanyaje utafuta za Kata, *alternative policy*, ndivyo tunavyoshindana.

Mheshimiwa Spika, lakini tukishindana utaboresha kwa shule za Kata ambazo Serikali tulijenga wenyewe, tutaboresha wenyewe. Nimesikia mtu ananijibu amekaa na mimi namjibu nimesimama. Nasema hoja kwa hoja na fujo haiwezi kuwa hoja. Fujo haiwezi kuwa hoja; toa hoja, jibu hoja.

Mheshimiwa Spika, waliotufundisha demokrasia hawa wakubwa hawa Wamarekani, Waingereza wao ni hoja, tena hoja ziko Bungeni. Wanabishana, hata kile kipindi cha *Prime Minister's Question Time* kule Uingereza, *The Leader of Opposition* ndiyo huwa anauliza, *ooh Mr. Prime Minister you promised this, you have not delivered. What is happening?*

Yeye anajibu anasema *we have done this, and this, and this and we tend to do this*. Ndivyo wanavyofanya waliotufundisha. Hawapigani, sasa sisi tena, au wanafunzi wanakuwa wajuzi kuliko Walimu. Huwa inatokea, lakini kama mfumo wenyewe ni huo, hiyo ni *problem*. (Makofi)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, nilitaka nizungumzie mambo haya katika kuhitimisha, lazima tukae rushwa, kwa sababu itapunguza thamani ya maendeleo yetu. Amani lazima tui-*preserve* na tusitumie sababu yoyote ya kuvunja amani. Sasa kama watu wanakaidi, halafu wakikadi tunasema...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Kengele ya pili hiyo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):
Sasa kila mtu atakaidi.

SPIKA: Kengele ya pili hiyo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Hiyo ni ya pili?

SPIKA: Ndiyo

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuungane katika kuupitisha mpango huu ili uanze kutekelezwa. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono. Sasa nitamwita mmoja wa Manaibu Waziri wa Fedha, nitakupa dakika 35.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):
Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja kwa kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya masuala yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja iliyozungumzia kuwa Serikali itoe tamko juu wa watumishi wa *TRA* na Bandari waliohusika na tuhuma za makontena 500 na kuhamishwa badala ya kufukuzwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa jibu kuwa, katika sakata la makontena 500 katika Bandari ya Dar es Salaam, jumla ya watumishi nane wametuhumiwa kuhusika na upotevu wa kodi za Serikali pamoja na tuhuma za rushwa kwa kushirikiana na Mawakala wasio waaminifu, kuondosha makontena Bandarini bila ya kulipa kodi stahiki.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tuhuma hizi Mamlaka ya Mapato imeanza kufanya uchunguzi wa kina kwa watumishi wake waliohusishwa na utoaji wa makontena 500 katika Bandari ya Dar es Salaam. Mara baada ya uchunguzi huo kukamilika, hatua stahiki za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya watumishi hao.

Mheshimiwa Spika, ili kuruhusu uchunguzi huo kuendelea Mamlaka ya Mapato Tanzania imechukua hatua za awali kwa kuwaondoa wafanyakazi hao katika maeneo ambayo walikuwa wanafanyia kazi ili kuruhusu uchunguzi kufanyika na hatua stahiki kuchukuliwa. Hili ni jambo la kawaida wakati wote watu wanapofanyiwa uchunguzi ili wasiweze kuingilia uchunguzi huo.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato inao utaratibu ambao umeainishwa kwenye Kanuni za Utumishi yaani *Staff Regulations* ambapo mtumishi yeyote anayejihusisha katika upotevu wa mapato ya Serikali anachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kumwondoa katika ajira na hata kushtakiwa. Kuanzia mwezi Oktoba, 2011 mpaka sasa jumla ya watumishi 15 walifukuzwa kazi kwa sababu mbalimbali ikiwemo ya kuikosesha Serikali mapato yake.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia vile vile kuna hoja kuwa *TRA* iendelee kuboreshwa ili iweze kukusanya mapato ya kutosha. Kwa kujibu hoja hii, Serikali inakubaliana na hoja

ya kuboresha Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Katika kutekeleza hili *TRA* hufanya kazi kupitia mipango ya miaka mitano ya maboresho.

Mheshimiwa Spika, Mpango huu wa Nne wa 2013/2014 hadi 2017/2018 utanza kutekelezwa Julai, 2013, ambao utaiwezesha Mamlaka kufikia dira yake ya kuongeza mapato ya kodi kutoka shilingi trilioni 10 hadi shilingi trilioni 18.8 mwaka 2017/2018, sawa na ongezeko la asilimia 88, katika kipindi cha miaka mitano. Mapato hayo ni sawa na asilimia 20 ya pato ya Taifa. Kiwango ambacho kitakuwa juu ya wastani wa nchi maskini zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa vile vile kuna hoja ya kukithiri kwa rushwa miongoni mwa watumishi wa *TRA* ambako kunasemekana ndiyo kunachangia katika ufanisi mdogo wa ukusanyaji wa mapato ya kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa majibu, suala la uadilifu wa watumishi ni moja ya changamoto ambazo *TRA* inazikabili kwa nguvu zote. Mamlaka imekuwa ikitekeleza mkakati wa kusimamia maadili ya wafanyakazi na kuimarisha uwajibikaji wa viongozi. *TRA* imeainisha maadili ya kimsingi ya wafanyakazi katika *Code of Ethics* ambayo kila mtumishi anatakiwa kuwa nayo ili kuhakikisha anafanya kazi kwa bidii na maarifa kwa minajili ya kuongeza tija. Ufanyakazi kwa uadilifu, bidii na heshima kwa wateja ni miongoni mwa maadili ya msingi ambayo *TRA* inayasimamia.

Mheshimiwa Spika, kuanzia 2008, *TRA* imeanzisha Kitengo Maalum ambacho kinaitwa *Internal Affairs Unit* kinachofanya kazi chini ya usimamizi wa Kamishna Mkuu, kushughulikia masuala ya uadilifu wa watumishi wake ndani ya Mamlaka. Kwa sasa Kitengo hicho kimepandishwa hadhi na kuwa Idara kamili kwa lengo kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, *TRA* imeandaa Sera kwa lengo la kuongeza ufanisi. Aidha *TRA* imeandaa Sera ya kupambana na rushwa yaani *TRA (Anti-Corruption Policy)* kuanzia mwaka 2010 ambayo inatekeleza ili kuhakikisha kuwa

vitendo vya aina yoyote ya rushwa vinashughulikiwa na hatua stahiki kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, *TRA* imeunda Kamati za maadili katika ngazi za Makao Makuu, yaani *Management Ethics Committee*, Mikoa na Wilaya. Kamati ya Bodi ya Maadili yaani *Standing Committee* hupitia Taarifa za Maadili ya wafanyakazi kila robo mwaka na kuchukua hatua dhidi ya wafanyakazi wanaobainika kuwa na makosa; ikiwemo kushushwa vyeo, kufukuzwa kazi na wakati mwingine kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola kupelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kati 2011 hadi sasa, wafanyakazi 15 wamefukuzwa kazi kutokana na makosa haya. Hata suala la makontena 500 ambayo Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia, nalo linafanyiwa kazi katika utaratibu huu huu.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato imeanza kufanya uchunguzi wa kina na baada ya uchunguzi huu kukamilika, *TRA* itachukua stahiki za kinidhamu. Kwa kupitia Idara yake inayoshughulikia masuala ya maadili *TRA* imeimarisha ushirikiano na vyombo vya kusimamia Sheria, ikiwemo TAKUKURU, Kitengo cha Utawala Bora katika Ofisi ya Rais, Usalama na Polisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, *TRA* inashiriki katika majukwaa mengine ya Kimataifa yanayohusu masuala ya maadili ya watumishi kama vile Jukwaa la Maadili kwa Watumishi wa Kodi wa Jumuiya ya Afrika Mashiriki, Kikosi cha Wataalam cha Umoja wa Afrika katika masuala ya maadili na vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, *TRA* pia ina sera na utaratibu wa kupokea na kushughulikia malalamiko kutoka kwa walipa kodi na wadau wengine juu ya masuala ya ukwepaji kodi au tuhuma za rushwa dhidi ya watumishi wa *TRA* chini ya *TRA Whistle Blowing Policy*.

Mheshimiwa Spika, tunatoa rai kwa wananchi wote, watupe ushirikiano wao kwa kutoa Taarifa zozote za ukiukwaji wa maadili unaofanywa na wafanyakazi wa *TRA* kwa Waziri au Kamishna Mkuu ili hatua stahili zichukuliwe dhidi yao.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zinazochukuliwa ni pamoja na uchunguzi kwa watumishi wapya kabla hawajaajiriwa (*Vetting*). Kuwa na utaratibu wa kutowaacha watumishi kukaa muda mrefu katika Kituo kimoja na kuwataka watumishi wote kutoa tamko la mali zao kila mwaka na kuzifanyia uhakiki.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja vile vile juu ya mapato ya kodi kwenye Makampuni ya Simu pamoja na utaratibu wa ukusanyaji wake.

Mheshimiwa Spika, kwa majibu, Sheria zote za kodi ikiwa ni pamoja na Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004, zinafuata utaratibu wa walipa kodi kujikadiria kodi wenyewe (*Self Assessment System*). Utaratibu huu unatumika katika nchi nyingi ulimwenguni, ambako muda, rasilimali watu, fedha na vitendea kazi hutumika kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pamoja na utaratibu huu, *TRA* wameweka utaratibu wa wazi wa kufanya ukaguzi wa taarifa za walipa kodi katika vipindi mahsusi vilivyopangwa kutegemea na aina ya biashara, vihatarishi na tabia ya mlipa kodi.

Mheshimiwa Spika, Serikali, imekamilisha ununuzi wa mtambo unaojulikana kama *Telecommunication Traffic Monitoring System*, utakaotumika na *TCRA* na *TRA* katika kutambua aina na kiasi halisi cha miamala inayofanywa na Makampuni ya Simu.

Mheshimiwa Spika, mtambo huu unatarajiwa kufungwa mwezi Julai, 2013 yaani mwezi ujao; kuwepo kwa mtambo huu kutaiwezesha Serikali, kujiridhisha na mapato halisi ya Makampuni ya Mawasiliano ya Simu.

Mheshimiwa Spika, vile vile kulikuwa kuna hoja kuwa, Serikali, idhibiti udanganyifu katika ukadiriaji wa kodi (*False and under declaration*) na kungeza ufanisi wa kuondoa ma-*container* bandarini.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali hili, napenda nitoe ufafanuzi kuwa, Idara ya Forodha ilipangiwa kukusanya kiasi cha 41% ya mapato yote yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 na sio 20%.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na wimbi la ukwepaji kodi linalofanywa na wafanyabisahara wachache wasio waaminifu, wakishirikiana na baadhi ya watumishi wa Mamlaka ya Mapato, *TRA* imeanzisha mfumo mpya wa udhibiti wa ma-*container* bandarini.

Mheshimiwa Spika, mfumo huo (*Cargo Management System*) huratibu ma-*container* tokea yanaposhushwa melini mpaka yanapotoka nje ya bandari ama bandari kavu (*ICD*). Halikadhalika Mamlaka imeimarisha ukaguzi wa ma-*container* bandarini kwa kungeza idadi ya wakaguzi, ambapo wenye mali, Mawakala pamoja na watumishi kutoka taasisi na vyombo vingine vya Serikali, wanakuwepo ili kuhakikisha kwamba, maslahi ya kila mmoja yanalindwa.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa hatua zilizochukuliwa kuondoa ucheleweshaji, baadhi ya mizigo hukaguliwa kwa kutumia *X-Ray Scanner*. Mizigo ambayo taswira yake haitiliwi mashaka huruhusiwa kuondolewa bandarini; mizigo ambayo hutiliwa mashaka, hulazimika kufanyiwa ukaguzi kwa kufungua ma-*container* na kufanyiwa *physical examination*, ili kuhakikisha kuwa hakuna ucheleweshaji Maofisa Wakaguzi husimamiwa kwa karibu, ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji wao.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja vile vile kuwa, kazi za wasanii zinaibiwa na wajanja na Serikali, ithibitishie ubandikaji wa *sticker* katika kazi za wasanii na ishughulikie hao wajanja kwanza.

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa *stamp* za kodi kwenye tasnia ya filamu na muziki umetokana na kilio cha muda mrefu kutoka kwa wasanii wenyewe, kutokana na wizi wa kazi zao katika mtiririko mzima (*The whole value chain*) wa kazi za tasnia hizi.

Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na uanzishwaji wa *stamp* za kodi kwenye bidhaa za filamu na muziki, kama wasanii walivyoomba, ili kuweza kubaini na kuzuia wizi na urudufishaji wa kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, hivyo, katika bajeti ya Serikali ya Mwaka 2012/2013, Bunge lako Tukufu lilidhinisha utaratibu wa kubandika *stamp* za kodi katika kazi zote za wasanii wa filamu na muziki, ikiwa ni pamoja na kazi zinazolingizwa kutoka nje. Utaratibu huu ulianza kutumika rasmi kuanzia mwezi Januri 2013, lengo ni kuzuia bidhaa zote zisizokuwa na *stamp* za kodi kwenye soko la Tanzania ifikapo mwezi Julai 2013.

Mheshimiwa Spika, suluhisho si kusitisha ubandikaji wa *stamp* za kodi, bali kuhakikisha hatua za Kisheria zinachukuliwa kwa wale wote watakaobainika kuuza kazi hizo bila ya kubandikwa *stamp* za kodi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyotolewa ilikuwa ni Serikali, ichukue jitihada za makusudi kuhakikisha kuwa, madeni katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi za Serikali, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa yanadhibitiwa na kumalizika.

Mheshimiwa Spika, Serikali, imeendelea kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya kulipa madai mbalimbali ya watumishi na wazabuni, yaliyohakikiwa. Aidha, ili kuhakikisha kuwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi za Serikali, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, haziingii tena katika madeni na kwamba, bajeti inatekelezwa kama inavyokusudiwa Serikali, itawajengea uwezo watumiaji wa mfumo wa malipo (*IFMS*) kuhusu maeneo yaliyoreshwa katika toleo la *EPICOR 9.05*, ili kuhakikisha kuwa, ulipaji wa huduma unafanyika kwa kuzingatia mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali, kupitia Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani, imeendelea kuhakiki madai mbalimbali yaliyowasilishwa na Wizara mbalimbali ili kujiridhisha na uhalali wake kabla ya malipo. Baada ya uhakiki huo kukamilika, Serikali italipa madeni hayo chini ya Fungu 21, chini ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni kuwa, Kada ya Ukaguzi wa Ndani iimarishwe ili kudhibiti mapato na matumizi ya fedha na mali za umma.

Mheshimiwa Spika, Serikali, imeendelea kuimarisha Kada ya Ukaguzi wa Ndani kwa kuendelea kutoa mafunzo ya ukaguzi wa kawaida na ya kiufundi. Kuendelea kutoa miongozo ya kiutendaji na kuhakikisha kunakuwepo na ubora katika utendaji kazi katika Kada ya Ukaguzi wa Ndani.

Mheshimiwa Spika, Serikali, itaendelea kuongeza idadi ya Wakaguzi wa Ndani katika Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa lengo la kuwa na Wakaguzi wa Ndani wa kutosha na wenye sifa. Hatua hii itasaidia kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani ili kusimamia vyema utekelezaji wa mipango iliyowekwa kupitia bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja vilevile kuhusiana na uhakiki wa madeni ya ndani. Serikali ina utaratibu wa kudumu wa kuhakiki madeni kabla ya kulipa. Kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, Mkaguzi Mkuu wa Ndani, alianza kazi ya kuhakiki madai yaliyowasilishwa. Kazi hii ilianza mwanzoni mwa Juni, 2013 na inatarajiwa kukamilika mwisho wa mwezi Julai, 2013. Baada ya zoezi hili kukamilika Serikali, itaweka utaratibu wa kulipa kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni fedha zinazotengwa kwa ajili ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitolewe zote na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Serikali hutekeleza bajeti kila mwaka kwa kuzingatia viwango vya mapato na matumizi vilivyoidhinishwa na Bunge. Ukusanyaji wa mapato hufanyika kwa kipindi cha miezi 12 na hivyo, kufanya Serikali, itoe fedha za matumizi kwa kipindi cha miezi 12.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali, imekuwa ikitoa fedha kulingana na upatikanaji wake katika mapato ya ndani pamoja na mikopo na misaada kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka ya hivi karibuni utekelezaji wa bajeti umekuwa ukikabiliwa na changamoto zilizo nje ya uwezo wa Serikali, ambazo husababisha baadhi ya Mafungu kutopata fedha zote, ikiwa ni pamoja na Mikoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa sababu hizo ni pamoja nja Wadau wa Maendeleo kutotoa fedha zote kwa wakati, baadhi ya mapato kutopatikana na kujitokeza kwa baadhi ya mahitaji ya dharura wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya Mwaka 2013/2014, Serikali imechukua tahadhari ya kukabiliwa na changamoto hizo ili zisiathiri utoaji wa fedha katika Mikoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja vile vile kuwa, Serikali Kuu isiweke ukomo wa bajeti kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ili ziweze kupanga vipaumbele wanavyotaka kuvitekeleza.

Mshimiwa Spika, jibu ni kuwa, vyanzo vya mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, vinatoka katika maeneo makuu mawili; mapato yanayokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zenyewe na ruzuku kutoka Serikali Kuu. Kwa upande wa mapato yanayokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Serikali Kuu haiweki ukomo na badala yake Mabaraza ya Madiwani wa Mamlaka hizo ndio yenye mamlaka ya kuamua matumizi ya fedha zinazopatikana kila mwaka kutoka kwenye vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Spika, ruzuku ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka Serikali Kuu, hutolewa kulingana na uwezo wa fedha zinazopatikana kutoka vyanzo vya ndani na nje kila mwaka. Mfumo wa bajeti unaotumika unailazimu Serikali, kutekeleza vipaumbele vinavyowiana na uwezo wa mapato kwa mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, msingi huu ndio unaosababisha kuweka ukomo na kutaka kila Fungu lielekeze fedha kwenye maeneo ya vipaumbele yatakayokuwa na tija kulingana na majukumu ya msingi yalivyokabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo Mamlaka za Serikali za Mitaa hupewa ukomo wa bajeti wa ujumla (*Global Ceiling*) kwa kila Idara pamoja na miradi ya maendeleo kwa kuzingatia Kanuni na vigezo vya ugawaji wa rasilimali fedha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupewa ukomo huo, kila Mamlaka hutenga fedha kwenye shughuli mbalimbali zilizopitishwa na Baraza la Madiwani kwa kuzingatia Sera ya Ugatuuji wa Madaraka na Rasilimali, ambapo kiasi cha fedha kwa kila shughuli au mradi huamuliwa na Mamlaka yenyewe.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Hazina huendelea kutoa ushauri wa kuzingatia Sheria, Kanuni na Viwango vya Kitaifa, kulingana na maeneo yaliyoainishwa kwenye Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa vile vile kuna hoja ya malipo ya Wastaafu yalipwe kwa wakati. Malipo ya kustaafu kwa Watumishi wa Umma yanalipwa na Wizara ya Fedha pamoja na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, wastaafu wanaolipwa na Wizara ya Fedha ni wafuatao; watumishi waliostaafu au kufariki kabla ya terehe 1 Julai, 2004 baada ya Mfuko wa *PSPF* kuanza jukumu la kulipa Mafao ya Kustaafu. Wanajeshi na Usalama wa Taifa wanaoendelea kustaafu kwa sababu, wao sio wanachama wa Mifuko. Watumishi wenye mamlaka mbili za

ajira sehemu ya Serikali Kuu, hulipwa na Wizara ya Fedha. Kwa mfano, Mtumishi aliyeajiriwa katika Mamlaka ya Serikali Kuu na kuhamishiwa Serikali za Mtaa au Shirika la Umma, sehemu ile aliyokuwa katika Serikali Kuu, hulipwa na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Viongozi wa Kitaifa ambao ni Marais Wastaafu, Mawaziri Wakuu Wastaafu, Viongozi wa Kisiasa Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na Watumishi wa Serikali wenye Ajira ya Mikataba.

Mheshimiwa Spika, wastaafu wengine wote wanalipwa na Mifuko ambayo wastaafu ni wanachama. Sababu zinazofanya malipo ya kustaafu yalipwe kwa kuchelewa ni pamoja na uwasilishaji wa nyaraka pungufu, uwasilishaji wa kumbukumbu kwa kuchelewa kunakofanywa na Waajiri wenyewe wakati mfanyakazi anapokuwa tayari amekaribia kustaafu.

Mheshimiwa Spika, malipo ya pensheni hulipwa kwa vipindi vya miezi mitatu-mitatu kuanzia Januari 2012. Katika utaratibu huu Wastaafu wanalipwa pensheni ya miezi miwili mapema (*in Advance*). Kwa mfano, pensheni inayolipwa mwishoni mwa mwezi Julai, inajumuisha malipo ya miezi ya Agosti na Septemba. Kwa utaratibu huu madai ya kulipwa pensheni kwa kuchelewa sio ya kweli, kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile kulikuwa kuna hoja kuwa Serikali, itengeneze jedwali la bei elekezi za ununuzi wa umma, ili zilingane na bei ya soko na ianze kutumika katika bajeti ya 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kupitia Sheria Mpya ya Ununuzi wa Umma, Namba 7 ya 2011, ambayo itaanza kutumika hivi karibuni, Serikali imeweka vifungu mahususi vinavyozielekeza Taasisi za Umma kutumia bei elekezi wakati wa kufanya ununuzi wa vifaa na huduma mbalimbali. Kwa utaratibu huu mpya, Taasisi za umma zitanunua vifaa na huduma

zinazotumika mara kwa mara kwa kuzingatia jedwali la bei elekezi litakaloandaliwa na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa vile vile kuna hoja ya je, Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma 2011 zitatolewa lini? Wizara ya Fedha, tayari imeandaa Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011. Maandalizi ya Kanuni hizi yameshirikisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na Wadau mbalimbali wa Sekta ya Ununuzi.

Mheshimiwa Spika, uandaaji wa Kanuni hizi umechukua muda mrefu kutokana na matakwa ya Sheria hii ambayo yanaendelea kuandaliwa kwa kina na taratibu maalum kwa sekta maalum (*Specific Procurement Methods*), kwa mfano, sekta ya miradi ya *PPP*.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya taratibu maalum kwa aina maalum ya sekta, yalihatiji kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali kwa umakini, ili kuepusha migongano kati ya Sheria Mama pamoja na Kanuni hizi. Aidha, baada ya kupitia Sheria husika, baadhi ya Sheria, kwa mfano Sheria ya *PPP*, imefanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2013, inayotarajiwa kujadiliwa na kupitishwa na Bunge, baada ya kuhitimisha Hotuba ya Bajeti na kuanza kutumika tarehe 1 Julai, 2013. Kanuni za Sheria ya Ununuzi ya 2011 zinatarajia kuanza kutumika tarehe 1 Julai, 2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali, pia ilipokea hoja kuwa, Serikali iuze vifaa chakavu kwa ushindani na uwazi. Mali za Serikali, hupatikana kwa njia nyingi, ikiwa ni pamoja na ununuzi kupitia zabuni, nukuu-bei (*Quotations*), ununuzi wa moja kwa moja (*Direct Procurement*), chanzo kimoja (*Single Sourcing*), Wafadhili, misaada na mikopo au kwa kutaifisha kwa mujibu wa Sheria, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha, mali za Serikali, zisizohitajika kutokana na uchakavu, huuzwa kwa njia ya zabuni za wazi, mnada wa hadhara, kuuzia watumishi au kuvihamishia katika Ofisi nyingine zenye uhitaji,

baada ya kupata kibali cha Mlipaji Mkuu wa Serikali. Mali hizi ni pamoja na magari, pikipiki, samani, mitambo, vifaa vya ofisi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, vile vile kulikuwa kuna hoja ya kuwa, zoezi la fidia kwa waathirika katika ujenzi wa barabara zinazojengwa chini ya ufadhili wa *MCC* za Pemba Kaskazini, ukamilishwe.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya mali zilizoathiriwa na ujenzi wa barabara zote tano za Pemba Kaskazini zenye urefu wa kilomita 35 ilifanywa na fidia kulipwa kulingana na tathmini ya mali na mpango wa fidia. Hata hivyo, kuna nyumba chache ambazo hazikuwa katika mpango wa fidia wa awali, ambazo zilikuwa karibu sana na eneo la hifadhi ya barabara na hivyo kuathirika. Tayari tathmini imefanyika na hatua za uhakiki zinaendelea, ili malipo kwa wahusika yafanyike kulingana na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, vilevile kulikuwa kuna hoja kuwa, Serikali inashauriwa iongeze fedha kwenye Mifuko ya Wanawake na Vijana na iboreshe utaratibu wa kukopesha na kuhakikisha marejesho yanafanyika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, majibu ya Serikali ni kuwa; katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Serikali, imetenga shilingi bilioni mbili kuwezesha Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na shilingi bilioni 6.1 kuwezesha Mfuko wa Maendeleo wa Vijana. Fedha hizi ni mtaji ambao utatumika kukopesha walengwa na marejesho yatatumika kukopesha walengwa wengine zaidi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, zitaweka utaratibu wa uwazi wa kukopesha na kutumia fedha hizo kwa kuwashirikisha wadau muhimu, zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kuwa jicho la pili katika kuhakikisha mikopo hii inatumika vizuri na inaleta maendeleo tarajiwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja pia kuwa, Serikali iwasilishe Taarifa ya Mashirika yaliyofilisiwa. Orodha ya mashirika yaliyofilisiwa hadi kufikia Mei 2013, ni 46. Kati ya hayo, 10 ufilisi wake ulikamilishwa na *CHC (Consolidated Holdings Company)* na mengine 36 ufilisi wake ulikamilishwa na *PSRC*. Aidha, mashirika 18, ufilisi wake bado unaendelea, orodha ya mashirika haya inapatikana iwapo Waheshimiwa Wabunge watahitaji.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja vile vile kuwa, Serikali, ishughulikie madai ya watumishi kwa wakati pamoja na kuzingatia makato sahihi ya mikopo wanayodaiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali, imeendelea kulipa madai ya malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wa Serikali na Taasisi; malipo hayo hulipwa kupitia mishahara ya watumishi. Katika Mwaka huu wa Fedha 2012/2013, jumla ya shilingi bilioni 32.7 zimelipwa kama malimbikizo kwa watumishi wa Serikali na taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu baadhi ya watumishi kukatwa mishahara kwa visingizio vya makampuni binafsi ya ukopeshaji utaratibu ni kwamba, watumishi ndio wanaoingia mikataba na taasisi za fedha, ili kupata mikopo husika. Waajiri ndio wanaoingiza makato hayo ya kulipa mfumo wa *Lawson* ambao kwa sasa umesambazwa kwa waajiri wote nchini, ili kushughulikia masuala yote ya mishahara kwa watumishi wa Serikali na taasisi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja vile vile inayohusiana na kuwa, Serikali isaidie kudhibiti asasi zisizo za Kiserikali (*NGOs*) na *Microfinance Institutions* zinazokopesha wananchi kwa riba kubwa kati ya 25% hadi 30%.

Mheshimiwa Spika, Serikali, inafanya mapitio ya Sera ya Taifa ya taasisi ndogo ndogo za huduma za fedha ya 2002. Lengo la mapitio hayo ni kuiboresha Sera hiyo, ili iweze kuendana na mabadiliko yaliyopo katika mfumo mzima wa sekta ya fedha na kuleta urahisi zaidi katika upatikanaji wa huduma za kifedha nchini.

Mheshimiwa Spika, mapitio hayo yatakamilika katika mwaka 2013/2014. Vile vile baada ya kuandaa Sera hiyo Serikali, itatunga Sheria ya Kusimamia Taasisi hizo na kuweka utaratibu wa usimamizi, udhibiti na utoaji wa leseni pamoja na kiwango cha riba.

Mheshimiwa Spika, hapa ningependa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Devatha Likokola. Kwa kweli, Mheshimiwa Mbunge huyu, anajitahidi sana kusukuma hili suala zima la *Micro Finance* kwa ajili ya Wajasiriamali wadogo wadogo. Tunastahili sana kumpongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja vile vile ya taasisi ndogo za fedha zinazokopesha Walimu na Watumishi wa Afya kwa riba kubwa hadi 30%. Kwa nini *NMB* isikopeshe wakati Serikali ina hisa *NMB*?

Mheshimiwa Spika, Serikali, inatambua umuhimu wa kuwepo kwa vyanzo mbalimbali vya utoaji mikopo kwa shughuli za kiuchumi, ikiwa ni pamoja na kuwakopesha watumishi wa Serikali, ili kutia chachu kwenye ukuaji wa uchumi. Kwa kulitambua hili, Serikali, kwa kushirikiana na Benki Kuu, inaendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ili kuweza kuongeza ushindani katika sekta hii ya fedha.

Mheshimiwa Spika, labda kwa ushauri tu ni kuwa, kwa kiasi kikubwa wafanyakazi wenyewe wanaokwenda kukopa katika taasisi hizi wafanye tathmini ya kutosha kabla ya kuanza kuingia kwenye mikopo ili kujidhihirishia kuwa mikopo hiyo haitakuwa mzigo kwao wakati wanapoingia katika mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, mabanki yote yameendelea kutoa mikopo kwa kasi nzuri ikiwa ni pamoja na benki ya *NMB* ambayo imejikita kwa kiasi kikubwa katika kutoa mikopo kwa wafanyakazi wa Serikali. Hadi kufikia Mei 2013 jumla ya shilingi bilioni 739.3 zilikuwa zimekwishatolewa kwa jumla ya wafanyakazi 278,338 kutoka shilingi bilioni 263 mwezi Desemba, 2008; ambalo ni ongezeko la shilingi bilioni 476.3 sawa na 181% kwa kipindi cha takribani miaka minne na

nusu tu. Hii ni wazi kwamba benki ya *NMB* imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kukopesha na kuboresha maisha ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja kuwa huduma za Benki ya Wanawake ifike hadi vijijini. Serikali inatambua umuhimu wa kupeleka Benki ya Wanawake katika maeneo ya vijijini ikiwemo Mkoa wa Iringa, naamini hii ilitolewa na Mheshimiwa Lediana ambaye alikuwa anataka kuhakikisha kuwa wanawake wa Iringa ambao ni wajasiriamali wazuri na wenyewe wanapata huduma hii ya kibenki. Ni imani ya Serikali kwamba benki hii itaendelea kupanua huduma zake ili kuwafikia wananchi walio wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja vile vile kuhusu uhalali wa Bodi ya *PSPF*. Napenda kutoa ufafanuzi juu ya muundo wa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Umma yaani *PSPF* kulingana na mabadiliko ya Sheria za Mifuko ya Pensheni ya mwaka 2012 yaani *Social Security Laws Amendment Act* ya 2012.

Mheshimiwa Spika, muundo wa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko unatokana na kifungu 52 (1) cha Sheria ya Mafao ya Kustaafu kwa Watumishi wa Umma, Sura namba 371 yaani *Public Service Retirement Benefits Act, Cap 371 Revised Edition* 2002 na kurekebishwa na kifungu namba 136(a) cha Sheria za Mifuko ya Pensheni ya mwaka 2012 kama ilivyorekebishwa.

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki kimetaja wajumbe wa Bodi ya Wadhamini kwa nyadhifa zao. Kwa hiyo, Bodi iliyopo inakidhi matakwa ya Sheria kwani wajumbe wake wana sifa kisheria. Hivyo basi kwa mujibu wa Sheria ya *PSPF*, Bodi ya *PSPF* kwa jinsi ilivyo sasa hivi, ipo kihalali.

Mheshimiwa Spika, isipokuwa naharakisha kusema kuwa, kama kuna haja ya kubadilisha kutokana na kuwa, sasa hivi kuna mdhibiti wa Mifuko ya Hifadhi, basi hilo nalo linaweza likaangaliwa na kuona jinsi gani ya kuboresha Bodi hiyo ili kusiwe na mgongano wowote wa maslahi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja nyingine ambayo inazungumzia fedha za mabilioni ya JK na za *TASAF* kuwa, ziwekewe utaratibu ili zitumike ipasavyo na kurejeshwa yaani ziwekewe utaratibu wa *revolving fund*. Majibu ni kuwa, Mfuko wa JK, *TASAF* na Mfuko uliopo wa Wizara ya Kazi, yote ilianzishwa kwa malengo tofauti na taratibu za utekelezaji wake pia zinatofautiana.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi, maarufu kama mabilioni ya JK ulianzishwa kwa lengo la kuwakopesha wajasiriamali wadogo kupitia kwenye benki ya *CRDB*, *NMB*, Benki za Wananchi na *SACCOS*. Fedha hizo huendelea kukopeshwa na kurejeshwa kwa utaratibu wa *revolving fund*. Aidha, vijana kupitia vikundi vya kijasiriamali au kama mjasiriamali mmoja mmoja wanayo fursa ya kukopa na kurejesha katika Mfuko huo wa JK kwa utaratibu wa kibenki.

Mheshimiwa Spika, fedha za *TASAF* zinatolewa kwa lengo la kupunguza kero za wananchi kuhusu huduma za msingi za jamii. Baada ya wananchi wenyewe kuainisha matatizo yao kwenye jamii, Halmashauri husika hushirikiana na wananchi kuandaa andiko la mradi na kuidhinisha maombi hayo ya wananchi na kuwasilisha *TASAF*. Aidha, *TASAF* hutoa fedha za kusaidia jamii maskini sana *Safety Net Program* kwa utaratibu wa *cash transfers* ambazo hazirejeshwi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe mwenyewe na Waheshimiwa Wabunge wa pande zote mbili kwa michango yao yenye ushauri wenye tija na maelekezo mazuri kwa Serikali Mungu awabariki wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa ruhusa yako, nifikishe shukurani zetu hasa hasa Waheshimiwa wa kwenye Kamati ya Bajeti na Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwa michango yao mizuri ambayo imetusaidia sana Serikali kuweza kujibu hoja hizi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Naibu mwingine, hawa wanaunga mkono hoja. Nakupa dakika 35!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia wote kuwepo hapa leo tukiwa wazima katika shughuli hii muhimu kwa ajili ya Taifa hili. Aidha pia nakushukuru sana kwa weledi wako wa kuendesha Bunge hili na leo ndiyo tunafikia tamati.

Mheshimiwa Spika, Nami pia naunga mkono hoja iliyoletwa mbele yetu na bosu wangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kujibu baadhi ya hoja ama kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja ambazo zimetolewa hapa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwanza kulikuwa kuna hoja ya kuongeza juhudi za ukusanyaji wa maduhuli yaani *Non Tax Revenue* ili angalau ifikie asilimia tatu hadi tano ya pato la Taifa. Naomba kukiri kwamba kuna changamoto katika eneo hili kwa sasa *Non Tax Revenue* inafikia asilimia mbili ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto nyingi zikiwemo uchache wa vitendea kazi, uchache wa watumishi, lakini watumishi wao wenyewe kutokuwa na *ethics* hasa katika kukusanya haya maduhuli, lakini vile vile kumekuwa kuna mifumo dhaifu ya ukusanyaji kwa kutokuwepo hasa hasa matumizi ya teknolojia katika kukusanya pamoja na kukadiria mapato haya. Kwa hiyo, tunakiri kwamba kuna changamoto hizi nyingi.

Mheshimiwa Spika, aidha, taasisi mbalimbali ambazo zinakusanya maduhuli zinatamia mifumo tofauti kwa ajili ya kukusanya maduhuli. Lakini Serikali hatujakaa bure tumekuwa tunafanya tathmini kila robo mwaka na tathmini ambayo sasa hivi inaendelea ambayo inafanyika chini ya ufadhili wa *Public Finance Management Reform Programme*. Kwa mara hii, lengo letu hasa katika ku-*address* changamoto hizi ni

pamoja na ku-*harmonize* hii mifumo ya kukusanya maduhuli. Tunataka ku-*harmonize* taasisi zote ambazo zinakusanya maduhuli ziwe zina mfumo mmoja kwa ajili ya kukusanya hii *Non Tax Revenue* na matarajio yetu ni kwamba tuta-*strengthen* hii *capacity* kwanza kwa ajili ya kukusanya.

Mheshimiwa Spika, sana tunachotaka ni kutumia mifumo ya TEHAMA. Tumeona kuna baadhi ya taasisi tayari zinaanza kutumia; ukienda *Immigration you're not paying hard cash in front*, lakini unalipa kwa benki na vitu kama hivyo. Bandari tayari na wao wameshatangaza kuwa watakuwa wanatumia mifumo kama hii.

Mheshimiwa Spika, lakini hata tukitaka kulipa kwa ajili ya *application* zetu za vyo vikiu sasa hivi tunatumia hii mifumo ya TEHAMA. Hata hivyo vile vile tumesikia hata kulipia tiketi kwa ajili ya kwenda kutazama mpira na vitu kama hivyo tunaanza kutumia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii nadhani itatusaidia, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge Serikali hatujakaa tu, tunafanya hiyo tathmini na huko ndiko ambako tunataka kuelekea. Tunajua kwamba kuna *potential*/kubwa sana kwa ajili ya kukusanya haya mapato ambayo ni *Non Tax Revenue*.

Mheshimiwa Spika, nyingine vile vile ni *institution set up*, tunataka sasa tuwe tuna vitengo maalum kwa ajili ya zile taasisi ambazo zinakuwa zinakusanya maduhuli. Kwa sasa tunaona kwamba Mhasibu huyo huyo ndiye anaweka mahesabu, lakini Mhasibu huyo huyo ndiye anayepokea hiyo pesa na Mhasibu huyo huyo ndiye anayetoa risiti.

Mheshimiwa Spika, hapo peke yake kuna *intimidation*, mtu hawezi kupokea, yeye ndiye akawa anayetoa risiti, yeye ndiye anayefanya mahesabu, kwa hiyo huo ni udhaifu tu wa *institution*. Kwa hiyo, wakati tunakwenda huko kuifanya tathmini ya mwaka huu kwa ajili ya hii *Non Tax revenue* haya ndiyo malengo yetu ambayo tumejiwekea. Waheshimiwa Wabunge nadhani hapa tutakuwa tunakwenda kule ambako sote tunatarajia kufika.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja nyingine ambazo zilikuwa zinasema mamlaka ya Serikali za mitaa hawakusanyi mapato ipasavyo kutokana na utaratibu wa kuwatumia mawakala. Serikali tumeshauriwa, Serikali iwatumie Viongozi wa Kata kukusanya mapato haya.

Mheshimiwa Spika, siwezi kusema kwamba, ushauri huu utafanikiwa lakini siyo ushauri mbaya isipokuwa kwamba kwa sasa Mamlaka za Serikali za Mitaa zenyewe zina uwezo wa kutathmini suala hili na kuamua utaratibu ambao wao wenyewe watautumia katika kukusanya maduhuli *whether* kutumia Viongozi wa Kata ama kutumia Mawakala ama wao wenyewe, sasa wataingia kwa ajili ya kukusanya maduhuli.

Mheshimiwa Spika, awali kilichokuwa kikifanyika ni kwamba, Serikali zenyewe za mitaa ndiyo zilikuwa zinakusanya maduhuli lakini tu kwa sababu ya *capacity*, uwezo duni ukiwemo wa watendaji na vifaa ndiyo wakaamua sasa watumie Mawakala, lakini pale ambapo wanaona kuna changamoto na sasa wao wenyewe wamesha-*strengthen capacity* yao, basi ina mamlaka kamili ya kusema kwamba *now* tunataka kukusanya sisi wenyewe maduhuli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mamlaka zikiona zinafaa wakiona wameshaji *strengthen*, wameshasimama kwa miguu yao, basi *well and good* wanaweza kukusanya maduhuli wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja nyingine kuhusiana na kutozwa ushuru kwa *sunscreen lotion particularly* hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Al-Shaymaa. Kiukweli Sheria za Kodi, yaani Sheria za Forodha Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na ile ya Ongezeko la Thamani hazitozi kodi kwenye vifaa vyote ambavyo vinatumiwa na watu wenye ulemavu mbalimbali hapa nchini. Kwa hiyo, tunaona kwamba, tayari tumesha-*provide exemptions* kwa ajili ya vifaa pamoja na madawa ambayo yanatumiwa na walemavu.

Mheshimiwa Spika, kinachofanyika hapa na tunaomba Waheshimiwa Wabunge tujitahidi sasa kushajiisha kama kuna taasisi ama kuna watu binafsi ambao wanataka kuingiza vifaa hivi, basi watumie utaratibu ambao umewekwa kwanza kwa madawa, lazima waende Wizara ya Afya ikathibitishwe, wakapate ile *certificate and then* Wizara ya Afya wanawasiliana na sisi Wizara ya Fedha na hiyo tunatoa *exemption*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *in general* kwamba hatutozi kodi katika vifaa hivi na hili linakwenda sambamba pamoja na hoja yake ya pili alisema kwamba vifaa kama magari vile vile vinatozwa ushuru.

Mheshimiwa Spika, hivi nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa wote Wabunge kwamba, hatutozi ushuru ili mradi tu *procedures* zimefuatwa na sisi kujiridhisha kwamba hivi ni vifaa ambavyo vinatumiwa na wenzetu wenye ulemavu mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kumetokea tu mambo mambo mengine, inawezekana vitu ambavyo pengine watu wengine wanasema vinatumiwa na walemavu lakini si kweli, lakini hatukuwa na *intention* hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, vifaa ambavyo *specification* zake zipo kabisa vinatumiwa na walemavu, basi huwa hatuvitozi ushuru wa aina yoyote mradi *procedures* zimefuatwa kwa ajili ya kupata uhakika wa matumizi ya vifaa kama hivi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja nyingine kuhusiana na matumizi ya mashine za kielektroniki yaani *EFD's*, hapa kuna changamoto. Waheshimiwa Wabunge kama utakwenda dukani na unahisi kwamba hili duka kutokana na mazingira yaliyopo kwamba ilifaa awe na *EFD* haipo, lakini ukishanunua matumizi yako ilifaa upewe risiti hujaidai, *definitely* hakuna atakayekupa, kwa *nature* yetu, hakuna muuza duka ambaye atakupa risiti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo changamoto kubwa, ipo kwa wanunuaji tukiwemo sisi Waheshimiwa Wabunge, maana tukitoka hapa sote tunakuwa ni watu wa kawaida, tunakwenda dukani tunanunua vitu, kama hujadai risiti, *nature* tu ya mazingira yetu muuza duka hakupi risiti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa kuna changamoto kubwa sana. Kwa hiyo, sisi Serikali kupitia *TRA* kwanza tunaendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kutoa risiti na wajibu wa wafanyabiashara kisheria kutoa risiti. Tunaendelea kutoa elimu na kwa sasa tunatafuta *innovative way* yaani tunatafuta njia nyingine, kwa sababu tulikuwa tunatoa kwa njia ya *radio, television*, magazeti lakini *we are thinking of new ways* za kuweza kutoa elimu hii.

Waheshimiwa Wabunge, tunaomba mtusaidie kwa hili kwa sababu tukija hapa tukasema Serikali haijapeleka kile kilichokusudiwa maana yake tumeshindwa kukusanya maana yake ni nini, wananchi wameshindwa kutusaidia kukusanya. Kwa hiyo tusaidiane katika kufikisha hili muhimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambalo ni jipya na nahisi litasaidia katika hili, Waheshimiwa Wabunge naomba mchukue kalamu na karatasi...

WABUNGE FULANI: Aaah! (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM): Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge watusaidie kutufikishia kwa wananchi namba hizi za bure kabisa, wapige pale ambapo watadai risiti na mwenye duka/ mfanyabiashara atashindwa kumpatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuna namba hizi kwa kutumia *Vodacom* na *TTCL* za bure kabisa 0800-110016 hii kwa wale wenye *Vodacom* pamoja na wanaotumia *TTCL*.

WABUNGE FULANI: Rudia tena.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):

Mheshimiwa Spika, narudia, kwa wale ambao wanatumia *Vodacom* na *TTCL* namba zetu ni 0800-110016; lakini kuna namba nyingine ya *Airtel* ni 0786-800000, hiyo ni kwa wale ambao wanatumia *Airtel*.

SPIKA: Utatupa hizo namba kusudi tuwawekee kwenye simu zao, lakini hii ilikuwa nzuri kwa wananchi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):

Mheshimiwa Spika, pamoja na *Tigo* ni 0713-800333. Namba hizi pia tutaendelea kuzibandika katika sehemu mbalimbali na tutatumia vyombo vya habari kwa ajili ya kuzitangaza. Ni namba za bure, pale ambapo unakwenda dukani mfanyabiashara anakataa kukupa risiti kwa manunuzi ambayo umefanya.

Mheshimiwa Spika, aidha, tunatarajia kuwa na utaratibu mwingine kuwashajiisha wananchi nao ili waweze kutusaidia kuhamasisha hii tabia ya kudai na wafanyabiashara kutoa risiti, ambapo kila mtu ambaye atachukua risiti ya malipo ya bidhaa au huduma ataingizwa moja kwa moja kwenye utaratibu wa kupata zawadi.

Mheshimiwa Spika, kutakuwa na utaratibu wa kutoa zawadi kwa washindi kila wiki au kila mwezi na baadaye kwa mwaka ambapo zawadi mbalimbali ikiwa ni pamoja na gari na fedha tasilimu zitatolewa kwa mshindi. Kwa hiyo, wananchi tushahijike, tuchukue risiti wafanyabiashara watoe risiti, utaratibu huu tunaanza katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha ambao unaanzia tarehe mosi mwezi Julai.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge mtusaidie kuhamasisha wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla katika Majimbo yetu kuhamasisha kutoa na kudai risiti mara wanapouza na kununua bidhaa au kulipia huduma ya aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, niseme pia kwa mwananchi, kama hujadai risiti kwa mtindo tunaokwenda nao,

wafanyabiashara wengi hawatakuwa risiti, ni wachache sana ambao tayari wameshajenga huo utamaduni.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyingine ambayo inasema kwamba, *TRA* wanajiwekea malengo madogo ya makusanyo na kutofikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa mwaka *peculiary* ilikuwa ni mwaka 2012/2013. Naomba kuchukua fursa hii kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba *TRA* kama Taasisi haijiwekei yenyewe malengo.

Mheshimiwa Spika, uratibu wa malengo ya makusanyo, ya mapato unaratibiwa na Wizara ya Fedha, lakini unashirikisha wadau mbalimbali. Kwanza kabisa kuna *Tax Revenue Focusing Model* kuna *Model computerized* ambayo kwa pamoja Serikali imeshirikiana na *East African (Afritag)* ambayo iko chini ya *IMF* kui-*develop model* hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwanza tunatumia hii *model* ambayo ni *computerized* kwa ajili ya ku-*focus revenue* za kila mwaka. Katika *model* hii ndani yake kunakuwa na viashiria vingi vikiwemo vya mwenendo wa uchumi pamoja na taarifa nyingine ikiwemo makusanyo halisi, mabadiliko kwenye mifumo ya kodi, maana yake kila ukifanya mabadiliko, basi mapato nayo yanaathirika.

Mheshimiwa Spika, inawezekana ni *positive* inawezekana *negative*, kwa hiyo, *model* hii nayo inachukua yale mabadiliko. Lakini hivyo vigezo sasa vya kuandaa hivyo viashiria, vinaratibiwa na Wizara ya Fedha, lakini tunashirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa sababu wao ndiyo wanaochukua zile takwimu za kila mara za uchumi na za kijamii.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunashirikiana na Benki Kuu ya Tanzania, kwa sababu wao ndiyo wenye *authority* ya hizi *finances* hapa nchini, pamoja na mwenendo wake mzima, huo nao unaathiri mapato. Pia tunayo Tume ya Mipango, tunashirikiana pamoja kwa ajili ya ku-*develop* hivi viashiria na hatimaye kuwa-*task TRA* kwamba, *this particular year we*

are going to collect this much of revenue, lakini juu ya yote tunashirikiana na Shirika la Fedha la Dunia (*IMF*), wao tunakuwa nao mara kwa mara kupitia *PSI*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mamlaka ya Mapato kama yenyewe haijiwekei malengo isipokuwa tunashirikiana katika kuweka haya malengo. Kwa hiyo, tunapoono kwamba haijafikia, basi labda kutokana na viashiria vile ndiyo vimesababisha wao kutofikia, lakini tukiona wamevuka lengo ni kwa sababu ya hivi viashiria, vikisaidiana pamoja na hiyo *model*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunasisitiza tu kwamba, siyo Mamlaka yenyewe peke yake ndiyo ambayo inajiwekea malengo. Kwa upande huu wa mwaka 2012/2013, naomba kutoa taarifa kwamba, hadi kufikia mwezi Mei, 2013, mapato ya kodi yalifikia shilingi trilioni 6.9, ambapo ni sawa na asilimia 98.4 ya malengo ambayo tumewawekea *TRA* ya kukusanya trilioni 7.057.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunajarajia *by the end of June*, tunaweza kupata asilimia mia moja ya malengo haya, lakini vile vile tunaweza tukavuka hata malengo hayo ambayo tulikuwa tumewawekea.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja nyingine ambayo ilikuwa inaonesha kwamba, Wizara ya Fedha hajatoa gawio la asilimia 4.5 ya Misaada ya Kibajeti (*General Budget Support*), pamoja na Fedha za Kodi ya Mapato (*PAYE*), kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama inavyotakiwa. Hili *particularly* lilikuwa *raised* hapa na Mheshimiwa Hamad Masauni, Mbunge wa Jimbo la Kikwajuni, ambaye pia ni Mbunge wangu kule Zanzibar.

Mheshimiwa Spika pamoja na Waheshimiwa Wabunge, napenda tu kutoa taarifa kwamba, kwa sasa utaratibu uliokuwepo ni kwamba kwa *General Budget Support*, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapata asilimia 4.5 ya fedha ambazo zinapokelewa kutoka kwa Wafadhili.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu si lingine isipokuwa ni utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar. Kama ilivyokuwa kuna MKUKUTA kwa Tanzania Bara, Zanzibar kuna Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini, ni lengo la *GBS* kutekeleza hii mikakati. Kwa hiyo, kwa sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapata asilimia 4.5.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba kwa kipindi cha Julai, 2012 hadi Mei, 2013, yaani mwaka huu wa fedha ambao unamalizika, kiasi cha fedha ambacho kilipelekwa Zanzibar ni shilingi bilioni 22,118,288,400, ambazo ni sawa na asilimia 4.5 ya misaada ya kibajeti na mikopo ya kibajeti vile vile ambayo imepokelewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa pia kuwa kwa mwezi wa Juni, matarajio yetu ni kwamba tutazipeleka fedha zingine ambazo zimebakia, lakini naomba kumjulisha Mheshimiwa Masauni pamoja na Waheshimiwa kwamba, utoaji wa fedha hizi za *General Budget Support* inategemea upatikanaji wake kutoka kwa wafadhili.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa kuna changamoto *sometimes* washirika wa maendeleo, kwa sababu tu ya *procedures* zao, wanaweza wakachukua miezi miwili, mitatu, hizi fedha za *General Budget Support* bado hazijafika. Kwa hiyo, zinapokuja ndipo ambapo *disbursement* inafanyika kuelekea Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tu tujue hii kwamba, changamoto pengine zilizokuwa zimetokea ni kwa sababu tu tumechelewa kupata hizi fedha za *General Budget Support* kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile kulikuwa kuna *issue* ya *PAYE*, ila naomba tu nitoe taarifa kwamba maamuzi ya kulipa *PAYE (Pay As you Earn)* kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya shilingi bilioni 21 kwa mwaka, yaani sawa na shilingi bilioni 1.75 kwa mwezi kuanzia mwaka 2012/2013, yalifanyika baada

ya Bajeti kuidhinishwa na Bunge. Hata hivyo, Serikali ilitafuta bajeti na kuongeza wigo wa bajeti kwa kiasi katika fungu husika ili kutekeleza maamuzi hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, wigo wa Bajeti uliongezwa kwa ajili ya kufanya malipo hayo na malipo hayo yamekwishafanyika hadi mwezi Mei, ambapo jumla ya shilingi bilioni 19.25 zimetolewa na kiasi cha shilingi bilioni 1.75 kwa ajili ya mwezi wa Juni. Hizi taratibu zimeshakamilika na fedha hizi tayari tumeshazitoa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukiangalia kwamba *almost* fedha zile za mwaka mzima, shilingi bilioni 21, mwisho wa mwezi huu wa Juni, zitakuwa zimetolewa. *The good news* ni kwamba, kwa mwaka huu wa 2013/2014, fedha hizi tayari zimo kwenye bajeti na zile changamoto ambazo tumekuwa tuki-*experience*, mwaka huu wa 2012/2013 nadhani kwa kiwango kikubwa tutakuwa tumezi-*address*.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna suala lingine kuhusiana na maduka ya kubadilisha fedha za kigeni (*Bureau De Change*), yanatumika vibaya na mengi hayatoi risiti. Serikali tulitakiwa tufanye uchunguzi na kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha kwamba maduka haya yanalipa kodi kama inavyostahili.

Mheshimiwa Spika pamoja na Waheshimiwa Wabunge, naomba tu kutoa taarifa kwamba, maduka ya kubadilisha fedha za kigeni, yanaanzishwa kusimamiwa na kukaguliwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za kigeni ya mwaka 1992 (*The Foreign Exchange Act of 1992*). Ambayo imeipa Benki Kuu ya Tanzania jukumu la kutoa Leseni na kusimamia uendeshaji wa maduka ya fedha za kigeni kwa kutoa Kanuni na Miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza jukumu hilo, Benki Kuu ya Tanzania imetoa Kanuni za uanzishaji na usimamizi wa maduka ya fedha za kigeni ya mwaka 2008 (*Foreign Exchange Burea De Change, Regulations of 2008*), ili

kuhakikisha kuwa maduka ya fedha za kigeni hayawi vyanzo vya kutorosha fedha za kigeni. Wamiliki wa maduka haya lazima wazingatie masharti yafuatayo kama yalivyoainishwa kwenye Sheria na Kanuni.

Mheshimiwa Spika, kwanza, tunataka maduka ya fedha za kigeni lazima yaanzishwe kama Kampuni, lakini vile vile maduka ya fedha za kigeni lazima yamilikiwe na kuendeshwa na Watanzania na wawe wenye sifa na tabia nzuri. Watanzania ndiyo wawe wamiliki wa maduka hayo, lakini maduka ya fedha za kigeni hayaruhusiwi kufanya biashara yoyote zaidi ya ununuzi na uuzaji wa fedha za kigeni wa papo kwa papo, biashara nyingine yoyote hawaruhusiwi.

Mheshimiwa Spika, lingine, maduka ya fedha za kigeni hayaruhusiwi kuuza kiasi kinachozidi dola za Kimarekani 10,000 kwa siku na mauzo yoyote, zaidi ya dola za Kimarekani 2,000 au kiasi kama hicho, katika aina nyingine ya fedha za kigeni, lazima kuwe na kiambatanishi kinachoonesha sababu ya ununuzi wake, kama vile tiketi ya ndege, ada ya shule, na kadhalika. Kwa hiyo, hizi ndizo taratibu ambazo zipo katika Sheria na Kanuni katika kuanzisha na kuendesha maduka haya ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, aidha ili kusimamia Sheria na Taratibu zilizowekwa, wakaguzi wa mabanki kutoka Benki Kuu, hukagua maduka ya fedha za kigeni, kuangalia utekelezaji wa Sheria na Kanuni za uendeshaji. Adhabu mbalimbali zilitolewa kwa *bureau de change* kuanzia mwaka 2010 mpaka 2013, maana yake hizi ni *data* ambazo tunazo, lakini adhabu zimeendelea kutolewa kwa wale waliokiuka taratibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna ambao walikiuka taratibu, wamepewa onyo kali kutokana na uzito wa ukiukaji wao, wao walikuwa ni 103, lakini kuna ambao wametozwa faini, walikuwa 33, waliofungiwa biashara kwa muda walikuwa watano na kuna wengine 17 tuliwafutia Leseni. Serikali tutakwenda kuziboresha Kanuni na Sheria ili kuhakikisha

kwamba maduka haya hayafanyi biashara nyinginezo aidha kwa kujitajirisha wao, lakini kwa kuikoshesha mapato Serikali.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuzikazia hizi sheria na tutaendelea kuchukua hatua kama inavyostahiki. Waheshimiwa Wabunge changamoto zipo, naomba kwa taratibu hizo basi tusaaidiane katika kuhakikisha kwamba hizi taratibu pamoja na sheria zinafuatwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja nyingine kuhusiana na mashirika yaliyobinafsishwa yaorodheshwe katika Soko la Mitaji na Dhamana (*Dar esa Salaam Stock Exchange*). Hili *particularly* lilikuwa limetolewa na Mheshimiwa Kafulila na Mheshimiwa Mahamoud Mgimwa naye alisisitizia.

Mheshimiwa Spika, ili Shirika liorodheshwe katika Soko la Mitaji na Dhamana (*Dar es Salaam Stock Exchange*), kuna taratibu na vigezo vinavyotakiwa kutimizwa kwa mujibu wa Sheria za Masoko pamoja na Mitaji.

Mheshimiwa Spika, vigezo hivi ni pamoja na kwanza, Shirika liwe na historia nzuri ya utendaji (*Management Performance*), lakini vile vile shirika liwe na historia ya kutengeneza faida kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu, lakini liende sambamba na *a good track record ya management performance*.

Mheshimiwa Spika, vile vile, kwa sababu *intention* ya haya mashirika na makampuni kujiorodhesha katika masoko haya ya hisa, ni pamoja na ku-*increase capital*, kama shirika litakuwa linahitaji *capital*/linakwenda kujiorodhesha pale kwa ajili ya ku-*raise* hiyo *capital*. Kwa hiyo, kigezo kingine ni kwamba, Shirika lifanye maombi ya hiari kusajili ikiwa ni mikakati ya shirika husika kutatua suala la mtaji, hivyo, ni hadi hapo ambapo kampuni husika itakapotimiza vigezo hivyo, ndipo iruhusiwe kujiorodhesha katika Soko la Hisa.

Mheshimiwa Spika, tuna makampuni tayari yapo pale, ikiwa ni pamoja na benki ya *NMB, Tanzania Oxygen Limited*,

TCC, TBL, CRDB, SWISS PORT, Twiga Cement, pamoja na Tanga Cement, lakini kutokana na vigezo hivyo, kuna mashirika ambayo very soon yataingia katika DSE. Mashirika yenyewe ni pamoja na Mtibwa Sugar, Kilombero Sugar, Mbeya Cement, Tanalec, ALAF, NBC, pamoja na Airtel. Kwa hiyo, mashirika hayo tayari yanakamilisha hizi taratibu kwa ajili na wao wenyewe waweze kujiorodhesha katika Dar es Salaam Stock Exchange.

Mheshimiwa Spika, aidha, tunatoa wito kupitia Bunge lako Tukufu kwamba, kuna makampuni mengine ambayo yanakidhi vigezo hivyo ambavyo tumevitaja, basi nayo tuyahamasishe, yahamasike kujiandikisha katika soko la mitaji, ili kwanza wao wenyewe waweze kuongeza mitaji, lakini kupanua ushiriki wa umma katika kumiliki shirika kwa njia ya hisa.

Mheshimiwa Kafulia *again* alikuwa na hoja ya kuwa, lini sasa Serikali itatengeneza Kanuni za kutekeleza Sheria ya Makampuni kuorodheshwa kwenye soko la mitaji na lini makampuni ya simu, madini na utafutaji mafuta na gesi, nayo yenyewe yataorodheshwa kwenye soko la mitaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge, sisi Serikali tumeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha kuwa utekelezaji wa Sheria hii unafanyika kwa ufanisi na mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na kuunda vikosi kazi viwili, kwa sababu *focus* yetu ya kwanza ilikuwa ni kwenye makampuni ya simu, lakini vilevile kwenye makampuni ya migodi.

Mheshimiwa Spika, vikosi kazi hivi tumeviunda kwa lengo la kuweza kuunda au kutengeneza taratibu ama kanuni ambazo zitasaidia utekelezaji wa zile sheria; Sheria ya kwanza ya Mawasiliano ya mwaka 2010, lakini na ile Sheria ya Madini ya mwaka 2010, tutajua kwamba zenyewe zimebadilishwa, kwa hivyo lazima tuzitengenezee Kanuni. Lakini kwa sababu tu hizi ni Sheria mbili tofauti zinahusisha sekta mbili tofauti, tumeunda vikosi kazi viwili tofauti kwa ajili ya kuzitekeleza hizi.

Mheshimiwa Spika, kikosi kazi ambacho kitawajibisha sasa Makampuni ya Simu nayo yanaingia katika soko la mitaji, inaratibiwa na *TCRA*, lakini kikosi kazi kile kingine kinaratibiwa na Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba kutoa taarifa kwamba, katika mwaka wa fedha 2013/2014, tunatarajia kwamba hizi Kanuni zitakuwa zimekamilika na hivyo kuwezesha sasa Watanzania kupata umiliki kwenye kampuni za madini kupitia uuzaji wa hisa za umma, kwa sababu tukishaunda hizo taratibu, basi wananchi wataweza kununua hisa, lakini kwa kupitia *IPO (Initial Public Offer)* na vile vile kuorodheshwa kwenye Soko la Hisa Dar es Saalam.

Mheshimiwa Spika, tunatarajia kwa mwaka huu wa fedha ambao utanza *1st July, any time* tutakamilisha hizi taratibu ambazo kwa sasa tunaendelea na *consultation, draft* tayari ipo tunaendelea na *consultation* na wadau mbalimbali na tunatarajia kwamba katika mwaka 2013/2014, hizi zitaanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, katika Kanuni hivyo hivyo kutakuwa na kipengele cha adhabu kwa yale makampuni ambayo yatashindwa kutimiza matakwa ambayo tumeyaweka katika hizo taratibu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja nyingine kuhusiana na Serikali tufanye jitihada katika kuendeleza utoaji wa vitambulisho vya Taifa kwa kuwapatia *NIDA* fedha ili wakamilishe zoezi hilo. Sisi Serikali tunajua sana umuhimu wa kila mtu kuwa na kitambulisho kwa upande mmoja, usalama zaidi, lakini kwa upande mwingine kwa ajili ya kukusanya mapato stahiki kutoka kwa wale wanaostahili kutoa kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, kwa mwaka 2013/2014, tumetenga shilingi bilioni 151.2 kwa ajili ya bajeti hii ya vitambulisho vya Taifa na tunahakikisha kwa sababu kutokana na umuhimu wa kipekee tutahakikisha kwamba hizi zinapelekwa, lakini *NIDA* nao vile vile wahakikishe kwamba

wanazitumia na tunafikia yale matakwa ambayo tulitaka tufike. Kwa mwaka wa fedha huu ambao tunamalizia, tuliweza kutoa shilingi bilioni 40 ambazo ndizo tulizitenga.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutajihidi kutoa fedha hiyo ambayo imebaki ili *NIDA* nayo iweze kutekeleza wajibu wake kwa ajili ya *impact* kubwa katika uchumi, lakini kwa usalama wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja nyingine kwamba, Serikali iwasilishe Bungeni taarifa za utekelezaji wa miradi mbalimbali kila baada ya miezi mitatu au sita.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa taarifa za utekelezaji wa Bajeti kila robo mwaka, ambazo zinaandaliwa na Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia vitengo vyake vya ufuatiliaji na tathmini (*Monitory Evaluation Departments Units*) na kuwasilisha kwa wakati taarifa hizo kwenye mamlaka husika. Tunawasilisha hizi taarifa katika mamlaka husika kwa ajili ya hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, vile vile, kwa kuzingatia huu mzunguko mpya wa uandaaji wa bajeti ya Serikali, naomba nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa hatua na juhudi zako binafsi kwa ajili ya kuwezesha huu mzunguko wa bajeti kubadilika, basi taarifa hizo za utekelezaji wa bajeti kwa sasa, sisi Serikali tutakuwa tunaziwasilisha pia kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti, kwa ushauri zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii, kuunga mkono hoja na nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana.

Kama nilivyosema, hawa Manaibu Mawaziri wamejibu hivi sasa, lakini mchana Waziri anayehusika ndiye atakayehitimisha hoja yake. Waheshimiwa Wabunge nawaomba tena, tukumbushane, ni wakati wa kupiga kura.

Kwa hiyo, ni vizuri wote watakaokuwa huko waliko, wajitahidi kuja, isipokuwa walio wagonjwa na walioko hospitali na wachache ambao wametoa taarifa kwa sababu ya dharura walizonazo, nimewakubalia, lakini wengi mfike.

Tutawataja kwa majina, kwa hiyo, hao waliowaweka kwenye viti watajua wewe haupo. Kwa hiyo, hiyo nayo siyo nzuri sana kwako, hata ukisema siyo, lakini upo, kwa hiyo, nayo ni vizuri zaidi kuliko kuacha kuja.

Pia napenda kusema, hili swali la kudai risiti kwa manunuzi jamani tulifanye, kwa sababu hiyo ndiyo namna ya kukushanya kodi. (*Makofi*)

Kama kuna tatizo tulilonaldo sisi hapa, ni matumizi makubwa kuliko makusanyo na makusanyo mengi yanapotea kwa kuona uvivu kudai risiti. Usipodai risiti, kweli mwenye duka anafaidika, kwa sababu zile fedha ambazo zilikuwa ziende Serikalini, anakaa nazo mwenyewe. Sasa kama tunadai maendeleo ni lazima tusimame pamoja kudai risiti.

Serikali nayo ihakikishe mashine zinakuwepo, siyo ukamtake mtu aandike risiti kwa mkono, hiyo shughuli hawezi, ziwepo *automatic machines*, hizi mtu anagonga tu, hata asiyejua kusoma atagonga vizuri, atatoa risiti.

Waheshimiwa Wabunge kwa sababu sina matangazo mengine, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 6.20 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Saa 11.00 jioni*)

24 JUNI, 2013

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha asubuhi Waheshimiwa Naibu Mawaziri pamoja na Waziri wa Nchi, washalitoa maelezo kuhusu hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge mlikuwa mmezitoa. Kwa hiyo, kwa sasa namwita Mheshimiwa Mtoa Hoja na muda wake utakuwa dakika 80. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote, awali ya yote, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki kikamilifu Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge la Jamuhuri la Muungano wa Tanzania, ambao unaelekea kufikia tamati wiki hii.

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, pamoja na Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa Mussa Z. Azzan, Mbunge wa Ilala na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mbunge wa Uzini, kwa jinsi mlivyoliongoza Bunge wakati wa majadiliano ya hoja ya Serikali niliyowasilisha tarehe 13 Juni, 2013 kuhusu mapendekezo ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka huu 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Mtemi Andrew M. Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi, kwa kuwasilisha maoni, ushauri na mapendekezo yake ambayo Serikali imeyapokea kwa ajili ya kuboresha maeneo mbalimbali yaliyopendekezwa na Kamati yake.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii vilevile kueleza kwamba, kumekuwa na ushirikiano mzuri wa Kamati na kufanyia kazi ushauri na maelekezo wakati wa utekelezaji wa bajeti hii.

24 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu), Mheshimiwa Steven Masatu Wasira, Mbunge wa Bunda, kwa kutoa maelezo na ufafanuzi wa kina kuhusu hoja mbalimbali zinazohusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2012 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Naibu Mawaziri wa Fedha, Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, kwa kuchapa kazi vizuri na kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote mliopo na wale ambao hawakufanikiwa kufika leo, kwa michango yenu ya kusema na kuandika. Nawashukuru kwa maoni na ushauri wenu, nimeuchukua na kufanyia kazi mapendekezo yenu kwa ajili ya kuiboresha bajeti ya mwaka huu 2013/2014. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, michango tuliyoipokea, ni matokeo ya mabadiliko ya mzunguko wa bajeti ambao umeleta fursa kwa Waheshimiwa Wabunge wengi zaidi kutoa maoni na ushauri wenye lengo la kuboresha utekelezaji wa bajeti hii na mipango mbalimbali ya Serikali kwa mwaka huu 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kujadili mapendekezo ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka huu 2013/2014, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza ni 119 na wale waliochangia kwa njia ya maandishi walikuwa 36. Nachukua nafasi hii kuwashukuru wote waliojaliwa kuchangia bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno yangu ya awali, sasa naomba nijibu baadhi ya hoja zilizoulizwa au kupendekezwa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

24 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na hoja nyingi lakini niseme awali, magwiji mbalimbali na waandishi wa *public finance* wanaeleza kwamba bajeti nzuri ni lazima walau ikidhi vitu vinne. Kwanza, kile kinachoitwa *public burden test* yaani nani ananufaika na sera zilizoenezwa ndani ya bajeti. Pili, nani analipa kodi hizo zinazofanya bajeti hiyo iwepo na tatu namna matumizi ya Serikali yatakavyochangia kuleta msukumo kwenye maisha ya wananchi kiuchumi. Swali hili, bajeti hii imejibu vizuri kwa kuelekeza kodi tutapata wapi na tutalipaje na kwamba kodi hiyo tutawekeza katika maeneo gani. Swali hili la msingi bajeti hii imekidhi na Waheshimiwa Wabunge wameona.

Mheshimiwa Spika, lazima bajeti ikidhi hoja ya pili, kwamba, kwa kiwango gani kuna upunguzaji wa umaskini ambao umedhamiriwa ndani ya bajeti, yaani *poverty reduction test*. Kwa kiwango gani maana yake, sera zilizomo ndani ya bajeti na utekelezaji unaolengwa kutekelezwa, zitachangia kupunguza umaskini wa wananchi wa nchi hiyo. Tumelekeza namna bajeti hii itakavyoelekeza fedha kwenye maeneo ya maji, umeme, barabara vijijini, kilimo na kwenye maeneo ya kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata fursa ya kushiriki katika shughuli za maendeleo. Bajeti hii imejibu hoja hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bajeti lazima ijibu swali lingine la tatu la msingi kwamba, je, bajeti hii kwa kiwango gani inatambua umuhimu wa kusaidia makundi ya jinsia hasa yale ambayo kiasili yalikuwa hayana nafasi ya kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kundi letu ni akina mama. Bajeti hii imejibu, kwa kutenga mafungu yanayosaidia kuhakikisha kwamba akina mama na wenyewe wanapata fungu na kuongezewa fungu katika benki yao. Vilevile vijana wetu nao wametengewa fungu kwa kujibu swali hili la msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la mwisho la nne, bajeti lazima ijibu *responsiveness test*, kwa maana bajeti inatambua vipaumbele muhimu ambavyo nchi lazima iwekeze ili vile vipaumbele viweze kuongeza uzalishaji wa uchumi nchini. Bajeti yetu imejibu kwa kiuwekezaji wa uhakika kabisa katika

maeneo ya msingi ya vipaumbele ili vichochoe katika kuboresha uchumi wa nchi yetu. Tumewekeza kwa nguvu katika barabara ambapo tumeweka shilingi trilioni 1.2, tumewekeza kwa kiwango kikubwa katika umeme, usafirishaji, maji na maeneo mengine ili yalete kichochoe kwa uzalishaji hapa nchini. Kwa hiyo, baada ya hayo ya msingi kabisa, tunasema bajeti yetu imejibu hoja za bajeti inavyotakiwa kuwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, sasa nianze kujibu maswali ya msingi. Nichukue nafasi hii Waheshimiwa Wabunge kusema kwamba majibu ya maswali yenu yote, tumeyaandika ili muweze kupata *booklet* itakayosaidia kujibu yale ambayo pengine hatutayaeleza hapa kwa kukosa muda, lakini yale ya msingi yanajibiwa leo.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kumekuwa na hoja nzuri kutoka kwa Wabunge wengi wakieleza kwamba Serikali haikusanyi kodi ya kutosha kutoka kwenye makampuni ya madini. Waheshimiwa Wabunge waliouliza swali hili nikitaka kutaja wachache ni Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Sara Msafiri, Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Subira Mgalu. Hawa wameuliza kwa nguvu wakitaka kujua kwa nini Serikali inelekea kwamba haikusanyi vya kutosha kutoka katika makampuni ya madini.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, jibu langu ni kwanza, makampuni makubwa ya madini ambayo tunayo ni makampuni saba nazo ni *Bulyanghulu Gold Mine Ltd, Geita Gold Mine, North Mara Mine, Pangea Minerals Ltd, Resolute Tanzania Ltd, Tanzanite One Mining Ltd* na *Williamson Diamonds*. Haya ni makampuni ya madini na ni makampuni makubwa nchini na kodi ambazo Serikali imekuwa ikichukua kutoka kwenye makampuni haya ni *VAT, Corporate Tax, PAYE, SDL, Withholding Tax* pamoja na *Stamp Duty*.

Mheshimiwa Spika, sasa nitakupeni picha walau kwa miaka mitano Serikali imekusanya kiwango gani kwa ujumla kutoka kwenye makampuni haya. Mwaka 2007/2008,

24 JUNI, 2013

tulikusanya shilingi bilioni 69.5 kutokana na makampuni haya, mwaka 2008/2009, tulikusanya shilingi bilioni 66.6, mwaka 2009/2010, tulikusanya shilingi bilioni 85.5 na mwaka 2010/2011, tulikusanya shilingi bilioni 119 lakini mwaka jana 2011/2012, tulikusanya shilingi bilioni 274.8 na mwaka huu 2012/2013 hesabu hizi mpaka mwezi Machi, tumekwisha kusanya shilingi bilioni 251.8. Jumla katika kipindi hiki cha miaka mitano kutokana na makampuni haya, tumekusanya shilingi bilioni 867.38. Hii ni asilimia 2.6 ya makusanyo ya kodi. Kwa jibu hili, ni dhahiri kabisa si kwamba hatukusanyi lakini tuna takwimu za kuthibitisha tumekuwa tukikusanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili la muhimu, Waheshimiwa Wabunge walipendekeza na wengine wameuliza ni kwa kiwango gani tumeitendea kazi hoja ya tozo ya *SDL* kupungua kutoka asilimia sita (6%) iende chini. Serikali tulilichukua elekezo hilo na tumelifanyia kazi na tumepunguza kutoka asilimia sita (5%) kwenda asilimia tano (5%). Pia tumeongeza wigo wa walipaji wa tozo hili ili kuleta nafuu na nafasi ya kukusanya fedha nyingi kutokana na tozo hii na vilevile kusaidia kuongeza mapato. Kwa hali hiyo, asilimia mbili (2%) iliyokuwa inakwenda *VETA* pamoja na mwendelezo wa Mkutano, tutaendelea kuipeleka huko. Ni tegemeo letu kwa kuongeza *base* ya walipa kodi wa kodi hii, makusanyo yataongezeka pamoja na kwamba tumepunguza kwa asilimia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine lililoulizwa ni kwamba, kwa nini Serikali inaacha kutoza kodi kampuni za utafutaji wa mafuta na gesi. Jibu hapa ni kwamba, kiutaratibu, kampuni yoyote ikiwa katika hatua ya utafiti, au ya utafutaji, haitozwi kodi. Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2006, inasema kwamba, kodi ya mapato hutozwa kwenye faida na biashara yake au kitega uchumi chake. Kwa sababu hiyo, mtaona kwamba kampuni zile ambazo ziko katika mchakato wa utafutaji na utafiti, hazijaingizwa katika mchakato wa kulipa kodi kwa sababu ya hoja hii ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine kwa uzito wake iliuliza Serikali ilifanya juhudi gani kushusha mfumuko wa bei

kutoka asilimia 19.8, iliokuwepo Desemba 2011 hadi asilimia 8.3 mwezi Mei. Hoja hii iliekea kutia shaka kama mteremko huu au punguzo hili inaonekana umekuwa ukipungua kwa asilimia kubwa mno. Naomba nitoe mfano wa Kenya na Uganda. Mwaka 2012 Kenya, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 13.06 lakini kwa mwezi huu uliopita wenzetu mfumuko wa bei ni asilimia 4.14. Wakati huohuo Uganda, mwezi Aprili mwaka jana, mfumuko wao wa bei ulikuwa asilimia 20.3 lakini kwa sasa mwezi huu iliopita kule Uganda mfumuko wa bei ni asilimia 3.4.

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei kwa upande wetu wa Tanzania, umekuwa unachochea sana na bei za vyakula. Ukiangalia katika lile kapu la bei za bidhaa na huduma ambazo ndizo zinazochangia katika kipimo cha mfumuko wa bei, chakula kinachangia kwa asilimia 47.8. Kwa hali hiyo, mikakati yote ambayo inalenga kupunguza mfumuko wa bei ni lazima kwanza kwa uzito huu ielekee kutatua tatizo la chakula.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012, kulikuwa na uhaba wa chakula nchi jirani hivyo chakula kilikuwa kikivushwa huko kwa njia zisizo rasmi na kwa sababu hiyo, hali ile ilichangia sana kuleta upungufu wa chakula hapa nchini. Kwa hiyo, hiyo nayo ilikuwa ni sababu mojawapo iliyofanya mfumuko wa bei mwaka 2010 uwe mkubwa. Hata hivyo, Serikali ilichukua hatua kubwa kwa ajili ya kudhibiti mfumuko ule wa bei ya vyakula. Vilevile mfumuko wa bei ulichangiwa na uagizaji wa mafuta kutoka nje ya nchi ambayo kwa wakati ule bei yake ilikuwa kubwa. Niseme tu hapa kwamba kwa sababu mfumuko wa bei ni lazima ushughulikiwe pande mbili, kwa maana ya *Monitory and Fiscal Policy*, kwa hiyo, wenzetu wa Benki Kuu vilevile walifanya juhudi kubwa kwa upande wa Sera za Fedha kwa kuleta udhibiti wa kutosha na kuhakikisha kwamba mfumuko wa bei unakuwa *contained*.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa linahoji au linapendekeza kwamba bei ya mafuta, kwa maana ya petroli, dizeli na mafuta ya taa ipungue. Kwa undani, suala hili tumelishughulikia vizuri na katika *percentages* ambazo

24 JUNI, 2013

tumezishughulikia za upungufu ambao Serikali inapendekeza, tutauleta kwenye *Finance Bill*. Napenda niwahakikishie kwamba Serikali tumeshalishughulikia vizuri sana suala hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niseme tu, kinachochangia katika matatizo ya bei na hali halisi, ni kwamba, mwaka 2011/2012, Serikali ilifanya marekebisho ya viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya dizeli, petroli na mafuta ya taa. Haya mabadiliko ya kurekebisha zile bei ilikuwa ni kwa ajili ya kulenga vile vitu vitatu. La kwanza, kuondoa uchakachujaji wa mafuta, ambapo wachakachujaji wanachanganya aidha mafuta ya taa na mafuta ya dizeli. Kwa hivyo, urekebishaji wa bei zile ulilenga kulikabili tatizo hili na kwa kusema kweli Waheshimiwa Wabunge, tulifanikiwa sana mpaka tukauwa uchakachujaji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ilikuwa ni kuimarisha uhusiano wetu na nchi jirani, hasa Rwanda na nchini nyingine ambazo walianza kuilaumu Tanzania kwamba mafuta yanayopitia bandari ya Dar es Salaam yalikuwa yanachakachuliwa na hivyo kuharibu biashara ya mafuta nchini mwao. Kwa hiyo, hii ilituchochea kuchukua hatua hiyo na kweli tukatatua tatizo hilo. Sababu ya tatu, ni ile ya mwisho ya Serikali kupata nyongeza ya mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo na mwaka huu tumelitizama kulingana na maelezo na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge, tumefanya *adjustment* fulani katika bei zile tukizingatia umuhimu wa kutoacha mafuta yale yachakachuliwe. Kama nilivyosema, tozo au kodi hizi, tutazieleza kiundani tutakapowasilisha *Finance Bill* ndani ya siku mbili zijazo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nyingine ililenga kuishauri Serikali kwamba izingatie mapendekezo ya Ripoti ya Kamati Maalum ya Bunge, kuhusu vyanzo vingine vya kodi ambavyo vimependekezwa na Kamati ya Mheshimiwa Spika. Waheshimiwa Wabunge wengi mlinihoji kwamba ni kwa kiwango gani Serikali ilichukua mapendekezo ya Kamati

Maalum ya Spika na kitu gani kilipatikana huko. Serikali ilifanyia kazi mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge na nichukue nafasi hii, kwa dhati kabisa, kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ile, Mtemi Andrew Chenge na Kamati yake, kwa mapendekezo ambayo mengi yalikuwa na nguvu ya hoja na kuisaidia Serikali ambayo imeyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii, kuyatamka maeneo ambayo ni dhahiri kabisa Serikali tumeyachukua. La kwanza, kupunguza tozo ya *SDL*, kama nilivyoeleza, hili tulilichukua na tumelifanyia kazi. Pili, kutoza kodi kwenye ngano inayoingizwa nchini na sisi hili tulilichukua, ni mapendekezo mazuri. Tatu, kufanyia mabadiliko ya mfumo wa kodi wa sekta za simu za mkononi. Hili tumelifanyia kazi na *Finance Bill* itakapokuja kesho au kesho kutwa, wote mtapata nafasi kuona namna tulivyofanyia kazi mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge. Nichukue nafasi hii, kwa dhati kabisa kuishukuru Kamati hii, kwa sababu katika kile kilichopendekezwa Serikali moja kwa moja tumeingiza katika Mfuko wa Mapato ya Serikali shilingi bilioni 414.6. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya nyingine, Serikali ipunguze matumizi. Nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kumshukuru Mheshimiwa Luhaga Mpina, nafikiri yupo hapa. Mheshimiwa Luhaga Mpina amekuwa akiizungumzia hoja hii kwa nguvu kabisa na Serikali sikivu tunasikia, kwamba ni wakati sasa tuangalie kiundani kabisa ni kwa namna gani tunaweza tukapunguza matumizi ya Serikali yasiyo na tija. Nachukua nafasi hii kwa dhati kabisa kumshukuru Mheshimiwa Luhaga Mpina, Serikali tumelifanyia kazi suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine, Mheshimiwa Luhaga Mpina, amekuwa akizungumzia vitu vitatu. Cha kwanza, kurekebisha au kubadili Sheria ya *Procurement* ili isiwe uchochoro wa wezi kupitia. Kama alivyosema Mheshimiwa Stephen Wasira asubuhi ya leo, Serikali tumechukua maamuzi sasa kwa kupitia ushauri wenu kubadilisha Sheria hii au kuifanyia kazi upya ili upungufu

24 JUNI, 2013

unaotokana na manunuzi, ambapo watu hupitia kwenye Sheria hii yaweze kutatuliwa.

Mheshimiwa Spika, pili, tumechukua hatua ya kutazama namna gani tunaweza tukatumia utaratibu wa *bulk procurement*, kununua hasahasa magari ya Serikali na kupunguza gharama za ununuzi wa magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tumetazama maeneo mengine ya *OC* ambayo Waheshimiwa Wabunge na hasahasa Mheshimiwa Luhaga Mpina amekuwa akilizungumza sana hili na sisi tumelifanyia kazi pamoja na ushauri wa Wabunge wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, ni suala la misamaha ya kodi ambayo mmependekeza tuitazame upya na sisi kama nilivyosema wiki iliyopita wakati nawasilisha bajeti...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba mnyamaze.

WAZIRI WA FEDHA: Tumetengeneza utaratibu, sasa tunapitia sheria hii kutazama na kupunguza maeneo yote ya sheria ambayo yanatoa msamaha wa kodi katika maeneo yasiyo na tija ili tubakie tu na maeneo yale yanayoleta changamoto ya uzalishaji wa uchumi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Waheshimiwa Wabunge mmekuwa mkisisitiza tuwekeze katika miradi ya maendeleo. Pamoja na kwamba mwaka huu tumefaulu kuongeza kidogo lakini ni nia ya Serikali huko tunakoendelea, tutaongeza uzito kwa kuwekeza mafungu katika *development expenditure*.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine na ambayo imekuwa ni lalamiko kubwa kwa Waheshimiwa Wabunge, kwamba fedha ambazo zinatengwa na Serikali, kwa kiwango kikubwa zimekuwa hazifiki kwa walengwa yaani kwenye miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali tumelitazama *positively*, kwamba hoja ya Waheshimiwa Wabunge ni lazima tuifanyie kazi ili tuweze tukaona maeneo ambayo *deliberately* yanatukwamisha hela ile isifike kwa wakati tuyatatue. Bado tunafanya uchambuzi wa namna ya kuboresha mfumo ambao utatusaidia wakati tunagawa pesa ziweze kufika kwa haraka zaidi kuliko ilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, kuna eneo ambalo tunatakiwa tusaidiane, nalo ni eneo la namna hela inavyofika kule kwenye Halmashari za Miji na Wilaya na ikakaa pale bila kutumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunayo ripoti, tumefanya tathmini, *as of June 5, 2013*, fedha ambazo tulikuwa tumepeleka kwa ajili ya miradi ya barabara yaani *Road Toll Fund*, bajeti ni shilingi bilioni 108.2, ndiyo bajeti kwa ajili ya kupeleka kwenye Halmashauri na Wilaya kwa mwaka huu. Katika fedha hiyo, tulikuwa tumeshapeleka shilingi bilioni 84.07 sawa na asilimia 77% ya fedha hiyo. Hapa tusaidiane sasa, ikiwa hela hiyo, shilingi bilioni 84 imeshapelekwa kwenye Halmashauri, ambayo ni sawa na 77%, sasa tatazameni takwimu. Wilaya 33 katika Wilaya 151 zilikuwa zimetumia asilimia 0.0 mpaka asilimia 11.56 ya fedha iliyopokelewa. Pili, Wilaya 11 katika hizo 33, zilikuwa hazijatumia hata senti tano katika zile hela ambazo wamepelekewa. Inawezekana kukawa na sababu nzuri au sababu ambayo haikuepukika, lakini tulitarajia Waheshimiwa Wabunge, tatizo la namna hii na ninyi mngekuwa mnafahamu kwa sababu fedha hii ni ya *Road Fund*, inakwenda kwenye Wilaya zenu. Sasa Wilaya 11 hazikutumia hata senti moja.

Mheshimiwa Spika, tatu, Wilaya 45, zilitumia kati ya asilimia 12 na 32 ya hela waliyopelekewa. Narudia, Wilaya 45 zimetua *only between 12% and 32%* ya hela ile ambayo wamepelekewa. Nne, Wilaya 45 zingine zimetumia kati ya 32% na 47% ya hela waliyopokea wakati iliyobaki haikutumika. Wilaya 28 ndizo zilizotumia walau kwa kiwango kikubwa, zilitumia kati ya 48% na 90% ya hela ile iliyopokelewa. Upande wa Serikali tunaweza kama nilivyosema tukawa na matatizo

ya hapa na pale katika mifumo au ulegevu na sisi ni lazima tujirekebishe lakini lile linalotokea kwa Halmashauri zenyewe na Wilaya, Serikali tunasema na wenzetu wajirekebishe. Si vizuri kukaa na fedha karibu mwaka mzima lakini haitumiki akalaumiwa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la deni la Taifa. Waheshimiwa Wabunge wamesema, tena kwa kurudia kwamba wangependa kujua deni la Taifa likoje. Swali hili liliuliza, je, deni la Taifa, madeni ya *ATCL*, *PSPF* na *NSSF*, nayo yamo ndani? Hili ndilo lilikuwa swali la kwanza katika deni la Taifa. Jibu langu katika hilo, ni kwamba hadi mwishoni mwa mwezi Machi, 2013, deni la Taifa likijumlisha deni la umma na sekta binafsi, ilikuwa shilingi bilioni 23,673.53. Hata hivyo, kiasi hicho cha deni hakikujumuisha madeni yaliyotokana na mikopo iliyokopwa na Taasisi za Serikali chini ya udhamini wa Serikali. Madeni hayo ni pamoja madeni ya *PSPF*, *ATCL* na *NSSF*. Madeni yatokanayo na mikopo iliyodhaminiwa na Serikali hujumuishwa kwenye deni la Taifa baada ya kuwepo kwa uhakika kwamba Taasisi iliyodhaminiwa na Serikali imeshindwa kulipa deni hilo na kuhakikiwa na Serikali. Tunapothibitisha katika hatua ile ndipo tunajumlisha, kwa sababu Serikali ilikuwa mdhamini tu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ilikuwa hoja kwamba, je, Serikali inaweza ikawasilisha taarifa ya mchanganuo wa deni la Taifa lililofikia shilingi trilioni 21, hii ilikuwa kabla ya mwezi Machi. Nimetayarisha jibu hili kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge na nimeweka kimaandishi kwa yule anayependa kuwa na *details* lakini nitasoma hapa kiujumla. Nikianza na *External Debt Portfolio*, Deni la Nje, *International Organization*, Mashirika ya Kimataifa, ni shilingi trilioni 9.6. *Bilateral Creditors* yaani *Paris Club Members*, shilingi trilioni 1.289. Vilevile *Non-Paris Club Members*, ni *Bilateral Creditors*, madeni yetu yalikuwa shilingi trilioni 2.577. Tuna madeni yanaitwa *Export Import Credit Source*, haya ni shilingi bilioni 711.9. Halafu tuna kundi la madeni ya kibiashara na haya ni madeni ambayo tumekopa kwa ajili ya miradi yote ya maendeleo, jumla ni shilingi trilioni 2.35 na ukijumlisha hayo yote, deni la nje linakuja shilingi trilioni 16.553.

Mheshimiwa Spika, lakini tuna madeni mengine, *short term domestic instruments* yaani hati fungani za kutambua madeni tuliyonayo. Ya kwanza, ni *Treasury Bills (TB)*, ni shilingi trilioni 1.012. Hati fungani za muda mrefu yaani *long term domestic instrument*, hii ni shilingi bilioni 257.081. *Bonds* ambazo tume-raise, ni shilingi bilioni 4.003. Mikopo mingine ya ndani, ipo kidogo kama shilingi bilioni 9.6. Deni la ndani kwa ujumla ni shilingi trilioni 5.283. Kwa hiyo, hii ndiyo *breakdown* ya madeni kwa tarehe ile kama Waheshimiwa walivyotaka kupata picha ya deni letu.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kwamba kodi ya mapato kwa wafanyakazi ipunguzwe hadi 10% badala ya 13% inayopendekezwa na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala hili lilizungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, nikitoa tu mfano liliulizwa na Mheshimiwa Bwanausi, Mheshimiwa Kigola, Mheshimiwa Hilda Ngoye, Mheshimiwa Rukia na Mheshimiwa Kisanji. Hawa waliuliza swali hili kwa msisitizo, kwa mawazo yao wanaona tumepunguza kidogo mno.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuendelea kumpunguzia mzigo mwajiriwa. Nitoe tu takwimu kwamba mwaka 2007/2008, kiwango cha chini cha kodi kilikuwa ni 18.5%. Serikali imekuwa ikiendelea kupunguza kidogokidogo ili kumpunguzia makali mfanyakazi na kumpa *more purchasing power* mpaka tulipofikia mwaka huu kuwa 13%. Serikali mbele ya safari kadri hali inavyoendelea kuboreka, itaendelea kuangalia namna ya kumpunguzia kodi mwajiriwa wa kipato cha chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni pendekezo la mabadiliko ya kufuta kodi ya leseni ya mwaka kwa vyombo vya moto vyenye ujazo wa injini usiozidi *CC500*. Swali hili au hoja hii imeletwa na Wabunge wengi sana kwamba Serikali itazame upya kiwango kile cha msamaha wa *road licence* kwa ajili ya vijana wetu wa bodaboda kwamba bodaboda zile siyo zao, ni za wenyewe. Serikali imekuwa ikilifanyia kazi suala hili kupata ukweli wa pembeni, wa mbadala. (*Makofi*)

24 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, niseme kifupi waliozungumza kwa nguvu sana juu ya suala hili ni Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa Yahya, Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa Chacha Nyangwine, Mheshimiwa Moza Abeid, Mheshimiwa Aliko Kibona na wengineo. Kwa ujumla, Waheshimiwa Wabunge wengi hawaridhiki na Serikali kusamehe *road licence* kwa bodaboda kwa sababu hailengi wale vijana. Serikali tumelifanyia kazi suala hilo, tutalionyesha kwenye *Finance Bill* ya keshokutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yalikuwa sehemu ya maswali yale makubwa ambayo Waheshimiwa Wabunge walitaka yapate majibu lakini maswali mengine tumeyaandika yote kwa sababu ya *interest of time* ili tuweze tukawaletoa kitu kilichoandikwa na kukidhi hoja ya maswali yenu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii, kuwashukuru kwa namna ya pekee Waheshimiwa Wabunge wote kwa jinsi walivyotoa maoni na ushauri wao na mimi kwa niaba ya Serikali, naomba kusema kwamba tumepokea ushauri wenu kwa moyo mkunjufu na kuutumia na tutaendelea kuutumia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba tutakapokwenda kwenye hatua ya pili, mpige kura ya ndiyo kwenye bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, bajeti hii imesheheni uwekezaji katika maeneo yanayogusa wananchi walio maskini. Tunataka sasa hivi kuhakikisha kwamba wenzetu walio vijijini, wanasaidiwa kwa kiwango kwa kutosha. Wote ni mashahidi, tumeongeza shilingi bilioni 184.5 kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wetu wanapata maji, tumeongeza shilingi bilioni 30 kuhakikisha kwamba miundombinu ya usafirishaji inakuwepo, tumeongeza shilingi bilioni 30 nyingine kuhakikisha kwamba viwanda vya EPZ tunaanza kuwekeza, tumewekeza katika maeneo ya vijana na ya akina mama, katika maeneo ya mifugo tumeongeza bajeti kwa shilingi bilioni 20 na tumeongeza bajeti kwa ajili ya kuboresha Mfuko wa Mbolea kwa jumla ya shilingi bilioni 21.5. Ukitazama yote hayo ni kwamba tumeelekeza fedha hizi kwa wananchi

wanyonge ili kuwapa nafasi na wenyewe waweze kuwa sehemu ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini isitoshe, tumeongeza shilingi bilioni 186 kwenye *REA* ili bajeti yetu iweze kujipambanua pamoja na maskini, wananchi wetu wapate umeme. Bajeti yetu ya awali ilionyesha kwamba *allocation* yetu ilikuwa ya shilingi bilioni 153. Kwa maombi ya Waheshimiwa Wabunge na Serikali kwa usikivu wake na kwa kutambua umuhimu wa kuwa na umeme katika vijiji vyetu, tukaongeza shilingi bilioni 186 ili kukidhi mahitaji ya umeme vijijini. Ili hili litekelezeke, kwa dhati kabisa, naomba mliunge mkono ili tuanze kulitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Hoja hii imeungwa mkono, sasa hatua inayofuata, ina utaratibu wa Kikanuni na Kikatiba. Kufuatana na Katiba, Ibara ya 94 inasema kwamba, akidi kwa kila kikao cha Bunge ni nusu ya Wabunge wote. Kabla ya kuingia katika zoezi la kupiga kura, tunatumia Kanuni ya 107(1) na (2) ambayo inasema kwamba, mjadala kuhusu hotuba ya bajeti ya Serikali utakapomalizika, Spika atalihoji Bunge litoe uamuzi wake wa kupitisha au kutopitisha Bajeti ya Serikali ili kukidhi matakwa ya Ibara ya 90(2)(b) ya Katiba.

Hii niliisoma juzi na kusema kwamba nafasi moja ambayo Rais anaweza kuvunja Bunge, ni pale ambapo bajeti ya Serikali imekataliwa.

Hivyohivyo Kanuni ya 107(2) inasema, uamuzi wa Bunge wa kupitisha au kutopitisha bajeti ya Serikali, utafanywa kwa kupiga kura ya wazi kwa kuita jina la Mbunge mmojammoja. Kwa hiyo, hapa tulipofikia, tutapiga kengele ili Wabunge waliopo nje, waingie ndani. Halafu pia tuna *register* ya majina yenu yote, tutawaita kwa majina mmojammoja na tunashawishi yule anayeitwa asimame...

24 JUNI, 2013

MBUNGE FULANI: *Yes!*

SPIKA: Maana Kanuni zetu zinasema utakapoitwa na Spika ndiyo unasimama.

MBUNGE FULANI: Sawasawa!

SPIKA: Kwa hiyo, usimame tukuone wewe unayesema 'Hapana' au 'Ndiyo' ni nani. (*Makofi/Kicheko*)

Maana ukimwita Mbunge mmoja utasikia 'Ndiyo', ukimwita mwingine utasikia 'Ndiyo', ukimwita mwingine tena utasikia 'Ndiyo' unafikiri ni Mbunge mwingine kaitikia kumbe ni huyohuyo mmoja kaitikia mara tatu. Kwa hiyo, mtasimama na kuitika kama inavyostahili. Kwa hiyo, naomba sasa tutulie ili kengele ipigwe na watu wote waweze kuingia ndani halafu tutaona itakavyokua. Naomba kengele ipigwe.

(Hapa Kengele Ilipigwa ili Waheshimiwa Wabunge walilopo nje ya Ukumbi wa Bunge waweze kuingia Ndani kwa Zoezi la Kupiga Kura)

SPIKA: Nadhani wenzetu waliokuwa nje ya ukumbi huu wameingia, sasa tunaweza kuanza kupiga kura, Katibu!

1. Mhe. Mizengo Kayanza Peter PindaNdiyo
2. Mhe. Samuel John Sitta.....Ndiyo
3. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha.....Hakuwepo
4. Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu.....Ndiyo
5. Mhe. Dkt. John P.J. Magufuli.....Ndiyo
6. Mhe. Prof. Mark James Mwandosya.....Ndiyo
7. Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi.....Ndiyo
8. Mhe. Stephen Masatu Wasira.....Ndiyo
9. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe.....Ndiyo
- 10.Mhe. Shukuru Jumanne Kawambwa.....Ndiyo
- 11.Mhe. Hawa Abdulrahman GhasiaNdiyo
- 12.Mhe. Sophia Mattayo Simba.....Ndiyo
- 13.Mhe. Bernard Kamillius Membe.....Hakuwepo

14.Mhe. Mathias Meinrad Chikawe	Ndiyo
15.Mhe. George Huruma Mkuchika.....	Hakuwepo
16.Mhe. Celina Ompeshi Kombani.....	Hakuwepo
17.Mhe. William Vangimembe Lukuvi	Ndiyo
18.Mhe. Dkt. Emmanuel John Nchimbi.....	Ndiyo
19.Mhe. Dkt. David Mathayo David.....	Ndiyo
20.Mhe. Gaudentia Mugosi Kabaka.....	Ndiyo
21.Mhe. Samia Hassan Suluhu	Ndiyo
22.Mhe. Dkt. Terezya Pius Luoga Huvisa.....	Ndiyo
23.Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa.....	Ndiyo
24.Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibajjuka.....	Ndiyo
25.Mhe. Eng. Christopher Kajoro Chiza	Hakuwepo
26.Mhe. Balozi Khamis Juma Suedi Kagasheki.....	Ndiyo
27.Mhe. Dkt. Harrison George Mwakyembe	Ndiyo
28.Mhe. Dkt. Fenella Ephraim Mukangara.....	Ndiyo
29.Mhe. Dkt. Abdallah Omari Kigoda.....	Ndiyo
30.Mhe. Dkt. William Augustao Mgimwa.....	Ndiyo
31.Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo.....	Ndiyo
32.Mhe. Jaji Frederick Mwita Werema.....	Ndiyo
33.Mhe. Job Yustino Ndugai	Ndiyo
34.Mhe. Dkt. Milton Makongoro Mahanga.....	Ndiyo
35.Mhe. Adam Kighoma Malima.....	Ndiyo
36.Mhe. Aggrey Deaisile Joshua Mwanri.....	Ndiyo
37.Mhe. Lazaro Samuel Nyalandu.....	Ndiyo
38.Mhe. Benedict Ngalama Ole-Nangoro.....	Ndiyo
39.Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa	Ndiyo
40.Mhe. Gregory George Teu	Ndiyo
41.Mhe. Pereira Ame Silima.....	Ndiyo
42.Mhe. Mahadhi Juma Maalim.....	Ndiyo
43.Mhe. Charles Muhangwa Kitwanga.....	Ndiyo
44.Mhe. Goodluck Joseph Ole-Medeye.....	Ndiyo
45.Mhe. Philipo Augustino Mulugo	Hakuwepo
46.Mhe. Ummy Ally Mwalimu.....	Ndiyo
47.Mhe. Dkt. Abdulla Juma Saadalla	Ndiyo
48.Mhe. Eng. Gerson Hosea Lwenge	Ndiyo
49.Mhe. Dkt. Seif Seleman Rashidi	Ndiyo
50.Mhe. Dkt. Binilith Satano Mahenge	Ndiyo
51.Mhe. George Boniface Simbachawene.....	Ndiyo
52.Mhe. Stephen Julius Masele	Ndiyo
53.Mhe. January Yusuf Makamba	Ndiyo

54.Mhe. Dkt. Charles John Tizeba	Ndiyo
55.Mhe. Amos Gabriel Makalla	Ndiyo
56.Mhe. Angellah Jasmine Kairuki	Ndiyo
57.Mhe. Janet Zebadayo Mbene	Ndiyo
58.Mhe. Saada Mkuya Salum	Ndiyo
59.Mhe. Brig. Gen. Hassan Athuman Ngwilizi	Hakuwepo
60.Mhe. Andrew John Chenge.....	Ndiyo
61.Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa	Ndiyo
62.Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa.....	Ndiyo
63.Mhe. Pindi Hazara Chana.....	Ndiyo
64.Mhe. Dkt. Hamis Andrea Kigwangalla.....	Ndiyo
65.Mhe. Lediana Mafuru Mng'ong'o	Ndiyo
66.Mhe. Margaret Simwanza Sitta.....	Ndiyo
67.Mhe. Jenista Joakim Mhagama	Ndiyo
68.Mhe. Peter Joseph Serukamba.....	Ndiyo
69.Mhe. James Daudi Lembeli.....	Ndiyo
70.Mhe. Prof.Peter Mahamudu Msolla.....	Ndiyo
71. Mhe. Anna Margareth Abdallah	Hakuwepo
72.Mhe. Edward Ngoyai Lowassa.....	Ndiyo
73.Mhe. Kabwe Zuberi Zitto	Hakuwepo
74.Mhe. Rajab Mbarouk Mohamed	Hapana
75.Mhe. Freeman Aikaeli Mbowe	Hakuwepo
76.Mhe. Tundu A.M. Lissu.....	Hakuwepo
77.Mhe. Said Amour Arfi	Hakuwepo
78.Mhe. Mch. Israel Y. Natse	Hakuwepo
79.Mhe. Susan A.J. Lyimo.....	Hakuwepo
80.Mhe. Vincent J. Nyerere.....	Hakuwepo
81.Mhe. Ezekia Dibogo Wenje.....	Hakuwepo
82.Mhe.Sylvester M.Kasulumbayi.....	Hakuwepo
83.Mhe. Prof. Kulikoyela K.Kahigi.....	Hakuwepo
84.Mhe.HalimaJ.Mdee	Hakuwepo
85.Mhe. Rose Kamil Sukum.....	Hakuwepo
86.Mhe. Mch.Peter S. Msigwa.....	Hakuwepo
87.Mhe. John John Mnyika.....	Hakuwepo
88.Mhe. Antony G. Mbassa	Hakuwepo
89.Mhe. Joseph O. Mbilinyi.....	Hakuwepo
90.Mhe. Highness S.Kiwia	Hakuwepo
91.Mhe. David Ernest Silinde.....	Hakuwepo
92.Mhe. Pauline Philipo Gekul.....	Hakuwepo
93.Mhe.Christina L.Mughwai.....	Hakuwepo

94.Mhe. Raya Ibrahim Khamis.....	Hakuwepo
95.Mhe. Sabreena H. Sungura.....	Hakuwepo
96.Mhe.Cecilia Daniel Paresso.....	Hakuwepo
97.Mhe. Conchesta L.Rwamlaza.....	Hakuwepo
98.Mhe. Joshua Samweli Nassari.....	Hakuwepo
99.Mhe.MwanamrishiT.Abama.....	Hakuwepo
100.Mhe. Maida Hamad Abdallah.....	Ndiyo
101.Mhe. Rashid Ali Abdallah	Hapana
102.Mhe. Munde Tambwe Abdallah	Ndiyo
103.Mhe. Bahati Ali Abeid	Ndiyo
104.Mhe. Abdul-Aziz Mohamed Abood.....	Ndiyo
105.Mhe. Chiku Aflah Abwao.....	Hakuwepo
106.Mhe. Khalfan Hilaly Aeshi	Ndiyo
107.Mhe. Rukia Kassim Ahmed.....	Hapana
108.Mhe. Lameck Okambo Airo	Ndiyo
109.Mhe. Mustapha B. Akunaay.....	Hakuwepo
110.Mhe. Abdalla Haji Ali	Hapana
111.Mhe. Juma Othman Ali	Ndiyo
112.Mhe. Mbarouk Salim Ali	Hapana
113.Mhe. Sara Msafiri Ally	Ndiyo
114.Mhe. Hussein Nassor Amar	Ndiyo
115.Mhe. Kheri Khatib Ameir.....	Ndiyo
116.Mhe. Abdallah Sharia Ameir	Ndiyo
117.Mhe. Abdulsalaam S. Amer	Ndiyo
118.Mhe. Amina Abdallah Amour	Hapana
119.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Ndiyo
120.Mhe. Iddi Mohamed Azzan	Ndiyo
121.Mhe. Mussa Zungu Azzan.....	Ndiyo
122.Mhe. Omary Ahmad Badwel	Ndiyo
123.Mhe. Faida Mohamed Bakar.....	Ndiyo
124.Mhe. Salum Khalfan Barwany	Hapana
125.Mhe. Elizabeth Nkunda Batenga	Ndiyo
126.Mhe. Gosbert Begumisa Blandes	Ndiyo
127.Mhe. Lolesia Jeremia Maselle Bukwimba	Ndiyo
128.Mhe. Ester Amos Bulaya	Ndiyo
129.Mhe. Selemani Said Bungara	Hakuwepo
130.Mhe. Felister Aloyce Bura.....	Ndiyo
131.Mhe. Agripina Zaituni Buyogera	Hapana
132.Mhe. Saidi Ramadhani Bwanamdogo	Hakuwepo
133.Mhe. Jerome Dismas Bwanausi	Ndiyo

134.Mhe. Josephine T. Chagulla	Ndiyo
135.Mhe. Kisyeri Werema Chambiri	Hakuwepo
136.Mhe. Dkt. Cyril August Chami	Ndiyo
137.Mhe. Mary Pius Chatanda	Ndiyo
138.Mhe. John Mwamose Cheyo.....	Ndiyo
139.Mhe. Hezekiah Ndahani Chibulunje	Ndiyo
140.Mhe. Capt. John Zefania Chillgati	Ndiyo
141.Mhe. Diana Mkumbo Chilolo	Ndiyo
142.Mhe. Muhammad Amour Chomboh	Ndiyo
143.Mhe. Amina Andrew Clement	Ndiyo
144.Mhe. Dkt. Maua Abeid Daftari	Ndiyo
145.Mhe. Mohamed Gulam Dewji	Hakuwepo
146.Mhe. Deo Haule Filikunjombe	Hakuwepo
147.Mhe. Josephine Johnson Genzabuke	Ndiyo
148.Mhe. Ali Juma Haji	Ndiyo
149.Mhe. Khatib Said Haji	Hapana
150.Mhe. Zahra Ali Hamad	Hapana
151.Mhe. Hamad Ali Hamad	Hakuwepo
152.Mhe. Azza Hillal Hamad	Ndiyo
153.Mhe. Asaa Othman Hamad.....	Hakuwepo
154.Mhe. Neema Mgaya Hamid	Ndiyo
155.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Ndiyo
156.Mhe. Maria Ibeshi Hewa	Ndiyo
157.Mhe. Mansoor Shanif Hiran	Ndiyo
158.Mhe. Agness Elias Hokororo	Ndiyo
159.Mhe. Yussuf Salim Hussein	Hapana
160.Mhe. Balozzi Seif Ali Idd	Hakuwepo
161.Mhe. Dkt. Christina G. Ishengoma	Ndiyo
162.Mhe. Yahya Kassim Issa	Ndiyo
163.Mhe. Waride Bakari Jabu	Ndiyo
164.Mhe. Jaddy Simai Jaddy	Ndiyo
165.Mhe. Selemani Saidi Jafo	Ndiyo
166.Mhe. Asha Mshimba Jecha	Ndiyo
167.Mhe. Juma Sururu Juma	Ndiyo
168.Mhe. Riziki Omar Juma	Hapana
169.Mhe. Abuu Hamoud Jumaa	Ndiyo
170.Mhe. Ritta Enespher Kabati	Ndiyo
171.Mhe. David Zacharia Kafulila	Hapana
172.Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu.....	Ndiyo
173.Mhe. Haji Khatib Kai	Hapana

174.Mhe. Naomi A.M. Kaihula	Hakuwepo
175.Mhe. Moshi Selemani Kakoso.....	Ndiyo
176.Mhe. Innocent Edward Kalogeris	Ndiyo
177.Mhe. Dkt. Titus M. Kamani.....	Ndiyo
178.Mhe. Vick Paschal Kamata	Ndiyo
179.Mhe. Josephat Sinkamba Kandege.....	Ndiyo
180.Mhe. Prof. Juma Athuman Kapuya	Ndiyo
181.Mhe. Mariam Reuben Kasembe.....	Ndiyo
182.Mhe. Rosweeter Faustin Kasikila	Ndiyo
183.Mhe. Eustace Osler Katagira	Ndiyo
184.Mhe. Vita Rashid Mfaume Kawawa	Ndiyo
185.Mhe. Zainab Rashidi Kawawa	Hakuwepo
186.Mhe. Gaudence Cassian Kayombo.....	Ndiyo
187.Mhe. Dkt. Kebwe Stephen Kebwe	Ndiyo
188.Mhe. Khalifa Suleiman Khalifa	Hapana
189.Mhe. Kheir Ali Khamis	Ndiyo
190.Mhe. Sadifa Juma Khamis	Ndiyo
191.Mhe. Yussuf Haji Khamis	Hapana
192.Mhe. Muhammed Seif Khatib	Ndiyo
193.Mhe. Aliko Nikusuma Kibona	Ndiyo
194.Mhe. Mendrad Lutengano Kigola	Hakuwepo
195.Mhe. Pudenciana Wilfred Kikwembe	Ndiyo
196.Mhe. Modestus Dickson Kilufi	Ndiyo
197.Mhe. Mkiwa Adam Kimwanga	Hapana
198.Mhe. Rosemary Kasimbi Kirigini	Ndiyo
199.Mhe. Mariam Nasoro Kisangi	Ndiyo
200.Mhe. Dunstan Luka Kitandula	Ndiyo
201.Mhe. Susan L.A Kiwanga.....	Hakuwepo
202.Mhe. Grace Sindato Kiwelu	Hakuwepo
203.Mhe. Silvestry Francis Koka	Ndiyo
204.Mhe. Capt. John Damiano Komba	Hakuwepo
205.Mhe. Mussa Haji Kombo	Hapana
206.Mhe. Kombo Khamis Kombo	Hapana
207.Mhe. Maulidah A.V. Komu	Hakuwepo
208.Mhe. Al-Shaymaa John Kwegyir	Ndiyo
209.Mhe. Michael Lekule Laizer	Ndiyo
210.Mhe. Godbless J. Lema.....	Hakuwepo
211.Mhe. Devotha Mkuwa Likokola.....	Ndiyo
212.Mhe. Dkt. Festus Bulugu Limbu	Ndiyo
213.Mhe. Alphaxard K. N. Lugola.....	Hakuwepo

214.Mhe. Riziki Said Lulida.....	Ndiyo
215.Mhe. Livingstone Joseph Lusinde	Ndiyo
216.Mhe. John Paul Lwanji	Ndiyo
217.Mhe. Sylvester Massele Mabumba	Ndiyo
218.Mhe. Moses Joseph Machali	Hakuwepo
219.Mhe. Betty Eliezer Machangu.....	Ndiyo
220.Mhe. Salvatory N. Machelili.....	Hakuwepo
221.Mhe. Zarina Shamte Madabida	Ndiyo
222.Mhe. Mwigulu Nchemba Madelu	Ndiyo
223.Mhe. John S. Magalle	Hakuwepo
224.Mhe. Catherine Valentine Magige	Ndiyo
225.Mhe. Ezekiel Magolyo Maige.....	Ndiyo
226.Mhe. Faki Haji Makame	Hapana
227.Mhe. Eng. Ramo Matala Makani	Ndiyo
228.Mhe. Amina Nassoro Makilagi	Ndiyo
229.Mhe. Anne Kilango Malecela	Ndiyo
230.Mhe. Annamarystella J. Mallac.....	Hakuwepo
231.Mhe. Ignas A. Malocha	Ndiyo
232.Mhe. Dkt. David Mciwa Mallole	Ndiyo
233.Mhe. Murtaza Ally Mangungu	Ndiyo
234.Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya	Ndiyo
235.Mhe. Abdul Jabiri Marombwa	Ndiyo
236.Mhe. Eng. Hamad Yussuf Masauni	Hakuwepo
237.Mhe. Augustino Manyanda Masele	Ndiyo
238.Mhe. Esther Nicholas Matiko.....	Hakuwepo
239.Mhe. Donald Kelvin Max.....	Ndiyo
240.Mhe. Lucy Thomas Mayenga.....	Ndiyo
241.Mhe. Kiumbwa Makame Mbaraka	Ndiyo
242.Mhe. James Francis Mbatia	Hapana
243.Mhe. Kuruthum J. Mchuchuli	Hapana
244.Mhe. Zakia Hamdani Meghji	Ndiyo
245.Mhe. Mariam Salum Mfaki	Ndiyo
246.Mhe. Athumani Rashid Mfutakamba.....	Ndiyo
247.Mhe. Subira Khamis Mgalu	Ndiyo
248.Mhe. Zabein Muhaji Mhita	Ndiyo
249.Mhe. Esther Lukago M. Midimu	Ndiyo
250.Mhe. Fatuma Abdallah Mikidadi.....	Ndiyo
251.Mhe. Desderius John Mipata.....	Ndiyo
252.Mhe. Mohamed Hamisi Missanga	Hakuwepo
253.Mhe. Faith Mohamed Mitambo	Ndiyo

254.Mhe. Margareth Agnes Mkanga	Ndiyo
255.Mhe. Dunstan Daniel Mkapa	Ndiyo
256.Mhe. Nimrod Elirehema Mkono	Ndiyo
257.Mhe. Felix Francis Mkosamali.....	Hapana
258.Mhe. Mustafa Haidi Mkullo.....	Ndiyo
259.Mhe. Rita Louise Mlaki.....	Ndiyo
260.Mhe. Martha Moses Mlata	Ndiyo
261.Mhe. Rebecca M. Mngodo.....	Hakuwepo
262.Mhe. Herbert James Mntangi	Ndiyo
263.Mhe. Mohamed Habib Juma Mnyaa	Hapana
264.Mhe. Ally Keissy Mohamed	Ndiyo
265.Mhe. Hamad Rashid Mohamed	Hakuwepo
266.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Ndiyo
267.Mhe. Luhaga Joelson Mpina	Ndiyo
268.Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda	Ndiyo
269.Mhe. Dkt. Augustine Lyatonga Mrema.....	Hakuwepo
270.Mhe. Maryam S. Msabaha.....	Hakuwepo
271.Mhe. Assumpter Nshunju Mshama	Ndiyo
272.Mhe. Saidi Mohamed Mtanda.....	Hakuwepo
273.Mhe. Abdul Rajab Mteketa	Ndiyo
274.Mhe. Abas Zuberi Mtemvu	Ndiyo
275.Mhe. Christowaja G. Mtinda	Hakuwepo
276.Mhe. Philipa G. Mturano	Hakuwepo
277.Mhe. Mtutura Abdallah Mtutura.....	Ndiyo
278.Mhe. Thuwayba Idrisa Muhamed.....	Hapana
279.Mhe. Joyce John Mukya.....	Hakuwepo
280.Mhe. Hasnain Mohamed Murji	Hakuwepo
281.Mhe. Benardetha Kasabago Mushashu	Ndiyo
282.Mhe. Mussa Hassan Mussa	Ndiyo
283.Mhe. Eugen Elishininga Mwaiposa	Ndiyo2
84.Mhe. Prof. David Homeli Mwakyusa.....	Hakuwepo
285.Mhe. Salome Daudi Mwambu	Hakuwepo
286.Mhe. Mch. Luckson Ndaga Mwanjale	Ndiyo
287.Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa.....	Ndiyo
288.Mhe. Clara Diana Mwatuka	Hapana
289.Mhe. Amina Mohamed Mwidau	Hapana
290.Mhe. Charles John Paul Mwijage	Ndiyo
291.Mhe. Hussein Mussa Mzee.....	Ndiyo
292.Mhe. Yusuph Abdallah Nassir.....	Ndiyo
293.Mhe. Richard Mganga Ndassa	Ndiyo

294.Mhe. Philemon Kiwelu Ndesamburo.....	Hakuwepo
295.Mhe. Dkt. Faustine E. Ndugulile	Hakuwepo
296.Mhe. William Mganga Ngeleja	Ndiyo
297.Mhe. Stephen Hilary Ngonyani	Ndiyo
298.Mhe. Cynthia Hilda Ngoye	Ndiyo
299.Mhe. Ahmed Juma Ngwali	Hapana
300.Mhe. Juma Abdallah Njwayo.....	Ndiyo
301.Mhe. Juma Selemani Nkamia	Ndiyo
302.Mhe. Said Juma Nkumba	Ndiyo
303.Mhe. Dkt. Lucy Sawere Nkya	Ndiyo
304.Mhe. Albert Obama Ntabaliba.....	Ndiyo
305.Mhe. Deogratias Aloyce Ntukamazina	Ndiyo
306.Mhe. Omari Rashid Nundu	Ndiyo
307.Mhe. Abia Muhama Nyabakari	Ndiyo
308.Mhe. Nyambari Chacha Nyangwine.....	Ndiyo
309.Mhe. Leticia M. Nyerere.....	Hakuwepo
310.Mhe. Tauhida Cassian Galos Nyimbo.....	Ndiyo
311.Mhe. Christopher O. Ole-Sendeka	Ndiyo
312.Mhe. Rashid Ali Omar	Hapana
313.Mhe. Asha Mohamed Omari	Hakuwepo
314.Mhe. Nassib Suleiman Omar	Ndiyo
315.Mhe. Meshack Jeremiah Opolukwa	Hakuwepo
316.Mhe. Lucy P. Owenya.....	Hakuwepo
317.Mhe. Saleh Ahmed Pamba	Ndiyo
318.Mhe. Ismail Aden Rage	Ndiyo
319.Mhe. Rachel M. Robert.....	Hakuwepo
320.Mhe. Mhonga Said Ruhwanya.....	Hakuwepo
321.Mhe. Mch. Dkt. Getrude Rwakatare	Ndiyo
322.Mhe. Jasson Samson Rweikiza	Ndiyo
323.Mhe. Mwanakhamis Kassim Said.....	Ndiyo
324.Mhe. Said Suleiman Said	Hapana
325.Mhe. Moza Abedi Saidy	Hapana
326.Mhe. Magdalena Hamis Sakaya	Hapana
327.Mhe. Kidawa Hamid Saleh	Ndiyo
328.Mhe. Ramadhani Haji Saleh	Ndiyo
329.Mhe. Masoud Abdalla Salim	Hapana
330.Mhe. Ahmed Ali Salum	Ndiyo
331.Mhe. Deo Kasenyenda Sanga	Ndiyo
332.Mhe. Muhammad Ibrahim Sanya	Hakuwepo
333.Mhe. Ali Khamis Seif	Hapana

- 334.Mhe. Joseph R. SelasiniHakuwepo
335.Mhe. Haji Juma SerewejiNdiyo
336.Mhe. Ahmed Mabkhut ShabibyNdiyo
337.Mhe. Abdulkarim Esmail Hassan ShahNdiyo
338.Mhe. Haroub Muhammed ShamisHapana
339.Mhe. Henry Daffa ShekifuNdiyo
340.Mhe. Beatrice Matumbo Shellukindo.....Ndiyo
341.Mhe. Fakharia Khamis Shomar.....Ndiyo
342.Mhe. Namelok Edward Moringe Sokoine.....Hakuwepo
343.Mhe. Jitu Vrajlal SoniNdiyo
344.Mhe. Suleiman Masoud Nchambi SuleimanNdiyo
345.Mhe. Shaffin Ahmedali Sumar.....Ndiyo
346.Mhe. Kaika Saning'o Telele.....Ndiyo
347.Mhe. Salim Hassan Abdullah Turkey.....Ndiyo
348.Mhe. Martha Jachi UmbullaNdiyo
349.Mhe. Zaynabu Matitu Vullu.....Ndiyo
350.Mhe. Anastazia James Wambura.....Ndiyo
351.Mhe. Godfrey Weston ZambiNdiyo
352.Mhe. Selemani Jumanne ZediNdiyo
353.Mhe. Said Mussa ZubeirNdiyo

SPIKA: Mtatupa muda kidogo ili tuweze kufanya *reconciliation*.

Tunapenda tuwatambue baadhi ya wageni waliopo hapa ambao ni timu ya *Stand United* ya Manispaa ya Shinyanga ambayo ni mabingwa wa Ligi Kuu,

Mkoa wa Shinyanga na waliokotoka Dar es Salaam wamefunga timu inaitwa *The France Ranges* mabao matatu kwa sifuri na hivyo kufuzu kucheza Ligi Daraja la Kwanza mwakani na ni wageni wa Mheshimiwa Stephen Masele, Naibu Waziri wa Nishati na Madini. Hawa ndiyo mabingwa wa Shinyanga. (*Makofi*)

Kesho Waheshimiwa Wabunge wote mtakapoingia Bungeni mtatumia mlango mkubwa huu kwa sababu mashine ya ukaguzi katika mlango wa kwenye *pigeon holes* imeharibika.

24 JUNI, 2013

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Spika, natumia Kanuni ya 68(7) ...

SPIKA: Samahani, Kanuni gani?

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Kanuni ya 68(7).

SPIKA: Ambayo inasemaje?

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Ndiyo Mheshimiwa Spika...

MBUNGE FULANI: Kaa chini.

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Spika, 68(7) inasema hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuendelea mbele, ushanifahamu?

SPIKA: Hakuna mwingine aliyekuwa anasema ndiyo maana nimekuita, endelea inasemaje?

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Mh! Jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusu au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye.

SPIKA: Mambo gani yaliyotokea yanayotaka kupata Mwongozo?

24 JUNI, 2013

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Spika, tulikuwa katika mfumo wa kupiga kura sasa hivi. Mfumo wenyewe ni wa 'Ndiyo' na 'Hapana' lakini katika hao ambao wanakubali 'Ndiyo' mgombewa wao ni Waziri wa Fedha na sisi ambao tulisema 'Hapana' tumekataa. Sasa tulikuwa tunahitaji, kwa sababu hizi kura zinaenda kuhesabiwa, kwa hivyo hatupati *agent* wa huku na huku ili tukahakikisha. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Haya, kwa sababu ni mambo ya Kanuni nitakujibu kesho. (*Makofi/Kicheko*)

Haya, tusikilize matokeo ambayo hayana wakala.

MATOKEO YA KURA

ND. JOHN JOEL – KAIMU KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, idadi ya Wabunge wote ambao walipaswa kuwepo Bungeni kwa sasa hivi ni 354. Wabunge ambao hawakuwepo Bungeni ni 83, Wabunge waliokuwepo na kupiga kura ni 270.

SPIKA: Waliopiga kura ni wangapi?

ND. JOHN JOEL – KAIMU KATIBU WA BUNGE: Waliokuwepo na kupiga kura ni 270. Kura za 'Hapana' ni 35 na kura za 'Ndio' ni 235. (*Makofi/Vigelegele*)

MHE. ALLY K. MOHAMMED: CUF oyeel!

ND. JOHN JOEL – KAIMU KATIBU WA BUNGE: Kwa mujibu wa Kanuni zetu kura za 'Ndio' zimezidi asilimia 50 ambayo ndiyo *quorum* ya Bunge kwa maana hiyo Bajeti Kuu ya Serikali imepitishwa rasmi. (*Makofi/Vigelegele*)

WABUNGE FULANI: CCM, CCM, CCM. (*Makofi*)

24 JUNI, 2013

MHE. ALLY K. MOHAMMED: *CUF* oyee!

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Kwa hiyo, kwa mujibu wa Katiba yetu, ni kwamba sasa bajeti ya Serikali ni halali. Naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza Waziri wa Fedha, Naibu Mawaziri wake, wataalam wote waliohusika na maandalizi ya bajeti hii na kwa namna ya pekee, Kamati yangu ya Bajeti ambayo iliingia kwa undani sana kujua haya makadirio yamekaa namna gani na hivyohivyo tuishukuru Serikali kwa kukubali kuja kwenye meza ya mazungumzo na mpaka tukafikia hapa tulipofikia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwangu mimi ni jambo ambalo nalionea fahari kwa sababu wingu la wasiwasi lilikuwa kubwa mno. Kama ukisikia kuna wingu la giza lilikuwa wingu la giza lakini tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa ushirikiano mzuri uliokuwepo kwa pande zote, Serikali na Waheshimiwa Wabunge, hadi tumeweza kufikia kitu ambacho ni cha namna yake. Kwa hiyo, Serikali sasa kuanzia tarehe 1 Julai, 2013 inaanza kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, ni mategemeo yetu kwamba utaratibu huu peke yake hauwezi kuwa na mafanikio mpaka kila mtu ashike hatamu zinazostahili. Hatamu moja ambayo mkikosea tu utaratibu utakuwa umefeli *miserable*, ni namna gani *revenue* itapatikana kwa wakati huo tuliotoa kazi. *(Makofi)*

Nadhani umesema mwenyewe katika mchango wako kwamba mnaangalia namna ya kuwa na utaratibu bora zaidi wa kuweza kupata mapato ambayo yanaweza kufanya kazi wakati wananchi wanaendelea kufanya kazi zao na ninyi mnaendelea kutafuta fedha. Kuna Mbunge

mmoja juzi alipochangia hapa alisema kwa nini hamwanganii uwezekano wa kuchukua fedha kwa mfano *BOT* au wapi mnatumia kwa nidhamu, wakati zinakusanywa zinaingia pale kusudi Serikali iondokane na lawama ya kutokupeleka fedha kwa wakati lakini wakati huohuo mwishoni *reconciliation* inakuwa kati ya huyo *BOT* na Serikali, lakini wananchi wanafanya kazi zao kwa utulivu na kwa nguvu zinazostahili kwa sababu nyenzo zipo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili suala mkiweza kulifanya hivyo, huu utaratibu utafanya kazi. *(Makofi)*

Kamati yangu ya Bajeti sasa sio kama imemaliza kazi, inaanza kufuatilia nyuma kule wanakofanya kazi kuona fedha yote inafanya kazi inayostahili na kwa wakati. Kwa hiyo, tutakuwa tunatembea hatua kwa hatua, Serikali ikikanyaga hapa na wenyewe wanakanyaga huku nyuma.

Kwa hiyo, ukweli tunachohitaji, ni nidhamu tu ya bajeti, fedha ndogo tulizonazo zifanye yale tuliyokusudia. Kama tutaweza kuongeza mapato yetu na tukawa kama wenzetu wengine basi tutakuwa tumefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mimi naomba niwapongeze wote walioshiriki katika kazi hii, bila ushirikiano tusingefanikiwa. Serikali imefanya kazi kubwa sana kujaribu kukubali kitu ambacho wamebadilishiwa katikati tu ya safari. Niwapongeze hasa watumishi wa Serikali, ndio waliotengeneza hata ratiba na ratiba ile ilifuatwa vizuri na tukafanya kazi yetu vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, mimi nasema tunapojadili bajeti, misimamo yetu ya kichama, haya ya kusema 'Ndiyo' au 'Hapana' sio muhimu sana, muhimu sana ni wakati tunajadili bajeti ni kwa maslahi ya watu wetu wale waliotupigia kura, wanaondokanaje na umaskini.

24 JUNI, 2013

Jambo lingine, bajeti peke yake nayo sio dawa. Nilimsikia Mheshimiwa Chomboh juzi alisema, bila sisi kufanya kazi, bila sisi kuwasimamia wananchi kufanya kazi katika maeneo yao, bajeti pia itakuwa haina maana kwa sababu kuna wengine wanafikiri sasa ni fedha za kupeana mkono kwa mkono, hamna, kila mtu azifanyie kazi ili ziweze kuzaa mara mbili ya hapo. Hapo tutakuwa tumefanya kazi nzuri sana.

Naomba katika Majimbo yenu, msione aibu kusema hivyo, hatutaondoa watu umaskini kwa kukaa tu hivi au mtu kupitisha kibakuli anaombaomba kila siku, hiyo inatudhallisha zaidi, tujaribu kuona kila mtu mahali pake anafanya kitu gani.

Waheshimiwa Wabunge, mimi sina matangazo mengine, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha na Serikali nzima kwa kupata Bajeti yake, kazi kubwa ni kuisimamia.

Kesho tunaendelea na ratiba nyingine, kama kawaida mtapata *Order Paper* asubuhi. Naomba niahirishe Kikao cha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 12.50 Jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 25 Juni, 2013, Saa Tatu Asubuhi)